ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi - Tarehe 4 Februari, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

KIAPO CHA UAMINIFU

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo

(Mheshimiwa aliyetajwa hapo juu alikula kiapo cha uaminifu na kukaa katika sehemu yake katika Ukumbi wa Baraza)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe wakati Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, anachukua nafasi yake na bahati nzuri amechukua nafasi karibu na Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa. Kwa hivyo, Waheshimiwa Mahmoud wawili wapo pamoja. (*Makofi*).

Ninachukua nafasi hii Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, nikukaribishe kwa dhati katika ukumbi wetu huu, ukumbi huu kwako ni mgeni kidogo lakini si mgeni wa Baraza la Wawakilishi, kwa sababu kabla ya hapo tulipokuwa Mnazi Mmoja eneo la Kikwajuni, jimbo la Mhe. Mahmoud mwenzio na wewe ulikuwa ni mjumbe katika Baraza lile kwenye kipindi kilichoishia 2010.

Kwa hivyo, nichukue nafasi hii nikukaribishe sana katika shughuli zetu za Baraza baada ya uchaguzi uliofanyika juzi siku ya Jumapili ambao Mungu amekujaalia kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki.

Kabla ya kuendelea na shughuli zetu Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, amekuja na ujumbe mzito ambao ulimsindikiza katika shughuli hii muhimu ya kuapishwa kwake. Wapo kati yao ambao ni wanafamilia na wengine ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mkoa na Wilaya anayotoka.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe naomba nitambue kuwepo kwake Bi. Zakia Mohamed, huyu ni mke wa Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, naomba vile vile mutambue kuwepo kwa mwana familia mwengine Bi. Zahra Mbamba, wengine kati ya wanafamilia ni Bi. Alkium Mbamba, wengine ni Bwana Kema, yupo vile vile Bi. Khadija Hassan na mwengine ni Bi. Faiza

Matishi, yule pale. Hao ni wana familia, ninakwambieni nyote karibuni sana katika ukumbi wetu huu.

Viongozi ambao waliofuatana na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi ambao nao wamekuja kushuhudia tukio hili muhimu la kuapishwa kwa Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Nao ni Ndugu Yussuf Mohamed Yussuf, huyu ni mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Magharibi. Katika Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Mjini/Magharibi umegaiwa katika mikoa miwili. Sasa huyu ni mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi katika Mkoa wa Magharibi wa Chama cha Mapinduzi.

Kiongozi mwengine aliyefuatana na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, ni Ndugu Abdalla Faki Shunda, huyu ni mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Dimani. Wilaya ambayo ndio iliyoshughulika na shughuli ya uchaguzi kwa upande wa CCM kwa Mhe. Mahmoud Thabit Kombo. Mwengine ni Ndugu Yahya Saleh Issa, huyu ni Katibu wa Wilaya ya Dimani.(*Makofi*).

Waheshimiwa Wajumbe ninaomba muwatambue wote hao wakiwa ni viongozi pamoja na wana familia. Lakini vile vile, naomba mutambue pia kuwepo kwa Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye naye amekuja kushuhudia shughuli hii.

Ninakushukuruni sana wanafamilia muliofuatana na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, lakini pia vile vile, ninakushukuruni viongozi mbali mbali wa Chama cha Mapinduzi, bila ya kumsahau Mhe. Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye naye amekuja kushuhudia tukio hili muhimu.

Kama kuna yeyote ambaye sikumtaja basi wote mutambue kuwepo kwenu na niwakaribishe sana katika shughuli zetu za Baraza la Wawakilishi.

Baada ya hapo karibuni munaweza kuendelea kuwepo mpaka wakati munaopenda ila tu pale tunapoahirisha shughuli zetu na nyinyi tunaomba kwa heshima zote mutoke nje tufunge milango yetu. Lakini munawea kuendelea kwa muda wote kushirikiana katika shughuli hizi katika nafasi ambazo mumepangiwa.

Baada ya hayo Katibu shughuli inaendelea.

Kabla hatujaanza shughuli hizo kwa kumkaribisha Mhe. Waziri wa Fedha pengine Mhe. Mahmoud Thabit Kombo ana neno la kusema, karibu.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ninamshukuru kwanza kabisa Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika siku hii ya leo. Lakini pili ninachukua fursa hii kukishukuru Chama changu Chama Chama cha Mapinduzi.

Na utaniwia radhi Mhe. Spika, naomba niseme CCM oyee! Kwa kunipa imani yao, wenzangu na kwa kunichagua kupitia demokrasia iliyokuwemo ndani ya Chama chetu Chama cha Mapinduzi na kuteuliwa kugombea nafasi ya Jimbo la Kiembesamaki na baada ya hapo ninawashukuru wananchi wote wa Jimbo la Kiembesamaki wakiongozwa na wana CCM kwa kunipa kura zao za ndio na kwa ushindi wa kishindo tuliopata. (*Makofi*).

Tatu, Mhe. Spika, naomba niwashukuru viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi, kuanzia ngazi ya Shina, Matawi yote ya Jimbo la Kiembesamaki, jimbo lenyewe, Wadi, Wilaya ya Dimani, Mikoa yote ambayo tumeshirikiana pamoja katika kupiga kampeni, vikao vya kitaifa vikiwemo Kamati Maalum na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM.

Mhe. Spika, pia, ninaomba nichukue fursa hii kuwashukuru ndugu zangu wote, familia yangu; kuanzia mke wangu Bi. Zakia ambaye yupo hapa pamoja na wana familia wote, maana tulikuwa tunakesha pamoja katika kupiga kampeni na kutafuta kura. Ninawashukuru sana kwa jitihada hiyo.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, ninakushukuru wewe pamoja na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na watendaji wako kuandaa mambo mazuri kama haya. Naomba niwashukuru Wawakilishi akinamama wa CCM kwa kuniandalia vitu vizuri kama hivi nilivyokuwa navyo hapa, na kwa kunisindikiza pamoja na Wawakilishi wa CCM wanaume wakiwa nao wanawasindikiza akinamama. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa hayo machache naomba nikushukuru tena wewe na watendaji wako wote kwa kuniapisha leo asubuhi na kuwa Mwakilishi rasmi na ninaomba kupitia Baraza lako nitoe tena shukurani zangu za dhati kwa wana Kiembesamaki wote kwa kunipa imani yao.
Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana karibu tena Mhe. Mahmoud tushirikiane na Wawakilishi wote waliomo ndani humu. Baada ya hayo sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Fedha.

TAARIFA ZA SERIKALI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Fedha): Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2012/2013.

Lakini Mhe. Spika, kabla sijachukua jukumu la kuwasilisha ripoti hii na mimi naomba nichukue wasaa huu kumpongeza sana Ndugu Mhe.Mahmoud Thabit Kombo, mwakilishi mpya wa Jimbo la Kiembesamaki. Jimbo hili kama unavyokumbuka Mhe.Spika, lilikuwa sehemu ya Jimbo la Dimani. Lakini kwa utaratibu mpya wa Tume ya Uchaguzi likakatwa na kuwa sasa jimbo kamili.

Aidha Mhe. Spika, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote waliomo ukumbini kushuhudia kumkaribisha Mhe. Mahmoud Thabit Kombo na kumuapisha na Waswahili wanasema, "Kweli ikidhihiri uwongo hujitenga". Sasa wenzetu walioamua kukaa nje, tunawaambia ndio wakubali demokrasi.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huu, sasa naomba niseme kazi au niwasilishe kazi uliyonipa.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa kwa mara nyengine tena kwa lengo la kupokea ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) tukiwa wenye afya njema. Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Fedha ninapenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuiwezesha Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Hesabu kuweza kufanya kazi zake kwa umahiri na uledi mkubwa.

Aidha, kupitia kwako naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya *PAC* inayoongozwa na mwenyekiti wake Mhe. Omar Ali Shekhe, Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake kwa kuisaidia sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoendeshwa kwa mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika kutushauri kwa njia ya kufanikisha utendaji wa majukumu ya serikali.

Kasoro zilizojitokeza

Mhe. Spika, katika ripoti ya mwaka 2012/2013 Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) iliweza kufuatilia ripoti tano za Mdhabiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Suala hili ni la

kupigiwa mfano sana, kwani kwa mara ya kwanza kamati hii imefanya kazi hiyo kwa wakati mmoja.

Tunathamini kwa dhati na jitihada na kazi nzuri iliyofanywa na kamati hii kwa kipindi hiki. Katika kipindi hiki ripoti zilizofanyiwa kazi ni kama hivi zifuatazo:-

1. Ripoti ya ukaguzi yakinifu wa miradi ya maendeleo ya wananchi na miradi ya TASAF kwa mwaka wa fedha 2009/2010.
2. Ripoti ya ukaguzi yakinifu ya udhibiti na uhifadhi wa mali za kudumu za serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010.
3. Ripoti ya ukaguzi wa hesabu kwa mawizara, mashirika na taasisi za serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010.
4. Ripoti ya ukaguzi wa hesabu kwa mawizara, mashirika na taasisi za serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011.
5. Ripoti ya ukaguzi yakinifu kwa miradi ya taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, kutokana na maoni ya kamati ilipokuwa ikichunguza ripoti hizo mambo yafuatayo yamejitokeza:-

1. Kutosimamiwa ipasavyo fedha za miradi ya maendeleo ya wananchi na matokeo yake matumizi ya fedha hizo yameachwa kwa wananchi ambao hawana uelewa wa masuala ya fedha.
2. Baadhi ya watendaji wa Kamati za Maendeleo zilizokuwa zinasimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi hawakuwa waaminifu katika kusimamia fedha za miradi hiyo, jambo lililopelelea kuwepo kwa migogoro mingi katika kamati zenyewe. Lakini pia maendeleo yaliyokusudiwa kukosekana kwa ukamilifu.
3. Fedha nyingi zimetumika kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na miradi ya *TASAF* lakini lengo la miradi hiyo baadhi yake haikufanikiwa ipasavyo kama ilivyokusudiwa.
4. Kamati za Maendeleo pamaoja na Kamati za Shehia zinashindwa kutekeleza sheria za fedha ipasavyo na wizara zinazohusika zimeshindwa kuwaelimisha wananchi hao, hali hii imepelekea miradi mingi ya wananchi kujengwa katika kiwango cha chini na baadhi ya miradi kufa kabisa.
5. Miradi mingi ya *TASAF* inayohusiana na ufugaji haikuendelea na imekufa kabisa mara tu baada ya miradi hiyo kukabidhiwa wananchi.
6. Taasisi nyingi za serikali bado zinakabiliwa na tatizo la kutokuwa na daftari la mali za kudumu za taasisi hizo na baadhi yao ambazo tayari wamekwishaanzisha madaftari hayo yana

mapungufu kadhaa ikiwa ni pamoja na kukosa taarifa muhimu zinazohitajika.

7. Bado hatimiliki imekuwa ni tatizo kwa baadhi ya taasisi za serikali ambapo tatizo la kukosekana kwa hatimiliki kwa mali za serikali linaendelea, kinachoishangaza kamati ni kwamba maombi ya kupatiwa hati hizo kwa taasisi za serikali yanachelewa wakati taasisi za watu binafsi sambamba na watu binafsi zinapata wepesi kwa kumiliki hatimiliki hizo.

8. Kamati imeshuhudia taasisi nyingi za serikali hazijaanzisha rasmi kitengo cha manunuzi. Tatizo kubwa linalokwamisha hatua hii kufikiwa ni pamoja na kutoajiriwa kwa maafisa manunuzi ambao kwa mujibu wa elimu zao na usimamizi wa vitengo hivi wana mchango mkubwa katika kuanzishwa kwake. Aidha, kwa zile taasisi zinazobahatika kuanzisha mpango huo bado zinakabiliwa na tatizo la kutofuata ipasavyo mpango huo.

9. Bado tatizo la kukosekana kwa vielelezo vya matumizi vya fedha ya serikali linaendelea. Aidha, kuna baadhi ya taasisi huisubiri kamati ili kuthibitisha vielelezo hivyo ambavyo wakati wa ukaguzi vimekosekana. Hii huleta tafsiri kwamba kamati hufanya kazi ithibitishe kuvunjwa kwa sheria ya fedha inayoelekeza vielelezo hutakiwa vipatikane mara tu fedha ya serikali inapotumika.

10. Utekelezaji wa miradi ya serikali bado haujazingatiwa kwa upana wake kwa maslahi ya taifa. Imeripotiwa kwamba kamati imebaini kwamba miradi mingi hutekelezwa bila ya kuzingatia sheria za fedha lakini pia hugeuka kuwa ni sehemu ya baadhi ya watendaji kujinufaisha kibinafsi.

Mhe. Spika, pamoja na kasoro za jumla zilizoainishwa na Kamati ya *PAC* lakini pia ripoti imeainisha kasoro zifuatazo:-

a) Kuchelewa kwa ufungwaji wa hesabu za mwaka kwa baadhi ya taasisi na kuchelewa kuwasilisha hesabu hizo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,

b) Udhaifu wa udhibiti wa ndani pamoja na jitihada zinazochukuliwa, nyingi za kasoro zinazojitokeza zinaashiria udhaifu katika usimamizi wa mali kutokana na kasoro katika udhibiti wa ndani. Moja ya sababu ya udhaifu huo ni udhaifu katika upatikanaji wa taarifa kwa uongozi, udhaifu katika ukaguzi

wa ndani na katika utekelezaji wa mapendekezo yake na katika vyombo (*organs*) mbali mbali vya utekelezaji; na

c) Udanganyifu katika viinua mgongo umejitokeza kwa baadhi ya wizara na taasisi kuongeza muda, kufanya udanganyifu wa viinua mgongo na kuongeza mishahara ya mwisho ya watumishi. Kufanya hivyo ni kwenda ni kinyume na taratibu za fedha za umma na utumishi serikalini, kuibebesha mzigo usiostahili serikali na ni dalili ya rushwa.

Hatua zilizochukuliwa

Mhe. Spika, maelezo haya ninayatoa ili kutimiza matakwa ya Kanuni ya 108 (15) ya Kanuni ya Baraza Toleo la mwaka 2012.

Mhe. Spika, naomba pia nieleze kwamba kwa jumla serikali inazipa uzito sana taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*). Taarifa ya mwaka 2011/2012 na 2012/2013 zimejadiliwa kwa kina na serikali na kutolewa muongozo mahususi kuhusiana na uimarishaji wa usimamizi wa fedha kwa ujumla na mapendekezo ya *CAG* miaka husika.

Wizara yangu pia iliandaa waraka na kuwasilisha serikalini kwenye mapendekezo ya namna ya kurekebisha kasoro zilizobainika na kuimarisha zaidi udhibiti na usimamizi wa fedha za umma. Ninafuraha kujuulisha Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kuwa serikali imekubaliana na mapendekezo hayo ambayo kimsingi yanaelekeza uwajibikaji zaidi wa Maafisa Wahasibu (Makatibu Wakuu), Wahasibu Wakuu wa mawizara na idara zinazojitegemea na Wakagunduzi wa Ndani.

Utekelezaji wa maelekezo hayo ni jambo la kuendelea. Lengo ni kuimarisha udhibiti wa ndani kwa kila wizara au idara inayojitegemea, kusimamia kwa ukamilifu ukusanyaji wa mapato ya kila wizara, kufuata kikamilifu matakwa ya sheria ya ununuzi na uondoaji wa mali za serikali.

Kuhakikisha kuwa malipo yanafanyika tu tunapokuwa na vielelezo husika, kudhibiti wizara au idara kujiingiza katika deni kinyume na matakwa ya sheria. Kuimarisha usimamizi wa ukadiriaji wa malipo ya kiinua mgongo na kuhakikisha ufungaji na uwasilishaji wa hesabu kwa wakati.

Muhtasari
Mhe. Spika, upeo wa maagizo ya serikali katika usimamizi wa fedha za umma ni mpana sana na unaendana na maelekezo ya Kamati ya *PAC*. Ni jukumu la watendaji wakuu wenye dhamana kutekeleza ipasavyo majukumu hayo.

Wizara yangu itafuatilia kwa karibu utekelezaji huo na haitosita kuchukua hatua zinazopaswa kwa watendaji watakaokiuka maagizo hayo.

Mhe. Spika, zaidi ya maelezo hayo ya jumla naomba pia nitoe maelezo juu ya maoni ya maelekezo ya Kamati ya *PAC* kwa maeneo mahususi.

1. **Usimamizi wa fedha za miradi midogo midogo ya wananchi**
Mhe. Spika, kwa ujumla utaratibu wa utekelezaji wa miradi midogo midogo umesaidia sana kukwamua baadhi ya matatizo yanayowagusa wananchi kabla ya kuanza utaratibu wa sasa wa mfuko wa maendeleo ya jimbo. Ni kweli kwamba kwa baadhi ya majimbo hujitokeza changamoto wakati wa utekelezaji kutokana na utendaji wa Kamati za Maendeleo za majimbo. Kwa sasa utaratibu wa kuwapatia wananchi fedha moja kwa moja haupo tena. Kufuatia kuanza kwa utaratibu mpya wa mfuko wa jimbo (*CDF*).

2. **Uendeleaji wa mradi wa *TASAF***
Mhe. Spika, suala hili ni muhimu na njia pekee ni kuimarisha ufumbuzi wakati wa uibuaji wa miradi katika ngazi ya wananchi. Mazingatio maalum yataekwa wakati wa utekelezaji wa awamu ya tatu ya *TASAF* ili kuepuka kasoro za awamu zilizopita.

3. **Ubora wa daftari la kudumu la mali za serikali**

Mhe. Spika, tayari wizara zote za SMZ zimeshaanzisha daftari ka kudumu. Hata hivyo, madaftari hayo sasa yatafanyiwa marekebisho ili yaendane na muundo mpya wa Wizara ya Fedha ulioanza kutumika mwezi wa Agosti mwaka jana. Wizara za serikali zinaendelea na zoezi la uwekaji thamani kwa mali za wizara tatu katika mwaka unaoendelea wa fedha kufuatia kukamilika kwa zoezi hilo kwa wizara nyengine tano.

4. **Upatikanaji wa hatimiliki kwa taasisi za serikali**

Mhe. Spika, urahisi wa upatikanaji hati kwa maeneo ya wananchi yanatokana na ukweli kwamba mengi ya maeneo hayo tayari yamepimwa, hivyo kurahisisha utowaji wa hati. Vile vile kwa upande wa maombi ya serikali, hasa kwa maeneo ya skuli na vituo vya afya, uchelewaji unasababishwa na wingi wa maeneo wenyewe, ugumu wa kukubaliana mipaka kati ya taasisi za serikali pamoja na vijiji na gharama kubwa za upimaji. Serikali inatambua

ugumu huo na inakusudia kuchukua hatua maalum za kuharakisha upatikanaji wa hati kadiri itakavyokamilika.

Mhe. Spika, sasa naomba kutoa maelezo ya maoni ya *PAC* kwa Wizara ya Fedha, ambapo ripoti ilitowa maoni mawili ambayo yanahitaji ufafanuzi. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

a) Kamati ilihimiza kulipwa kwa deni lililobakia la Shirika la Umeme la shilingi bilioni 1,317,770,425/= ili shirika liweze kupata fedha za kujiendesha na kusimamia vyema majukumu yake.

b) Kamati imesisitiza kuwa watalii walipie ada ya *Visa* moja kwa moja kwa kupitia benki. Mhe. Spika, tayari Wizara ya Fedha, *ZECO* na *ZAWA* zimekamilisha uhakiki wa deni linalodaiwa *ZAWA* na *ZECO*, kwa sasa deni hilo ni kubwa zaidi kuliko kiasi kilichoelezwa na *PAC*. Wizara imekubaliana na *ZECO* juu ya kutenga malipo maalum kila mwezi kuanzia mwezi wa Januari 2014 hadi hapo deni hilo litakapokamilika.

Aidha, kwa sasa utata wa ankara za malipo kutoka *ZECO* kwa *ZAWA* tayari umeshapatiwa ufumbuzi *ZAWA* itapaswa kulipa ankara zote mpya bila ya malimbikizo. Naomba ieleweke kwamba serikali imebeba jukumu la kulipa deni la siku zilizopita tu. *ZAWA* italazimika kuongeza jitihada za kukusanya mapato yake ili ilipie ankara kwa wakati.

Mhe. Spika, tayari nimetoa maelezo juu ya hatua iliyofikiwa katika kuanzisha utaratibu wa kukusanya ada ya *Visa* kwa kupitia benki. Maelezo hayo nimeyatoa katika kikao hiki wakati nikiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya kamati ya kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Kwa kuhitimisha Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kukushukuru tena wewe binafsi na wajumbe wote wa Baraza hili, kwa mashirikiano mnayoipa Wizara ya Fedha. Pia namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*, Mhe. Omar Ali Shehe pamoja na wajumbe wake wote wa kamati, kwa ushauri na maelekezo yao ambayo yanatusaidia sana katika kufanikisha majukumu yetu. Ni matarajio yangu kwamba ufafanuzi nilioutoa umewasaidia sana wajumbe kufahamu utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na kamati ya *PAC* katika mwaka uliopita wa 2012/2013. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

Mhe. Omar Ali Shehe: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*): Mhe. Spika, jambo lolote linaloanzwa kwa jina la Mwenyezi Mungu, hilo ni jambo lenye kheri na neema, na kinyume chake sio tu kwamba kukosa Baraka ya Muumbaji, lakini

pia huchangia sana katika makosa ya kulitenda jambo hilo. Nianzapo kuwasilisha hotuba yangu hii kwa jina la Mwingi wa Rehema, hunifanya niwe katika amani ya moyo na roho ya kuona kuwa, kweli kamati imejitahidi sana kutekeleza na kuyakidhi mahitaji ya wananchi.

Mhe. Spika, mara nyingi kama ilivyo desturi ya wenyeviti wenzangu wa Kamati za Kudumu, tusimamapo mbele ya Baraza hili, huwa tunatoa shukurani kwako. Tukuthibitishie tu kwamba, shukurani hizo sio maneno ya kusifu pekee, lakini hutoka katika udhati wa nyoyo zetu, kwa kufahamu kwamba, uteuzi wa kamati zetu, utekelezaji wa majukumu yake na hata kuwasilisha ripoti zake, ni mwili na roho baina yako wewe Mhe. Spika na kamati hizi. Kwa maana, kukosekana kwako na kukosekana mashirikiano yako, kamati zetu haziwezi kufanya kazi na wala hazitaweza kutoa ripoti iliyokamilika, ripoti ambazo mwananchi akizisikiliza, hatoamini kwamba, chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi na kamati zake, vipo kwa kumsaidia yeye na maisha yake ya kila siku.

Mhe. Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ambayo inapotamkwa kwa jina hilo, mtamkaji huwa rahisi sana kuitamka Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika, hushirikiana vizuri sana na kamati, na hutoa mchango usioweza kukosekana katika kazi za Kamati. Kwa hali hii, kukosa kuishukuru ofisi hii na watendaji wake wote, huwa ni koseo kubwa lisiloweza kusameheka kwa mara moja. Naamini kuwa, nafasi yangu hii kabla ya kutoa hutoba yangu, ina haki ya kuishukuru ofisi hii kwa kuthubutu kwake kutoa ripoti nzuri zenye kufichua udhaifu mkubwa katika matumizi ya fedha za serikali.

Mhe. Spika, sasa niwashukuru wajumbe wa kamati yangu ya *PAC*, juhudi zao za kufanya kazi bila ya kujali machofu, kufanya kazi bila ya kuendekeza posho, kufanya kazi kwa mashirikiano kumenipa imani kubwa sana na kujisikia raha kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Bila ya wao kunijengea imani hii, ingeendelea kuwa kazi hii ya Uenyekiti wa Kamati ya *PAC*, ni shubiri isiyopendwa kutumika, hata kama mtumiaji ni mgonjwa wa kutumia shubiri hiyo.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Kamati ya *PAC* yanatofautiana sana na kamati nyengine za kisekta. Mamlaka ya kuchunguza fedha za serikali, wakati wanaochunguzwa ni watendaji wa serikali hiyo, ni mamlaka mazito yanayopata msuguano mkubwa wa kufikia kazi zinazofanywa. Mamlaka haya yaliyokasimiwa na kanuni ya 118(2) ya kanuni za Baraza la Wawakilishi, ni mamlaka yanayohitaji uvumilivu, ushujaa, kujituma na kujitolea kwa kila hali.

Kwetu sisi tukitoa ripoti nzuri itakayopokelewa na kukubaliwa na Baraza hili, itakayopokea maoni na furaha ya wananchi na kurejesha imani yao kwa Chombo hiki, itakayoisaidia Serikali kuona udhaifu wa watendaji wake na itakayopendekeza hatua za kuchukuliwa kwa kutibu maradhi ya udhaifu huo, kwetu sisi hujawa na furaha isiyo na kifani, kuona na kuamini tu kwamba, kweli tumewatumikia wananchi wa nchi hii.

Mhe. Spika, kama ilivyo kwa Kamati nyengine za kudumu za Baraza, na kama inavyoelekezwa na kanuni ya 107 ya kanuni za Baraza, Kamati ya *PAC* nayo imeundwa na Waheshimiwa Wajumbe wenye kutambulikana kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Omar Ali Shehe	-	Mwenyekiti.
2.	Mhe. Fatma Mbarouk Said	-	Makamo Mwenyekiti.
3.	Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	-	Mjumbe
5.	Mhe. Rufai Said Rufai	-	Mjumbe
6.	Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mjumbe
7.	Mhe. Salma Mussa Bilali	-	Mjumbe
8.	Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	-	Mjumbe

Mhe. Spika, kama ilivyo kwa kamati nyengine za kudumu za Baraza na kama inavyoelekezwa na kanuni ya 107(7) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Makatibu wa Kamati wa Kamati ya *PAC* waliofanya kazi katika kamati ni:-

1. Ndg. Nasra Awadh Salmin; na
2. Ndg. Othman Ali Haji.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, amewasilisha ripoti mbili kwa Baraza la Wawakilishi, ambazo zote zimekabidhiwa kwa Kamati. Ripoti hizo ni:-

- Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2011/2012.
- Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, kwa mara ya kwanza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu amefanya ukaguzi katika sekta ya ardhi. Kwa niaba ya kamati yangu natumia fursa hii kumpongeza sana *CAG* kwa kulitupia macho eneo hilo muhimu na nyeti katika nchi yetu. Nampongeza kutokana na ukweli kwamba eneo la ardhi ni moja kati ya sekta inayoongoza kwa migogoro, lakini nampongeza

kutokana na ukweli kwamba kwa Zanzibar ardhi ni sehemu muhimu ya uchumi hasa katika sekta ya uwekezaji wa utalii nchini.

Mhe. Spika, ripoti nyengine ni Ripoti ya Ukaguzi wa Kawaida ya mwaka ambayo imegusa katika taasisi mbali mbali za umma.

Kwa masikitiko makubwa mara hii kamati yangu haikumudu kumaliza kupitia maeneo yote yaliyomo kwenye ripotii hizi, hii ilitokana na ufinyu wa muda na kwamba sekta ya ardhi pekee ambayo ni eneo nyeti lililochukuwa asilimia Thelanithini (30%) ya muda wa kamati. Wizara ya Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa upande wa Serikali za Mitaa kwa maana ya Halmashauri za Wilaya, Mabaraza ya Miji na Manispaa zilichukua asilimia Hamsini (50%), Idara Maalum ilichukua asilimia Kumi na tano (15%) na asilimia Tano (5%) ilichukuliwa na Idara ya Majenzi na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Hii ni kusema kuwa kwa awamu hii sehemu kubwa ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haikufanyiwa kazi.

Kwa ujumla, Kamati imeifanyia kazi Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Wizara moja kati ya Wizara zilizoripotiwa na ripoti hiyo na kamati imeweza kufanyia kazi asilimia sabiini (70%) ya Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu.

YALIYOMO KWENYE HOJA ZA MDHIBITI NA MAJIBU YA KAMATI

Mhe. Spika, wajumbe wako wanazo ripoti za Mdhibiti na Ripoti ya Kamati katika kufuatilia majibu ya hoja ya Mdhibiti.

Ripoti ya Mdhibiti imeonesha sura tofauti katika Ukaguzi wa kawaida na Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu za mwaka 2011/2012.

Kwa upande wa Ripoti ya Ukaguzi wa Matumizi ya fedha za umma kwa mwaka huo hoja zifuatazo ziligusa katika maeneo mbali mbali:-

1. **Matumizi ya Fedha za Umma Yasiyofuata Utaratibu wa Sheria za Fedha na Sheria ya Manunuzi za mwaka 2005.**

Mhe. Spika, kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, jumla ya Tsh. 2,234,880,487.92, ziliripotiwa kutumika kinyume na utaratibu wa sheria.

Taasisi zilizoguswa kwa viwango tofauti ni:-

- Chuo cha Mafunzo
- Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM)
- Kikosi cha Valantia
- Mkoa wa Mjini Magharib
- Halmashauri ya Wilaya ya Magharib
- Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A'
- Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
- Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
- Mamlaka ya Mafunzo ya Amali
- Wizara ya Afya
- Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati
- Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano
- Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA)
- Mamlaka ya Maji (ZAWA)-Pemba; na

Aidha, taasisi zilizoguswa na ambazo zilipata fursa ya kufika mbele ya kamati na kujibu hoja ni:-

- Chuo cha Mafunzo
- Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM)
- Mkoa wa Mjini Magharib
- Halmashauri ya Wilaya ya Magharib
- Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A'
- Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati
- Mamlaka ya Maji (*ZAWA*)-Pemba

Vile vile, Jumla ya Tsh. 2,410,226,559 na *USD* 354 ziliripotiwa kulipwa bila ya vielelezo (nyaraka pungufu). Taasisi zilizoguswa ni:-

i. Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM),
ii. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi,
iii. Chuo cha Mafunzo,
iv. Baraza la Manispaa,
v. Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho,
vi. Wizara ya Afya; na
vii. Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

Kwa upande wa yaasisi ambazo zilipata fursa ya kufika mbele ya kamati na kujibu hoja hizo ilikuwa ni ile ile:-

i. Kikosi cha Kuzuia Magendo,
ii. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi,
iii. Chuo cha Mafunzo,
iv. Baraza la Manispaa,
v. Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho,
vi. Wizara ya Afya; na
vii. Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Hivyo, jumla ya Tsh**.** 996,237,291 zimethibitika kukosa vielelezo kufuatia kazi ya kamati.

2. Taasisi kutowasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa ajili ya ukaguzi

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2005 kila Taasisi ya umma inapaswa kufunga hesabu na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ukaguzi wa Mdhibiti na Uchunguzi wa kamati umebaini kuwa kuna baadhi ya Taasisi zetu hazifungi hesabu ya mwisho wa mwaka kama sheria inavyoelekeza.

Tatizo hilo ni kubwa zaidi katika Serikali za Mitaa na Taasisi nyengine kama vile Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar, Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Shirika la Umme, Chuo cha Kilimo cha Kizimbani nakadhalika. Vile vile, zipo taasisi ambazo hufunga hesabu za mwisho wa mwaka nje ya muda uliowekwa na Sheria ya Fedha ya mwaka 2005. Baadhi ya Taasisi hizo ni Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Jeshi la Kujenga Uchumi, Mkoa wa Kaskazini – Pemba, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais nakadhalika (Majibu na hoja yako Ukurasa wa 24 hadi 63 wa ripoti ya Kamati). Kwa hoja hiyo, Kamati ilipata fursa ya kuonana na Halmashauri, Mabaraza ya Miji Manispaa.

3. Mali za Serikali Kukodishwa kwa Maslahi Binafsi

Mhe. Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amebaini kuwa Taasisi za Serikali hukodisha mali za serikali kinyume na matakwa ya sheria namba 9 ya mwaka 2005 inayohusiana na Ununuzi na Ugavi wa Mali za Serikali.

Kamati ya *PAC* imelithibitisha hilo wakati wa uchunguzi wake. Kitendo hiki kinapekelea upotevu mkubwa wa fedha za umma. Baadhi ya taasisi zilizobainika na kadhia hiyo ni;

i. Mikoa yote miwili ya Pemba juu ya ukodishwaji wa Vituo vya Mafuta, (Ukurasa wa 38 na 43 wa ripoti ya kamati inapatikana taarifa hiyo); na

ii. Idara ya Ardhi na Usajili kuhusiana na kuwapunguzia kodi za ardhi au kuwaongezea '*grace period*' wawekezaji kinyume na sheria (kuanzia ukurasa wa 89 wa ripoti yetu)

4. Madeni kwa Taasisi za Umma

Mhe. Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Kamati kwa ujumla imebaini kuwa baadhi ya Taasisi za Umma zinakabiliwa na madeni makubwa. Madeni haya ni ya muda mrefu na miongoni mwa madeni hayo yameshakuwa hayalipiki tena.

Miongoni mwa taasisi zinazofanyiwa kazi na kamati na kukabiliwa na madeni hayo ni:-

i. Vikosi vya SMZ. Kwa mfano, Kikosi cha Valantia kinadaiwa Tsh. 252,625,000; Kikosi cha JKU kinadaiwa Tsh. 149,115,200; Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kinadaiwa Tsh. 120,631,000; Chuo cha Mafunzo kinadaiwa Tsh. 215,800,973 na kufanya jumla ya madeni yote ya Vikosi kuwa ni Tsh. 738,172,173; na

ii. Wizara ya Miundombinu na Wawasiliano inadaiwa Tsh. 266,814,550.

Pamoja na hayo, madeni yote yaliyoripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ni Tsh.3,595,056,399.6.

Mhe. Spika, taasisi hizi nne tu nilizozitaja zinadaiwa jumla ya Tsh. 1,004,986,723, hali hii inasikitisha sana na inatia aibu, lakini pia kuwepo kwake ni kinyume na mfumo sahihi wa kiuhasibu unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu ambao unatumika kwa Mawizara ya Serikali.

Mhe. Spika, kamati yetu inasikitishwa sana na serikali kama vile inavyosikitishwa na Wizara ya Fedha kutolitia mkazo suala la madeni kwa Taasisi za Serikali. Mhe. Spika, Kamati yetu mwaka 2011/2012, ilifanya juhudi kubwa sana ya kufuatilia suala zima la madeni ya Taasisi za Serikali, kwa kukaa pamoja na Taasisi zote zenye madeni sugu, kukaa pamoja na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hata Wizara ya Fedha, kushirikiana kwa karibu na Afisi ya Baraza la Wawakilishi na hatimae kuikabidhi ripoti ya madeni hayo kwa Mhe. Waziri wa Wizara ya Fedha, ili

kwa kutumia sheria ya fedha za umma, namba 12 ya mwaka 2005 awasilishe taarifa hiyo Barazani ili kufutwa kwa madeni yasiyolipika tena.

Mhe. Spika, kamati yetu inasikitishwa na ahadi za kila siku za wizara hii juu ya kuwasilisha taarifa ya madeni hayo Barazani, huku bado kamati inaendelea kupokea taarifa zisizopendeza kwamba, baadhi ya wafanyabiashara tayari wanakuwa wameshalipwa na Wizara ya Fedha huku pia wakipokea malipo kutoka katika taasisi husika.

Kuna tatizo Mhe. Spika, wenye madeni hawa huenda Wizara ya Fedha wakachukua fedha, na hapo kunakuwa na malipo ya mara mbili.

Mhe. Spika, hali hii haiwasaidii wananchi wetu, na ni hasara kwa serikali, lakini inapoendelea kuwepo, inaashiria mambo mengi yasiyopendeza. Mhe. Spika, kamati yetu bado inaitaka serikali kuwa na mikakati madhubuti katika kulishughulikia suala la madeni.

5. Suala la Ripoti ya *CAG* kuchukuliwa hatua na Serikali kabla ya kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi

Mhe. Spika, mbali na maelekezo ya Katiba ya kueleza kwamba, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iwasilishwe katika Baraza la Wawakilishi, ikiwa kwa njia ya kupitia kwa Mhe. Rais ama kupitia kwako wewe Mhe. Spika wa Baraza hili. Serikali yetu kupitia taasisi zake mbali mbali imekuwa ikichukua hatua kwa ripoti hizo hata kabla ya kuwasilishwa hapa Barazani.

Mhe. Spika, baada ya ripoti hizo za Mdhibiti kuwasilishwa Barazani, kamati yetu hukabidhiwa kwa lengo la kuifanyia kazi, lakini kamati yetu pia imeshuhudia taasisi mbali mbali za serikali huchukua hatua ya kufikisha mahakamani hoja mbali mbali zilizoibuliwa na Mdhibiti, huku kwa mujibu wa kanuni ya 108(17) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la 2012, kamati yetu hupata kikwazo cha kulishughulikia suala hilo.

Hoja yetu sio serikali kuchukua hatua, bali hoja yetu ni kukiukwa kwa taratibu kwa kulizuiya Baraza kupitia kamati zisifanyie kazi kwa kukosa vielelezo vilivyoko Polisi au Mahakamani.

Mhe. Spika, mfano wa mambo ambayo yameshindwa kufanyiwa kazi vizuri na Kamati kwa kuharakishwa jambo kufikishwa Mahakamani ni pamoja na;

i. Mkoa wa Kusini Unguja kuhusiana na wizi wa fedha za wazee wasiojiweza, zenye thamani ya Tsh. 47,939,150/-. Hivyo kamati

ilishindwa kwa sababu tayari wao walichukua hatua ya kupeleka polisi; na

ii. Idara ya Majenzi na Utunzaji wa Nyumba kuhusiana na wizi wa Tsh.57,000,000.

Kwa mnasaba huo, tunapenda kuliarifu Baraza hili kuwa Kamati yetu imeshindwa kupitia baadhi ya hoja hizo kutokana na vikwazo nilivyovieleza hapo awali.

RIPOTI YA UKAGUZI YAKINIFU KWA MIRADI YA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR, YA MWAKA 2011/2012.

Mhe. Spika, kama tulivyotanguliza kueleza awali kuwa, kamati yangu imefanyia kazi ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ya mwaka 2011/2012, ambayo kwa sehemu kubwa imegusia katika ukaguzi wa eneo la ardhi.

Uchambuzi wa majibu na hoja, yamo kwenye ripoti ya Kamati ambayo ni imani yangu kuwa, kila mjumbe kapata muda wa kuipitia na kuifahamu kwa undani majibu ya kila hoja. Hata hivyo, kwa ujumla, hoja za Mdhibiti na uchunguzi wa kamati katika Ukaguzi Yakinifu, katika sekta ya ardhi iligusia katika maeneo yafuatayo:-

1. **Hoja ya serikali kufuta ardhi kwa wawekezaji, bila ya kufuata utaratibu ama kushindwa kwa wawekezaji kuyaendeleza maeneo husika.**

Mhe. Spika, hoja hii iligusa kufutwa kwa umiliki wa ardhi katika maeneo mbali mbali ya uwekezaji kama yanavyoonekana katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na kama majibu ya hoja yanavyoonekana katika ripoti ya kamati.

Kimsingi uchunguzi wa kamati umebaini kuwa, ufutaji wa baadhi ya maeneo ulifuata utaratibu wa sheria na baadhi ya maeneo haukufuata sheria. (majibu ya hoja yako kwenye ukurasa wa 145 hadi 156).

2. **Hoja ya wawekezaji kupewa ardhi na kutoiendeleza kwa kipindi kirefu**

Mhe. Spika, hoja hii iligusa maeneo yapatayo 119 ambayo yametolewa kwa wawekezaji kwa lengo la kuyaendeleza maeneo hayo ambayo licha ya Serikali kufaidika kupitia malipo ya ardhi, mategemeo ya serikali ni kupata

faida kubwa ya kodi mbali mbali kupitia uwekezaji huo pamoja na ajira kwa wananchi.

Mhe. Spika, uchunguzi wa kamati umebaini kuwa, ni kweli kuna maeneo yametolewa kwa kipindi kirefu na yameshindwa kuendelezwa hadi sasa na hivyo kuitia hasara kubwa Serikali. Kushindwa kuendelezwa kwa maeneo hayo, kunatokana na sababu tofauti kama vile:-

i. Wawekezaji kutokuwa na uwezo. Wawekezaji wanaopewa ardhi yetu imebainika kwamba wengi hawana uwezo,

ii. Pingamizi za Kimahakama. Pingamizi hizi za Kimahakama zimepelekea kwa kweli baadhi ya wawekezaji kushindwa kuendeleza, kwa sababu mashauri yako mahakamani; na

iii. Migogoro kati ya wawekezaji, wawekezaji na wananchi ama wawekezaji na wizara.(Waheshimiwa Wajumbe majibu ya hoja hii yako kwenye ukurasa wa 117 hadi 129)

3. Madeni ya ardhi ya muda mrefu kwa miradi ya mahoteli na miradi mengineyo ya uwekezaji na serikali

Mhe. Spika, Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu, kama ilivyoripotiwa na kamati katika ukurasa wa 113 na 139 imegusia hoja za madeni ya ardhi ya muda mrefu ambapo taasisi iliyopewa mamlaka ya ukusanyaji wa kodi hizo *ZRB* ilikuwa haifanyi kazi ipasavyo katika kuzikusanya kodi hizo.
Uchunguzi wa kamati umebaini kuwa, kurundikana kwa madeni kunatokana na sababu tofauti kama vile:-

i. Tatizo la usimamizi,

ii. Kutoingizwa katika mtandao wa ulipaji kodi kwa baadhi ya wawekezaji; na

iii. Kutosajiliwa kwa ardhi kwa baadhi ya Miradi ya Uwekezaji. (majibu ya hoja yapo katika ukurasa wa 113 hadi 116 na ukruasa wa 139 hadi 145).

4. Wawekezaji kutumia ardhi bila ya kulipia kodi

Mhe. Spika, hoja hii imegusa maeneo yaliyotumika na wawekezaji kwa ajili ya ujenzi wa jeti. Hata hivyo, uchunguzi wa kamati umebaini kuwa, licha ya jeti kuna maeneo yametumika kwa ujenzi wa mahoteli na sehemu nyengine za

uwekezaji kama vile ujenzi wa chumba cha chini ya bahari, bila ya kuwa na *lease* na hivyo kutolipia kodi ya ardhi. Mapungufu haya ya usimamizi yamesababisha hasara kubwa kwa serikali, (majibu ya hoja yapo ukurasa wa 98 hadi 104).

5. Hoja ya kodi za ardhi kutofanyiwa mapitio

Mhe. Spika, ukaguzi umebaini kuwa, kwa kipindi cha miaka kumi, tokeao 2003 hadi 2013, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati imeshindwa kuzifanyia mapitio kodi za ardhi kwa lengo la kuzifanya ziendane na hali halisi ya soko (*current market value*).

Kawaida, wizara ilitakiwa kufanya mapitio ya bei (*Land Rent Review*) kila baada ya miaka mitatu. Hilo halikufanyika, lakini baya zaidi hata pale ilipofanya mapitio baada ya miaka 10, haikuzingatia tofauti ya muda uliopita ambapo ilipaswa iwe ni zaidi ya mara tatu kwa kipindi cha miaka 10 kupita.

Mhe. Spika, kitendo cha wizara kutozifanyia mapitio bei za ardhi, kimeitia hasara kubwa serikali. (majibu ya hoja yapo ukurasa wa 104 hadi 105).

6. Hoja ya Idara ya Ardhi ya Kutokuwa na Kumbukumbu kwa Baadhi ya Maeneo Yaliyotolewa kwa Wawekezaji.

Mhe. Spika, uchunguzi wa kamati umebaini pia kwamba Wizara kupitia Idara ya Ardhi wamekosa kuwa na kumbu kumbu kwa baadhi ya maeneo waliyoyatoa kwa wawekezaji hasa kwa kisiwa cha Pemba. Hali hii si tu imetutia mashaka, bali pia inadhihirisha kiwango duni cha watendaji wetu katika maeneo haya.

Kamati yangu imetoa muda wa miezi mitatu, ili ikabidhiwe orodha hiyo kwa ajili ya kuifanyia kazi.

H**ali ya Jumla na Mambo Mengine Muhimu Yaliyojitokeza Katika Uchunguzi**

Mhe. Spika, kwa ujumla Kamati ya *PAC* katika uchunguzi wake wa hoja mbali mbali za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu katika Ripoti zote mbili na maeneo iliyofanikiwa kuyachunguza imebaini mambo yafuatayo:

1. Watendaji Kuendelea Kukiuka Taratibu za Matumizi ya Fedha za Umma

Mhe. Spika, uchunguzi unaendelea kuonesha kwamba baadhi ya watendaji wanaendelea kukiuka taratibu za matumizi ya fedha za umma na hivyo,

kuingiza serikali hasara kubwa na kuwabebesha mzigo mzito walipa kodi ambao ni wananchi wetu wanyonge.

Hali hii inaendelea licha ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuchukuwa juhudi kubwa ya kuandaa ripoti kila mwaka na kuziwasilisha mbele ya Baraza hili na Kamati kutoa mapendekezo kadhaa ya kufanyiwa kazi na serikali.

Mhe. Spika, serikali kuendelea na tabia yake ya kutokuwachukulia hatua madhubuti kwa wahusika ni sawa na kuvibariki vitendo hivyo na kuwalea wanaofanya vitendo hivyo.

Katika eneo hili la watendaji kukiuka kwa makusudi taratibu za matumizi na manunuzi. Kamati yangu inaendelea kutoa wito kwa serikali ichukuwe hatua zinazoonekana na zinazoelekeza kwa watendaji wanaojihusisha na vitendo hivyo.

2. Mapungufu ya Sheria ya Fedha, Sheria ya Manunuzi, Sheria ya Ardhi, Sheria ya Uwekezaji, Pamoja na Kutokuwepo kwa Sheria ya Serikali za Mitaa, Sheria ya Mitaji ya Umma, Kanuni za Ardhi na Sera

Mhe. Spika, mbali ya mapungufu ya watendaji na kiutendaji, eneo jengine linalosababisha usumbufu mkubwa na hivyo, wakati mwengine kuwapa mwanya watendaji, ni mapungufu yaliyomo ndani ya sheria zetu mbali mbali zinazohusika na sekta husika. Ni ukweli kuwa sheria nyingi haziendani na wakati wa sasa na hivyo, kuleta ukinzano katika utekelezaji wake. Kamati yangu inaishauri serikali kuchukuwa hatua za haraka za kufanya mapitio na kuzifanyia marekebisho sheria hizo ili ziendane na mazingira halisi pamoja na kuendana na Sera za Serikali.

3 Uwezo Mdogo wa Maafisa Wahasibu *(Accountants)* wa Serikali za Mitaa Pamoja na Kutokuwepo Wakaguzi wa Ndani

Mhe. Spika, uchunguzi umethibitisha kwamba matumizi mabaya ya fedha za wananchi katika Serikali za Mitaa pamoja na mambo mengine kama vile mapungufu ya Sheria, yanachangiwa pia na uwezo mdogo wa Maofisa Wahasibu ambao kawaida huteuliwa na Mhe. Waziri, anayehusika na wizara hii.

Kamati yangu inatoa wito kwa serikali kwamba, katika mchakato wake wa kuelekeza nguvu na kuziimarisha Serikali za Mitaa, basi izingatie zaidi kuteuwa watendaji wenye uwezo na sifa kama vile inavyofanya kwa wahasibu wa taasisi hizo.

Tunaishukuru serikali kwamba sasa hivi katika Serikali za Mitaa wanapeleka wahasibu ambao wanakuwa na uwezo. Kwa hivyo, hilo tunaliomba pia na makatibu wa taasisi hizo nao wawe ni watu wenye uwelewa katika kuendeleza kazi zao.

4. Matumizi Ovyo na Holela na Yasiyofuata Taratibu ya Fedha Katika Fungu la Mfuko Mkuu wa Serikali

Mhe. Spika, uchunguzi wa Kamati yangu umebainisha matumizi yasiyofuata utaratibu wa fedha zinazoidhinishwa na Baraza hili katika Fungu la Mfuko Mkuu wa Serikali. Sote tunashuhudia jinsi fungu hili linavyononeshwa kila mwaka. Ukiacha mbali na hoja iliyoguswa katika Ripoti ya Mdhibiti ya mwaka 2011/2012 ya ujenzi wa Kituo cha Mnara wa Bungi ambazo ni mnasaba wa fedha zilizoibiwa Idara ya Majenzi, fedha kutoka katika fungu hili hasa zinazohusiana na miradi mingi ya ujenzi na manunuzi ya vitu mbali mbali, matumizi yake hayafuati utaratibu wa sheria.

Mhe. Spika, Kamati yangu inatoa wito kwa Wajumbe wa Baraza na Ofisi ya Mdhibiti Mkuu kuwa makini sana na matumizi katika fungu hili. Aidha, tunatoa wito kwa serikali kuwa makini sana na matumizi ya fedha katika fungu hili kubwa la nchi.

5. Uwezo wa Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*)

Mhe. Spika, kuna umuhimu mkubwa kwa Bodi ya Mapato Zanzibar kuwa na uwezo katika kukagua mifumo ya kihesabu katika maeneo ya uwekezaji pamoja na umuhimu wa *ZRB* kutumia Mashine Maalum za '*Electronic Fiscal Devices' – EFD* kama vile *'Electronic Tax Register' – ETR, 'Electronic Fiscal Printer' – EFP na 'Electronic Signature Devices' – ESD* katika kukusanya kodi. Moja kati ya magonjwa makuu yanayoikumba nchi yetu kwa sasa ni tatizo la ukusanyaji wa kodi hasa hasa katika sekta ya uwekezaji wa mahoteli ya kitalii.

Utafiti usio rasmi uliofanywa na Kamati yangu wakati ikichunguza hoja ya ardhi katika uwekezaji. Mhe. Spika, umeonesha kwamba kodi inayokusanywa katika sekta ya ardhi na uwekezaji wa mahoteli ya kitalii haizidi asilimia ishirini na tano (25%) tu. Hali hii tumebaini inachangiwa na udanganyifu wa wawekezaji kufunga mashine na kuweka mifumo ya kihasibu ambayo watendaji wa *ZRB* hawana uwezo wa kuingia kwa undani katika kubaini uhalisia wa mapato na kodi inayostahiki.

Pamoja na uwezo wa Maofisa. Pia, mfumo wa ukusanyaji kodi hauna budi kuimarishwa kwa kufungwa kwa mashine hizo ambazo kwa sasa zinapatikana

nchini kwetu pamoja na kuwekwa kwa mifumo ya kihesabu inayokubaliwa na *ZRB.*

6. Kusuasua kwa Kituo cha Uwekezaji '*One Stop Centre'* Kunakochangia Matumizi Mabaya ya Ardhi.

Mhe. Spika, azma kubwa ya serikali ya kuanzisha *'One Stop Centre'* ni kuondosha urasimu katika kuhamasisha wawekezaji nchini.

Uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa mpango huu ni nadharia ambayo utekelezaji wake umekuwa ni mgumu, kwa vile hadi sasa ni taasisi chache tu ndizo zinazokutana katika kujadili na bila ya kufikia maamuzi kwa vile wawakilishi katika kituo hicho wengi wao ni wale wasiokuwa na maamuzi.
Mhe. Spika, mbali ya tatizo la ushiriki na udhaifu katika kushiriki, uchunguzi umebaini kukiukwa kwa sehemu kubwa ya taratibu katika uwekezaji kutokana na kutokuwa na mashirikiano, migongano na kutoaminiana kati ya Taasisi moja na nyengine.

Katika kuvutia na kuimarisha sekta ya uwekezaji nchini. Kamati yangu inatoa wito kwa serikali kufanya mapitio juu ya washiriki wa kituo hichi, pamoja na sera ya uwekezaji ili lengo liendane na uhalisia katika utekelezaji wake.

7. Kuwepo kwa Wawekezaji Ambao Ama Shughuli Zao ni Kinyume na Maombi ya Mwekezaji Ama Kutojuulikana kwa Shughuli Wanazofanya Nchini.

Mhe. Spika, ni ukweli kwamba kuna faida na fursa kubwa kwa nchi kufungua milango kwa ajili ya kuvutia na wawekezaji. Fursa hiyo inaweza kutumika vibaya na wawekezaji na badala ya nchi kupata faida ya uchumi, inaweza kugeuka na ikawa ni majanga kwa nchi iwapo serikali haikuwa makini katika kuratibu na kusimamia wawekezaji pamoja na watendaji ambao si waaminifu.
Mhe. Spika, uchunguzi wa Kamati yangu katika kufuatilia hoja ya ardhi katika maeneo ya uwekezaji umebaini kuwa, kuna baadhi ya wawekezaji shughuli zao ni tofauti na zile zilizomo kwenye maombi yao. Vile vile, kuna wawekezaji ambao wamekaa nchini kwa kipindi kirefu bila ya kuwa na shughuli yoyote wanayofanya, tena bila ya kulipia kodi ya ardhi na kodi nyengine yoyote.

Mhe. Spika, Kamati yangu imefedheheshwa sana na suala hili na hivyo, kuomba mambo yafuatayo yafanyike:

1. Kuwe na usimamizi makini katika chombo chetu cha *ZIPA.* Inaonekana kuwa *ZIPA* ni legelege, moja katika shauri tunalotoa kuwa na usimamizi makini kwa *ZIPA.*

2. Kufanya mapitio ya sera na sheria za uwekezaji.

3. Kuimarishwa kwa kituo cha uwekezaji *'one stop centre'*.

4. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu aelekeze nguvu katika ukaguzi kwa miradi yote 547 ya uwekezaji iliyopo Zanzibar.

8. Kuwepo kwa Madeni ya Muda Mrefu Katika Taasisi za Umma.

Mhe. Spika, tatizo la madeni katika Taasisi zetu, bado linaendelea kuziandama Taasisi nyingi za Umma. Licha ya Kamati kuishauri serikali kuandaa utaratibu maalum wa kuyalipa madeni hayo na hivyo kuweka sawa mahesabu ya Taasisi hizo. Pamoja na kutoziyumbisha Bajeti za Taasisi hizo hasa katika Idara Maalum ya SMZ.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena tunaiomba serikali kupitia Hazina, kuratibu madeni yote ya Taasisi za Umma na kuyaandalia utaratibu wa kuyalipa ili kuziondoshea mzigo mzito wa kibajeti taasisi zetu hizo.

9 Usimamizi Mbovu wa Sekta ya Ardhi.

Mhe. Spika, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2011/2012 imejikita katika ukaguzi katika sekta ya ardhi kama tulivyoona kabla. Kamati yangu inaipongeza serikali kwa hatua inazoanza kuzichukua kurekebisha kasoro nyingi katika sekta hiyo. Hata hivyo, bado Wizara ya Ardhi, kupitia Idara ya Ardhi na Usajili ina changamoto kubwa ya kurekebisha mambo mbali mbali yanayoiandama sekta ya ardhi ili hatimae ardhi iwe ndio tegemeo la mapato na uchumi wa nchi yetu.
Mhe. Spika, katika kufikia hatua hiyo, Kamati yangu inapendekeza mambo yafuatayo:
1. Kuwe na usimamizi makini kwa watendaji wa Idara ya ardhi.
2. Kuharakishwa kukamilishwa kwa Sera ya Ardhi.
3. Kuharakishwa kukamilishwa kwa mapitio ya Sheria ya Ardhi.
4. Kukamilishwa kwa usajili wa Ardhi.
5. Kukamilishwa kwa *Master Plan* ya Ardhi, Unguja na Pemba.

Chamgamoto Zinazoikabili Kamati Katika Utekelezaji wa Majukumu

Mhe. Spika, Kamati ilifanya jukumu zito la kuchunguza na kudhibiti hesabu za serikali. Katika utekelezaji wa jukumu hili zito, bado Kamati inaendelea kukabiliana na changamoto mbali mbali zinazokwamisha utekelezaji bora wa shughuli zake kwa maslahi ya wananchi.

- Kamati inakabiliwa na tatizo la utaalamu ama uwezo wa kukodi wataalamu katika fani mbali mbali za ukaguzi.

- Kamati inaendelea kukabiliwa na tatizo la muda wa kuzifanyia kazi ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hapa naomba ikumbukwe na nimkumbushe Mdhibiti kuwa tunapaswa tutenganishe baina ya uwasilishaji wa Ripoti za ukaguzi wa kawaida na ukaguzi maalum katika Baraza la Wawakilishi.

- Kamati inakabiliwa na tatizo la utekelezaji hasa wa mapendekezo ya Kamati, hali inayopelekea kasi ndogo ya uwajibikaji mzuri kwa watendaji wa sekta ya fedha katika Taasisi za Umma nchini.

Mhe. Spika, mbali na changamoto zinazoikabili Kamati yangu moja kwa moja, changamoto nyengine kubwa inayotukabili ni uwezo wa taasisi ambayo tunaitegemea kutufanyia ukaguzi na kutuzalishia ripoti kila mwaka ama kila baada ya kipindi fulani, yaani Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kama kweli serikali inahitaji kudhibiti mapato au kuongeza mapato yake, haina budi kuiwezesha Ofisi ya Mdhibiti kibajeti pamoja na kuboresha maslahi ya Wakaguzi. Bado Mdhibiti wetu hajatumika ipasavyo na kuna maeneo mengi ambayo yanapoteza fedha nyingi za wananchi na ambayo anapaswa kuyafanyia kazi kama hivi alivyoanza katika sekta ya ardhi. Sote hatuna budi tumuunge mkono kwa maslahi ya nchi na wananchi wetu.

Mhe. Spika, tunapaswa tutanabahi kwamba Zanzibar sio masikini na wala Zanzibar hatupaswi tuwe omba omba wa kila kitu. Zanzibar tuna uwezo mkubwa wa kuimarisha vyanzo vyetu vya kodi. Tuna uwezo mkubwa wa kutanua vyanzo vya kodi na tuna uwezo mkubwa (tukiamua) wa kukusanya kodi na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu, kuimarisha mapato ya watu wetu, kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii na hivyo, kuondokana na umasikini kwa watu wetu.

Uchunguzi wa Kamati yangu umebaini kwamba kuna ugoigoi mkubwa katika usimamizi katika Nyanja ya ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa sheria, ubunifu wa vyanzo vya mapato, matumizi ovyo ya fedha, wizi wa macho macho na wizi wa hadaa, uharibifu wa makusudi wa mali za umma na mengineyo mengi, hali iliyopelekea Zanzibar kutegemea misaada na mikopo hata katika shughuli za uendeshaji wa serikali.

Natoa changamoto kwamba iwapo tutakuwa makini na kila mmoja akayakinia, Zanzibar inaweza kuendesha mambo yake pasina kuomba omba!

HITIMISHO

Mhe. Spika, naomba sasa uniruhusu nimalize hotuba yangu kwa kukushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako na kuwa karibu sana na Kamati yangu na kuipa maelekezo na ushauri wa mara kwa mara Kamati yangu, miongozo iliyopelekea kukamilisha sehemu ya kazi na kutoa ripoti ambayo leo tunaiwasilisha mbele ya Baraza hili.

Naomba nimshukuru pia Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano ya karibu sana anayotupatia katika Kamati yetu, mashirikiano yaliyopelekea mambo mazito kugeuka na kuwa mepesi.

Mhe. Spika, niendelee kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, maofisa pamoja na wakaguzi wote kwa mashirikiano makubwa na ya karibu wanayoendelea kuipatia Kamati hii. Nikiri kwamba, mafanikio ya Kamati yamechangiwa kwa asilimia kubwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar.

Naomba niwashukuru pia Makatibu Wakuu wa Wizara, Maofisa wa hesabu wa taasisi mbali mbali wakiwemo Makamanda wa Vikosi, Maofisa Tawala wa Mikoa, Makatibu wa Halmashauri na Mabaraza ya Miji, Wakurugenzi wa Mawizara na Mashirika na wale wote walioitika wito wa Kamati yangu kwa njia moja ama nyengine. Nawashukuru sana.

Mhe. Spika, shukurani maalum na za kipekee ni kwa Wajumbe wa Kamati yangu na Makatibu Kamati kwa namna wanavyofanya kazi kwa umakini na mashirikiano makubwa. Kwa yakini tena bila ya kuchoka. Katika nukta hii naomba nimpe pongezi maalum Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mwakilishi makini, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mwakilishi wa jimbo la Amani, kwa mashirikiano makubwa katika kuiongoza Kamati hii.

Mwisho, naomba niwashukuru wenyeviti wenzangu wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Baraza kwa mashirikiano ya karibu kati ya Kamati zetu. Aidha, niwashukuru Wajumbe wa Baraza kwa kuwa makini katika kunisikiliza, naamini wataichambua vizuri na kuichangia Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nataka nikushukuru sana kwa kutumia kiti chako vizuri. *(Vicheko)(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka nikushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii nikawa mchangiaji wa mwanzo katika ripoti hii ya Kamati ya *PAC* ya Kuchunguza Hesabu za Serikali. Vile vile, nimpongeze mwenzetu Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, kwa kuja kuungana nasi, hasa upande tuliokuwepo wa *backbencher*. Naamini uzoefu wake utaweza kutusaidia sana kuikamata vizuri serikali ili iweze kuwatumikia wananchi.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo sasa, nataka niende moja kwa moja ili tukaendelee na majukumu mengine. Mhe. Spika, kwanza mimi nataka niipongeze Kamati. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri. Kila mwaka ripoti zao zinaonyesha kuboresha mambo mbali mbali. Ingawa kuna baadhi ya maeneo kuna mapungufu. Lakini haya mapungufu ni kawaida yetu kukumbushana na wenzetu kuweza kuyarekebisha ili mambo yetu yaende vizuri.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kidogo nitumie kama dakika mbili kabla sijaanza mchango wangu, kurejea tena. Jana hali yangu kidogo ilikuwa sio nzuri, ingawa nilikaa nyumbani na seruni, lakini nilikuwa nipo pamoja na Baraza. Nilimuona Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu kwenye televisheni na masuala yangu mengi aliyajibu vizuri. Ingawa moja hakulifahamu, lakini nitakuja kumueleza siku nyengine.

Mhe. Spika, kubwa zaidi nilitaka nieleze ufafanuzi alioutoa Mhe. Waziri wa Miundombinu. Mimi naomba sana Mhe. Waziri wa Miundombinu, awe makini sana na hoja tunazozijenga hapa, asiangalie amesema nani. Hoja tulizozijenga jana ni hoja za mapato ya serikali yaliyopotea ndani ya Wizara ya Miundombinu tena katika eneo la Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Sisi ripoti yetu ile ya Kamati Teule anayo Ofisini. Yeye kama ni mjumbe wa Baraza la Wawakilishi nataraji pia alipewa. Kwanza alikuwa aangalie ile ripoti ilisema kitu gani, halafu ndio aje atujibu yale majibu aliyotujibu.

Jana nilipokuwa nimeeleza kuhusu hanga. Mhe. Spika, hanga bado analimiliki Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Hanga bado hajapewa mtu mwengine. Kama wanadanganywa, wanadanganywa wao serikali, sisi hatudanganyiki. Sisi tumesoma na Mhe. Spika, unazidi kutusomesha na tunajitahidi kuichunguza serikali.

Mhe. Spika, mkataba ule ulikuwa unasema kwamba lile hanga amekodishwa. Pindipo atakaposhindwa kuendeleza kazi au atakapotaka kubadilisha matumizi kwanza lazima alirejeshe serikalini. Mhe. Waziri, kwanza alikuwa aniletee barua ya yule aliyekodishwa lile hanga, kwamba kuna barua gani alirejesha serikalini. Kama kalirejesha serikali na akampa mtu mwengine, ndio maana tukasema kwamba bado pale kuna mtu muwekezaji, lakini kuna mtu bado ni Meneja. Mhe. Spika, nataka kusema bado nitaendelea kuja

kuikamata bajeti ya Wizara ya Miundombinu na hili Mhe. Waziri, lazima tujuane moja.

Mhe. Spika, tuzungumza hanga jengine ambayo wanamiliki wale *Tropic Air* miaka karibu 15, Kamati imekwenda na kuona halilipiwi kodi. Tukauliza je ile kodi itakuja kufanyiwa kitu gani. Leo anakuja kunijibu Mwanasheria Mkuu, sijui kasema hivi. Mwanasheria Mkuu kasema yeye kwa sababu kuna mambo hawezi kuyasema, tunajua sisi. Kwa sababu kuna watu hawezi kuwagusa na ndio maana akanijibu kama vile. Kama Mwanasheria Mkuu kweli kama yale ndio majibu aliyonijibu vile, wewe leo unasema kwamba yeye keshajiondoa katika Kampuni, lile hanga limerudi serikalini.

Mhe. Spika, hanga lile kodi inayokodishwa ni mara 20 zaidi ya kodi inayopata serikali, halafu leo anakuja kulalamika sijui hatuna mashine za *X-ray*. Mhe. Spika, bado nataka Wizara ya Miundombinu waendelee kusimamia mapato ya serikali na Waziri hapa lazima aje atujibu jawabu hili. Mhe. Spika, baada ya hayo naendelea na mchango wangu.

Mhe. Spika, nataka nije moja kwa moja katika hichi kitabu chetu. Mimi nilimsikiliza Mwenyekiti, lakini vile vile, niliangalia na hichi kitabu. Mhe. Spika, nimefurahi sana kwamba sasa hivi Kamati ukiacha ile ripoti ya Mdhibiti Mkuu, lakini kuna mambo ambayo wanahisi ni muhimu kwa taifa wanayafanyia kazi, Mhe. Mwenyekiti, endelea na uzi huo huo.

Suala la mradi wa chumba cha Chini. Mradi huu upo katika hoteli ya Mantarif kule Pemba, umejengwa na umezinduliwa na Makamu wa Pili wa Rais. Nilivyoangalia ile ripoti Mhe. Mwenyekiti, mradi huu haukufuata taratibu za kisheria. Sio mradi huu tu, miradi mingi ya wawekezaji hasa katika maeneo ya mahoteli Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema. Zanzibar sisi si watu wa kupita na bakuli tukaomba omba, fedha zipo, uchumi tunao tumeukalia.

Mhe. Spika, ukiangalia miradi mingi ya uwekezaji ya mahoteli pamoja na huo wa chumba cha chini, kwanza haufuati taratibu. Muwekezaji anapopewa ardhi Mhe. Spika, kwanza anatakiwa ile ardhi aliyopewa anaipeleka *ZIPA. ZIPA* wanaangalia eneo lile na mipaka yake halafu *ZIPA* wao ndio wanatoa kibali cha ujenzi, kibali cha mradi.

Mhe. Spika, ukiangalia miradi mingi ile kodi ya ardhi wanayolipa, sio ile ambayo wameiripoti *ZIPA*, kule anapewa eneo dogo, huku anakuja kutumia eneo kubwa. Kwa hivyo, ina maana hapa kuna wizi, fedha za serikali nyingi hapa zinaibiwa na wenyewe tupo. Mhe. Spika, hapa kayazungumza katika ripoti na katika maelezo yake kwamba *ZIPA* kunalegalega. *ZIPA* hakulegilegi, watu wanajua wanachokifanya. Sisi humu ndani ndio hatujui tunachokifanya.

Mheshimiwa hebu tufanyeni kazi yetu, halafu tuangalie kama mapato hayatoongezeka serikalini.

Leo muwekezaji hawezi kuongeza eneo bila ya kushirikiana na *ZIPA*. Lakini *ZIPA* wapo wawekezaji wa mahoteli, wanachukua maeneo wanayaongeza, eneo lile halijarudi tena ardhi, likazidishwa tena likapimwa upya. Anapofanya *extension* muwekezaji ina maana pale lile eneo linakuwa linaongezeka na kodi ya ardhi itaongezeka. Sasa haya hayafanyiki. Lakini leo miradi mingi ukenda ya wawekezaji wa mahoteli, lile eneo walilopimiwa, basi ameongeza zaidi.

Mhe. Spika, humu katika hili buku kuna huyu muwekezaji mmoja ambaye kila siku naendelea kumsema na nitaendelea kumsema, muwekezaji wa hoteli ya *Kristal*. Nyinyi mnasema hadaiwi, huyu anadaiwa, kakufumbeni macho. Hiyo ardhi mliyokwenda kuikagua katika eneo lake, kazidisha na eneo jengine kinyume cha sheria. Muwekezaji hawezi kufanya *extension* bila ya kurudi tena ardhi akapimiwa upya eneo lake likatanuliwa.

Sasa hii mnayosema kwamba huyu hadaiwi, huyu anadaiwa. Mwenyekiti naomba rudi tena ili ukaangalie hilo eneo jengine analolimiliki. Sio hivyo tu, analikalia mpaka eneo la muwekezaji mzalendo. Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya *PAC*, rudini tena mwende mkafanye kazi. Sisi tuna macho mengi wajumbe wako Mhe. Spika.

Mhe. Spika, narejea tena katika mradi wa chumba cha chini. Mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi wa Kitaifa, inabidi sasa ijaribu kutoa angalizo, hasa katika hizi Ofisi zetu kubwa tatu, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mradi wowote ambao wanapelekewa barua ya kwenda kuuzindua kwanza waombe *documents* zote kisheria.

Mradi ule umejengwa kisheria, umefuata taratibu zote za kisheria. Inakuwa ni aibu kubwa mradi ambao haukufuata taratibu za kisheria, tunampeleka kiongozi mkubwa wa nchi anakwenda kuuzindua mradi ule. Ina maana pale watu wanakwenda kuficha makucha yao. Watu wameshajua, wameshajificha katika kichaka cha njugu, wanamwita kiongozi kwa sababu anajua akishakwenda pale yanapigwa mapicha, halafu zinawekwa pale mlangoni, hakuna Afisa yeyote wa kodi atakaekwenda kuuliza.

Mimi naomba sana hii miradi ambayo tunayoizundua, basi ni vizuri viongozi wetu hawa lazima kwanza wajulishwe kwamba taratibu zimefuatwa, halafu baadae ndio izinduliwe. Isiwe kwamba mtu amezindua mradi halafu ,vile vile, ukahalalalishwa. Hili mimi nataka niwaambie watendaji wetu wa serikali

kwamba pamoja na kwamba kiongozi mkubwa kenda kuuzindua, tusiridhike tu.

Tuigeni mfano wa wenzetu Bara. Bara wenzetu kule Arusha kuna mradi mmoja mkubwa upo njiani wa uwekezaji wa Hoteli. Alikwenda kuufungua Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, nadhani alikuwa Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, keshaingia madarakani. Wiki moja tu baada ya kuondoka tu, *grader* ikenda kuondoa pote pale mbele. Ndiyo, kwa sababu wamekiuka taratibu. Wenzetu kule Bara hakuna mjomba, wala hakuna maneno maneno kule. Ndani ya wiki moja Mhe. Rais, kakata utepe, kafungua hoteli, baada ya wiki moja Wizara ya Ardhi, imekwenda na *grader* imeondoa ile sehemu aliyokiuka sheria yote imeondolewa, ameachiwa ile hoteli yake.

Mhe. Spika, na sisi tufanye mpango kama huo. Namuomba sana Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati ukifanya tena ukaguzi wa ardhi, tena eneo hilo naomba ulikamate kweli kweli kwa sababu hapo ndio tunapoliwa. Ukifanya ukaguzi wa ardhi, angalia barabara mpya ya Matemwe. Mahoteli yale yote mwanzo kulikuwa kuna njia iliyokuwa inapita ndani. Ilikuwa ile ndio mwisho wa ujenzi wa mahoteli yao.

Lakini walikuja kutumia nafasi ile baada ya kujengwa hii barabara ya mbele, wakajiongezea wao wenyewe. Sijui kama watu wa ardhi wamepima maeneo yale, ile ni ardhi ya wananchi. Kama wanaitumia, sisi hatukatazi wawekezaji kutumia ardhi, tunachotaka kwamba iwe imepimwa kihalali. Muwekezaji akifanya ongezeko kama hilo, lazima arudi tena ardhi, apimiwe, aende tena *ZIPA*, halafu afanyiwe tathmini ya kodi ya ardhi. Mhe. Spika, nilikuwa naomba na hilo nalo tulifanyie kazi au Kamati yako iweze kulifanyia kazi.

Chengine ambacho nilichokuwa nataka niseme kwa haraka haraka kwa sababu kama nilivyokuomba Mhe. Spika, kamati yangu leo kidogo tumewaita wananchi ambao wana matatizo na muekezaji.

Nataka nirudi kidogo pale pale *ZIPA*. Mhe. Spika, *ZIPA* tunapoijua sisi ni *one stop centre* na sisi tulisema kama ile sheria yao ina matatizo kupelekwa pale maofisa ambao hawana kauli walikuwa Makatibu Wakuu ndio washiriki wenyewe kwa sababu wale wanakuwa ndio wenye maamuzi ya mwisho. Leo matokezeo yake katika ripoti hii Mhe. Spika, ukiliangalia ni aibu kubwa, mradi umepata kibali cha *ZIPA* ukiangalia *ZIPA* watu ardhi wapo, watu wa mazingira wapo, lakini ukiangalia katika ripoti watu wa mazingira wanasema sisi hatukutoa *certificate* yoyote.

Sasa huu mradi ulitoka vipi huku *ZIPA*? Mimi nadhani Mhe. Spika, hii *ZIPA* inahitaji kusukwa upya. Hivi karibuni tulisikia wajumbe wameongezwa wa

Bodi, lakini inaonesha bado kazi yao hasa wanayotakiwa kwenda kuifanya pale Mhe. Spika, inaonesha bado hawajaweza kuifanya vya kutosha.

Sasa mimi nilikuwa naomba kwa sababu hawa *ZIPA* ndio tuliowakabidhi dhamana zote katika suala zima la uekezaji. Sasa tukishindwa wao kuweza kuwasimamia vizuri au wakishindwa kusimamia kazi zao kwa kweli Mhe. Spika, tutaweza kuharibikiwa. Sasa Mhe. Spika, humu katika hii ripoti vile vile nilikuwa kuona kuna orodha ndefu hapa ya watu ambao waliokamata ardhi zimeshakaa muda mrefu hazifanyi kazi. Mhe. Spika, ukiliangalia hili kuanzia ukurasa wa 114 imekwenda zake mpaka inakaribia mwisho wa kitabu hiki imezungumziwa wale wamiliki wa maeneo ya ardhi ambao wamekiuka taratibu za kisheria.

Sasa Mhe. Spika, hapa pia Mhe. Mwenyekiti wa Kamati naona kidogo umefanya upendeleo, lakini vile vile umefanya ujaji, sasa huu ujaji Mhe. Mwenyekiti mimi sikubaliani nao yaani umefanya maamuzi huyu apewe miezi 6, sijui huyu apewe, hakuna. Mhe. Spika, mimi ninafikiri ungelirudi kwa mzee wetu ukafata *reference* ya ripoti ya Mhe. Ali Mzee Ali, ile ya Kamati ya Ardhi, ripoti haikusema huyu mpe miezi 6, huyu mfunge kifungo cha nje hakuna taratibu za kisheria zifatwe. Mhe. Mwenyekiti, ukishasema tu taratibu za kisheria zifatwe, Mheshimiwa taratibu ziko nyingi.

Sasa kama hazikufatwa taratibu hizi kwani hao mawaziri si kuna bajeti zao wanakuja tena, naomba sana waheshimiwa haya mabuku tusiyatupe na tusifungie njugu, haya mabuku tunatakiwa kila mtu aliyeagizwa tunamsubiri, yaani safari hii katika bajeti mimi nitashangia sana mtu akose la kusema, ya kusema haya humu, hizi ripoti za kamati haya ndio maagizo ya serikali.

Sasa kwa sababu haya tunayatupa, tunayafungia maandazi, hawa ndio maana wanasinzia ndio maana wote hawapo kila mmoja anafanya shughuli zake, hii ripoti ya Kamati ya *PAC* Mheshimiwa hii ndio serikali. Sasa Mhe. Spika, serikali mimi naomba sana na safari hii tunakwenda Dodoma, tukirudi huko salama maana ninasikia Mbowe anasema kutakuwa na ngumi, lakini hizo ngumi watapigana wao wenyewe sisi tunajua tunachokwenda kukifanya, tukirudi tutakuwa tushakolea, tunataka serikali haya mabuku wayachukue huko huko katika Bunge la Katiba, kila mmoja aangalie niliagizwa nini natakiwa niende nikafanye nini.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache ninapenda kukushukuru sana na huu mchango wangu leo ulikuwa wa kumkaribisha Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, ili ajue hili Baraza liko vipi. Lakini kwa bahati naona shamra shamra bado hazijesha huko ili sasa tunataka na yeye sio Kikwajuni sio Baraza la zamani kwenye asumini, huku mpaka ziletwe.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naunga mkono ripoti ya kamati, lakini vile vile, ule ushauri wangu wa kurejea tena kule ukachunguze tunavyotafunwa, basi naomba ufanye kazi hiyo katika bajeti hapa mambo yawe mazuri.

Mhe. Spika, ninakushukuru kunipa nafasi.

Utaratibu

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*: Mhe. Spika, tunajadili ripoti muhimu sana ripoti inayohusu matumizi ya serikali kwa ujumla. Tulitaraji leo serikali iwepo hapa. Serikali ina mawaziri 16 waliopo sasa hivi mawaziri ni watatu, hawafiki alau nusu. Sasa nina hofu kwamba hizi kelele tunazopiga zikapotea bure. Mhe. Spika, nadhani Baraza lako ungeliliahirisha ili tukapate muda mawaziri waweze kufika hapa *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ningependa nimtoe hofu Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* na Wajumbe wote wa Baraza hili kuwemo humu ndani kwa mawaziri waliopo hakumaanishi kwamba haipokewi taarifa ya kile kinachosemwa na wajumbe, mawaziri wapo hapa kwa niaba ya mawaziri wengine kila kinachosemwa inapokelewa na taarifa zitakwenda kwa utaratibu wake kwa mujibu wa serikali na majibu yatatoka kwa mujibu wa yote yatakayokuwa yamezungumzwa katika Baraza hili. Kwa hivyo, naomba Baraza letu liendelee na wasiwe na wasiwasi na idadi iliyomo humu ndani. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Pamoja na ukweli huo kwamba Waheshimiwa mawaziri waliopo wanafanya kazi kwa niaba ya wengine chukua nafasi ya kuwaita wenzio ambao hawana dharura, kwa sababu mimi ninajua dharura za waheshimiwa wacheche sana kati ya Mawaziri. Mhe. HarounAli Suleiman, ni mmojawapo tunajua anaumwa, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameniaga, lakini waheshimiwa wengine sina taarifa nao. Ila Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na Mhe. Waziri wa Fedha ninajua wapo safarini kikazi. Sasa wengine watafute waje hapa.

Wakati Mheshimiwa anaendelea kuwatafuta wenzake waje tuendelee na shughuli.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na sisi *backbencher* tungesema leo tupunguke tutoke nje waliobakia watawasilisha hoja sijui Mhe. Spika, kama ingekuwa sahihi hivyo kutokana na unyeti wa ripoti hii ya *PAC*.

Mhe. Spika, imekuwa siku zote tunaimba wimbo na si kawaida yetu kuwa sisi tuje hapa tuoneshe suti na nini tuimbe nyimbo inakuwa halihalisi Mheshimiwa. Naomba sana Mheshimiwa marekebisho ya sheria lazima yawepo.

Mhe. Spika, kama tutarekebisha sheria nimesema siku moja Mheshimiwa kuwa sheria ya *PAC* tungewapa kama wenzetu Uganda huko kama watu wakimbaini pale pale wanamtia pingu. Mhe. Spika, ingekuwa amani kubwa sana na wale mapanya wanaokula zile mali zetu, basi wasingefika hadi hiyo. Mheshimiwa inasikitisha sana leo ripoti hii nimekaa tangu jana usiku mimi sijawahi kusoma hata siku moja ripoti siku mbili. Nimekaa nyumbani ninasoma mpaka macho yananiuma, Mheshimiwa kutoka machozi ndani peke yangu kutokana na ripoti hii, uchungu wa fedha za wavuja jasho Mhe. Spika, zinavyopotea za wanyonge nikupeni hongera sana *PAC* hongera sana.

Sitoona haya kumsifu na yule mama *CAG* lazima nimpe haki yake. Mhe. Spika, mama jasiri na *inshaalla* Mungu atamlinda hii kazi ina fitna, lakini Mwenyezi Mungu atamlinda asiogope kabisa hakuwekwa na binaadamu kawekwa na Mwenyezi Mungu. Na anaowatetea ni wanyonge maskini kutokana na haki zao Mhe. Spika, *wallahi* inasikitisha sana mimi leo nilisema nisichangie, lakini itabidi nichangie kutokana na uchungu Mheshimiwa.

Mhe. Spika, sheria hazifatwi, kama mimi ni mtaalam wa ushauri muelekezi wa bure, sheria hazifuatwi ni msingi wa matatizo haya ya sheria, hatuzifati. Sisi Wawakilishi kazi yetu kutunga sheria, lakini nimegundua kuwa tukishatunga hapa sheria, tukipitisha ndio maana kama unanipeleleza mara nyingi sana ninakuwa siungi mkono Mhe. Spika, kwa sababu naona bure tu zinatiwa kwenye *briefcase* Mheshimiwa. Hali imekuwa ngumu sana.

Mhe. Spika, hali halisi ukiona ya kodi zetu hizi ambazo zilizokuwa zinatakiwa ipasavyo hasa zilipo kwa mujibu wa sheria ya ardhi, watu hawalipwi kwa makusudi. Sasa niseme sijui kunakuwa na miaya au kutokana na nini. Mhe. Spika, naomba sana sasa, serikali kwa vyovyote ikitaka isitake ipate tabu ile hasara kwa *PAC* wawe ndio washauri wetu waelekezi kutokana na mambo kama haya. Vyengine vyovyote maana yake tuseme ukweli Mheshimiwa kipindi kidogo tu walichoingia hawa michakato ya kufatilia masuala haya wameokoa pesa ngapi, sasa hivi watu wanalipwa kwa *speed* kubwa sasa, hivi Mheshimiwa hii ukweli tuseme, kwa nini tuwanyime haki zao Mheshimiwa *PAC*.

Mheshimiwa twende katika nchi za wenzetu huko, *PAC* wanafanya kazi 24 *hours*, lakini sisi tumeweka *special* kipindi hadi kipindi, hapana, sheria tuigeuze, sheria tuitunge kuwapa hawa muda mrefu wa kufanya kazi, hawa

ndio waokozi wetu wa mapato Mhe. Spika, tukitaka tusitake lazima tuwape nguvu. Lakini si hivyo, tutafanya mchezo tutakuja hapa tutaimba nyimbo basi, kavaa suti nzuri tumeondoka. Ninaomba sana Mheshimiwa hili suala lifatiliwe.

Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati Teule ameshamaliza kazi, ameonesha ustadi wake na ameonesha jinsi gani mapato yanavyoteketea. Ameeleza sheria watu wanavyonyang'anywa viwanja kwa mujibu wa kutokutekelezwa sheria, ameeleza hapa. Mhe. Spika, tutasema mpaka tutadata hapa, lakini watekelezaji wanakuwa ni wazito sana. Nishukuru sana leo sijui Makatibu wapo wangapi huko juu, lakini kama nimemuona Katibu wangu wa Ardhi, ninafikiri na Mawasiliano na wengine sijui wako wapo kama wapo na wao vile vile iliwapasa leo wakati mgumu huu wa ripoti hii wawepo.

Mheshimiwa, nimshukuru sana Mhe. Waziri, futa futa sasa anaifanya *PAC*, mama yangu *CAG* nae wamempa njia nzuri Mhe. Waziri, lakini *PAC* niwaambie hata na mimi sikubaliani la kusema aaa kuiregeza kamba hapana, tuondoe hicho kitu bwana, hakuna miezi sita wala miezi hulipi ondoa. Hiyo ndio hatua tutakayoifanya sasa hiv, Mheshimiwa hulipi ondoa.

Mheshimiwa, Kuna hoteli viwanja vyao wamefutiwa kwa mujibu wa sio sheria nilisema sana kipindi kilichopita, hii Hoteli ya Nugwi kiwanja chake alifutiwa kinyume na utaratibu, naomba sana Mheshimiwa na *PAC* wameiona kitu hicho, arejeshewe kiwanja chake, hawa jamaa wa *spice*, naomba sana Mheshimiwa, hapo mwanzo hakufutwa kwa mujibu wa sheria hakuwa na *notice*, hakuwa na indhari, Mheshimiwa, hili suala limefutwa, baadhi ya kampuni zifutwa, lakini imebakia kampuni hii moja, madhali wao wote wameweza kufutiwa, basi hiyo iliyobaki ifutwe. Tunaomba hili suala isiwe kama ndio nyimbo ifanye utekelezaji.

Mhe. Spika, nataka niwageukie Makatibu na Wakurugenzi mimi naomba sana wao ndio watendaji wakuu, maamrisho haya, maoni haya ya Wawakilishi mimi naomba sana Mheshimiwa wawe *faster* katika kuyatekeleza, makatibu wapo wengine wazuri tu wanatekeleza au Makatibu wengine ukiwapigia simu wanakuwa hawapokei simu zetu, sijui wanaonaje, kumbe unataka kumwambia kitu *before*, ee bwana, kuna kitu fulani, lakini nayo tabia wanakuwa nayo wengine simu zetu hawazipokei, sijui wanatuona maadui, hapa na sisi si maadui, sisi tunawaongoza wao kwa kuwasaidia wananchi, sisi hatuna uadui na mtu. Uadui utajijengea wewe mwenyewe tu.

Kwa hivyo, naomba sana Mheshimiwa kuwa hili suala la huyu muekezaji haraka sana asaidiwe. Na si vibaha akaweza kushuka mahotelini au kwenye ardhi yenyewe.

Mhe. Spika, nimeona hapa ni kweli *ZIPA* ndio wasimamiaji wetu wakuu Mheshimiwa, naomba sana jambo ambalo limenisikitisha sana tuna wazalendo wetu wa nchi yetu wanataka kuweka miradi yao na wengine sheria mimi hapa kitu kinanishangaza, kumbe kuna wazalendo wengine hawajafuata sheria, lakini kuna wazalendo wengine wamefuata sheria kila kitu wamefanya mpaka leo wanataka, naomba sana sioni vibaya mradi ule wa chelezo wa mzalendo yule Mhe. Spika, apewe *certificate* yake. Kafanya utafiti wa mambo ya *environment* ameshapewa *certificate* kilichobakia naomba sana Mheshimiwa kama huyo uliyomkusudia kutaka kumpa wao, jirani yake basi naomba Mhe. Spika, hili suala lisiwepo atizamwe kwa jicho la huruma na aweze kupatiwa.

Mimi nawaomba sana watu wa *ZIPA* sana kabisa kuna barua nyengine wasiziangalie kwa sababu *ZIPA* afate sheria kwa mujibu wa sheria aliyokuwa nayo yeye. *ZIPA* asiendeshwe na hii Mhe. Spika, ndio tatizo letu, tunaweka au tunaunda mamlaka, lakini baadae mamlaka tunazihodhi, tunaziingilia kati na tunazinyima uhuru Mheshimiwa.

Sasa na hii *ZIPA* wasipokee barua hata kama mkubwa gan, wafuate utaratibu wa sheria wanavyojua wao. Sasa hili ndio tatizo. Mheshimiwa, tatizo moja hilo kubwa tunalo wanaingiliwa katika utendaji wao kwa kulazimisha, kwa kumuogopa mtu au kwa kupeleka barua iliyokuwa kali sana ambayo ina neno Siri. Mheshimiwa, hatufiki. Ukweli tuseme tunawanyima uhuru watendaji wetu, Waheshimiwa tunawatisha barua sitaki huyo, muweke huyu, tutafika wapi Mheshimiwa? naomba Mheshimiwa hilo suala lifikiriwe sana.

Mhe. Spika, kuna sehemu nyingi sana humu nimeona zimefutwa, kuna wengine kama ukurasa huu hapa kuna muekezaji Said Bakhresa, kamati imetoa ushauri kwa Waziri kuwa avumiliwe muekezaji, tunakosa mapato mangapi, hakuna kuvumiliwa sasa hivi hapa. Mhe. Spika, naomba sana Mwenyekiti wangu wa Kamati hili neno la mtu kungojewa na kuvumiliwa umekwisha wakati huo sasa hivi ni wakati ambao tayari Mheshimiwa kashindwa awache, wapo watu wamekaa na *briefcase* zao wanangojea kazi. Sasa wewe ukinambia avumiliwe, mimi nitakuwa ninashangaa sana.

Mhe. Spika, nikenda katika masuala hayo hayo katika suala la viwango, hata na mimi linanipa utata kidogo, naomba sana Mhe. Waziri, anisaidie suala hili kuhusu habari ya viwango vya kodi. Kuna wengine utakuta sijui tunakwenda kwa hekta au basi mtu anaamua tu katika kushuhudia kutaka kumkomoa mtu kumuwekea kodi kubwa, lakini majibu anasema viwango vinafanyiwa kwa mujibu wa utaratibu unavyoonekana haja ya matumizi yenyewe, sasa mimi naomba Mheshimiwa hebu tuekeni sawa tuweke *fix* zenyewe za uhakika, hasa kuwa tunakwenda kwa hekta zenyewe au tunakwenda kutokana na mujibu

kuwa aa ule mradi uhalisia ulivyo ndio tunaamua hivyo, ningemuomba hili suala kidogo niweke sawa hapa ili kuweza kujua na nini.

Lakini vile vile, Mheshimiwa nimesikia mambo ya jeti, ninakumbuka kipindi fulani dokta mwenyewe aliye-*act* leo alisema hizi jeti zitatolewa kodi, zitakuwepo kodi sasa sijui kama hizo kodi zimeshaanza hizi jeti kulipiwa kodi kwa sababu tulisema kuwa, kuwaondoa moja kwa moja jeti, si jambo zuri kwa sababu wenzetu kule hata huko nje wanafata vile vitu kama hivyo jeti ndio *market* yenyewe inapokuwa.

Hoteli nyengine kama hukuweka jeti na *market* yenyewe huna. Lakini katika njia ya kuweka utaratibu au pengine kumpiku mtu mbele pengine ashindwe tulisema kuwa kutakuwepo na *special* kodi ya zile jeti yenyewe. Sasa sijui *PAC* kama na hilo ulililiona na kama hawajaliona, basi ninawashitua kuwa rudini tena na mimi nakwambieni rudini tena kaangalieni, tulitoa kauli hapa Waziri mwenyewe husika alisema kuwa kutatolewa kodi za jeti. Hilo mimi ninafikiria kama halijaonekana kama limeonekana, lakini sawa.

Vile vile, Mhe. Spika, tulisema tutakuwa na utaratibu wa kuwa hizo jeti wenyewe kabla ya kuzijenga mamlaka husika utaratibu utafuatwa halafu na kuonesha kuwa huyu amepata vibali vinavyohusika kwa kupitia watu wa uvuvi, kwa kupitia watu wa mazingira, nalo hilo Mheshimiwa naomba sana kuwa tusiingie katika dimbwi ambalo lililokuwa halina msingi.

Lakini Mheshimiwa nimekwenda katika hizi Halmashauri zetu, kwanza nitoe pongezi kwa Halmashauri ya Kaskazini B nimeona hapa na kidogo na nyinyi mliwasifu na mara hii wamefika malengo mazuri sana mpaka sasa wanakusanya milioni arubaini. Ama kwa kweli ninawasifu na ninawapongeza sana kwa *acting* aliyekuwepo sasa hivi Afisa wa Mipango nimshukuru sana na Mwenyezi Mungu amjaalie Mheshimiwa na si vibaya mkampa huyu kwa sababu ana fani nzuri ya uchumi na ndio maana kipindi kidogo anakusanya mapato mengi sana. Mhe. Spika, hilo nilione na hizo Halmashauri ndio zinazotusaidia katika majimbo yetu.Na zile sheria za serikali za mitaa nazo zingekuwa tunaharakisha sana zingweza kutusaidia nazo katika kuona maeneo ya uchumi wetu jinsi gani ambavyo tunaweza tukapata na sheria zile ambazo zinaweza zikalinda.

Mhe. Spika, kama nilivyokueleza, utaratibu wa sheria ni muhimu sana, namalizia Mheshimiwa nakuona unanitizama, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Teule, amekwisha tuonesha njia sasa tusikae hapa kila siku ikawa tunapiga kelele. Mimi ninafikiria utaratibu ule tungeupata kwa sababu ile ripoti ilikwisha kutoa hukumu za aina yote kwa sababu ametueleza jinsi gani uhasilia wa ardhi thamani zake, jinsi gani mtu anavyotaka kufutiwa ile ardhi,

utaratibu upitie na nini. Mimi naomba sana kuwa wenyewe wapo huko juu wanatusikia na utaratibu wataweza kufuata.

Mhe. Spika, nikushukuru sana na nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* pamoja na mama yangu *CAG* aliyejitolea kabisa kuweza kufichua mambo haya mengi sana na nimshukuru kwa mara ya mwisho mzee wangu Ali Mzee Ali Mwenyekiti wa Kamati Teule, ametuongoza ametupa kigezo kikubwa na mpaka leo *hansard* zake ninazo kwenye begi langu nitatembea nayo kutokana na masomo haya, tunaonana katika bajeti. Naunga mkono asilimia mia. Ahsante sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, ninakushukuru kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia. Mhe. Spika, mimi nianze kwa kumshukuru Mhe. Mwenyekiti kwa uwasilishaji wake mzuri kabisa na kwa ufafanuzi wake ambao ameutoa juu ya ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Baraza.

Mhe. Spika, mimi nianze kwa masikitiko kabisa na masikitiko yangu dhidi ya serikali, kwa sababu Mhe. Spika, ukiangalia ripoti ya Kamati ya *PAC* huwa imekusanya taasisi zote za serikali kuanzia Wizara na Masharika yake. Ukiangalia huu uwasilishaji ambao ameutoa Mhe. Waziri, hapa wa majibu au hoja zile ambazo zilitolewa na Kamati kipindi kilichopita kikurasa hichi hapa hakiendani na yale maelekezo yaliyotolewa na chombo hiki ninasikitika sana Mhe. Spika. Ukiangalia ripoti yetu ya mwaka jana kitabu ninacho kina kurasa katibu 188 na maagizo zaidi ya mia na, kwa sababu maagizo ya *PAC* tofauti na ya kamati zile za kisekta. Kamati za kisekta utakuta mna Wizara mbili ama tatu.

Maagizo unaweza kukuta yapo 28,40 *PAC* ni serikali nzima sasa leo waziri anakuja na majibu haya hayakujitosheleza hata kidogo Mhe. Spika, ukiangalia majibu ambayo ameyatoa waziri na maelekezo au maoni ambayo yalitolewa na Kamati yakaridhiwa na chombo chako hiki hayaendani kabisa Mhe. Spika. Hii inaonekana ni dharau ya serikali juu ya chombo hiki na hili jambo kwa kweli huwa tunalipigia kelele sana Mhe. Spika, lakini linaonekana bado linaendelea na matokeo yake ndio haya ambayo yanaonekana sasa hivi hapa.

Kamati inawasilisha ripoti serikali, hapa wapo mawaziri watatu ingawa umemuagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili awaite wenzake, lakini wapo wapi tunapiga kelele, huyo ambaye anapaswa awepo pia hayupo kakaimisha, lakini ukiitizama hii ripoti ambayo kampa huyo kaimu haina saini, humu haina chochote sasa sijui kama kweli Waziri wa Fedha ndio kampa yeye Dr. Mwinyihaji, sijui tutakuwa tuna uhakika gani.

Maana yake hii inawezekana kaandika mwengine yeyote tu akaiwasilisha hapa. Lakini hata ukiangalia Mhe. Spika, tarehe ile iliyowasilishwa inawasilishwa tarehe 28 Januari, ndio imeletwa huku Barazani ,sijui kama ndio kweli au vipi, maana yake sisi tupo tarehe 4 Februari, sasa nilitegemea labda ameiwasilisha leo kwamba itafatana hata na tarehe hizo.Lakini napata shaka mimi Mhe. Spika, juu ya utaratibu unaotumika na serikali katika kuleta majibu ya hoja zinazotolewa hapo.

Inaonekana kama ni kitu cha kutupia tupia tu kwa kweli Mhe. Haipendezi hata kidogo, serikali iliyokuwa makini inawajibika mbele ya chombo hiki. Sasa kama leo serikali ndio inatwambia hivi, ndio umakini wake huu hapa, mimi kwa kweli Mhe. Spika, ninasikitika kabisa na uwajibikaji wa serikali katika chombo hiki.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele baada ya kutoa hayo masikitiko yangu, sasa mimi niingie katika ripoti hii ya mwaka 2013/14 maana hii ya 2012/2013 majibu Mhe. Spika, sijayaona sijaridhika nayo hata kidogo, maagizo ukiyaona haya ni mengi mno, lakini serikali imeshindwa kuleta hapa majibu.

Sasa nakuja kwenye hii sasa sijui nao watafanyaje. Lakini ukiangalia Mhe. Spika, hii inaonekana ndio mfumo wa hii serikali yenyewe wa majibu katika chombo hiki, hata ukiangalie zile Kamati Teule tuliokuwa tunaunda, tuliunda ile ya mwanzo ile ikawasilisha ripoti hapa ikakataliwa, lakini majibu yake mpaka leo hatukuyaona tena hapa, tutaleta mwaka wa tatu huu, hakuna majibu. Tukaunda nyengine ile ndio hivyo hivyo, imekuja ile ya *ZECO* ndio hivyo hivyo.Kwa hivyo, Mhe. Spika, inaonekana hiyo ndio aina ya serikali tuliyonayo.

Mhe. Spika, niingie katika ripoti ya kamati ya 2013/2014 ukurasa wa 82 kwenye ukaguzi yakinifu. Mimi nitaingia kwenye masuala ya ardhi moja kwa moja, haya mengine ya kawaida haya kutokufuata taratibu za manunuzi sijui kufanya nini tushayazoea tunawambia hapa, lakini utaratibu ndio ule ule. Kwa hivyo, labda kwenye hii ardhi labda watabadilika maana huko wameshakuwa hawabadiliki, tunawaelekeza tunawashauri, lakini hakuna kitu kinachofanyika.

Sasa kwenye ukaguzi yakinifu sehemu ya ardhi, mimi nianze na kitengo cha ukodishaji ardhi kwenye ukurasa wa 89. Mhe. Spika, ukiangalia hapa kwenye ukurasa wa 89 Idara ya Ardhi kitengo cha ukodishaji ardhi kwa mwaka wa fedha huu 2011/2012 anasema kwenye hoja naomba 13(1) malipo ya kodi ya ardhi yaliyolipwa pungufu, dola 98,209.5 ikiwa sawa na *Tshs.* 152,224,725. Mhe. Spika, hapa Mdhibiti amechukua *sample* tu hakukagua maeneo yote.

Mara nyingi anapofanya kazi zake anafanya *sampling*, sasa uone namna gani ya serikali inavyoacha hizi kodi.

Maana hapa anasema malipo ya ardhi yaliyolipwa pungufu, pungufu maana yake kinajulikana kiwango cha kulipwa lakini kwa makusudi tu, kinaachwa hakilipwi, ukiuliza sababu inaonekana hakuna. Sasa sijui Mhe. Waziri atatwambia nini katika hili? Kwa sababu utaratibu umewekwa, sheria zipo na kwa nini hazifuatwi?

Sisi tunabishana huku, tunahangaika katika kuhakikisha serikali inakusanya kodi, tunawatungia sheria nzuri kabisa ili ile kodi iweze kukusanywa, matokeo yake sheria zile wanatia mkobani, mtu anatoa sheria zake mfukoni anakwenda kutukusanyia anavyotaka yeye. Sasa tukijiuliza hizo zinazosalia zinakwenda wapi.

Nikiendelea mbele Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa wa 93 kwenye malipo ya kodi pungufu baada ya kufanya utanuzi. Alilizungumza hili Mhe. Hamza Hassan Juma hapa, lakini kwa kweli Mhe. Spika, hili ni tatizo. Mkaguzi alipokagua haya maeneo ambayo ameyaonesha tu yanaonekana yako mengi mno, kwamba baadhi ya wawekezaji wetu wanafanyiwa utanuzi sio wanafanya, wanafanyiwa na Idara ya Ardhi, lakini kile wanachoongezewa baada ya kufanyiwa ule utanuzi hakifanyiwi mahesabu na hivyo tunashindwa kukusanya kodi zetu. Wakati tunamkamata mwananchi wa kawaida kuhakikisha kwamba analipa kodi, huyu mwekezaji ambaye katoka huko kwa ajili ya kuja kuwekeza akijua na sheria zipo na anazisoma vizuri kabla ya kufanya kazi zake, lakini serikali inashindwa kabisa kukusanya kodi zetu.

Hivi ni vitendo ambavyo Mhe. Spika, vinafanywa kwa makusudi. Kwa sababu kama watakuwa wamekwenda watendaji, wamelipima lile eneo ambalo wameongeza, kipi kilichokuwa kizito sasa kukusanya kodi katika eneo ambalo limeongezwa? Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi namuomba sana Mhe. Waziri atapokuja kutoa majumuisho yake aje atusaidie kikwazo chake ni kitu gani kutukusanyia hizi kodi zetu. Nataka nione zile sababu za msingi zinazofanya akashindwa kuzikusanya hizi. Maana sisi kama kamati tulipokwenda huko hatukupata majibu, sijui Mhe. Waziri yeye atatusaidiaje katika hili.

Mhe. Spika, nasogea katika ukurasa wa 104 wa kitabu hiki hoja nambari 13(6) Idara ya Ardhi na Usajili kutozifanyia mapitio ya bei za kodi za ardhi. Hapa hata Mwenyekiti wa Kamati alipokuwa akiwasilisha ripoti yake pale alilizungumza hili, kwamba kuna upotevu wa pesa nyingi sana katika eneo hili. Kwa mujibu wa sheria waziri anapaswa kufanya *land rent review* kila baada ya miaka mitatu, lakini kwa masikitiko kabisa Mhe. Spika,

waheshimiwa mawaziri wetu wa ardhi kwa miaka kumi hawajafanya hiyo kazi. Kwa maana hiyo, kama mtu alikodishwa kule kwa dola 100 ndani ya miaka kumi, kaendelea pale pale na hiyo juzi ambayo inasemekana imefanyika haikufuata huo utaratibu, mtu amefikiria tu katika kichwa chake, sasa tuondoke katika mia tufanye 110, wakati utaratibu unaelekeza namna ya kufuata.

Lakini Mhe. Spika, Mwenyekiti wa Kamati katika uwasilishaji wake alisema hapa kwamba kuna mapungufu mengi katika eneo hili. Kulikuwa kunatakiwa kuwe na kanuni pale, hazipo, ambazo ndizo zitakuwa zinamuelekeza huyo Mhe. Waziri namna ya kufanya hivyo. Kwa hivyo, anaamua tu Mhe. Waziri katika kichwa chake leo nafanya hivi baada ya miaka mitatu ijayo kama yupo yeye anaendelea, maana kila siku wizara hii inabadilishwa mawaziri, anaamua tena na yeye afanye anavyoona.

Kwa hivyo, serikali hapa inashindwa kukusanya, kwa sababu kila mnapofanya yale maana yake viwango vinaongezeka ndio inategemea na hali ya soko lilivyo. Ardhi ile kwa miaka kumi iliyopita sio bei iliyopo sasa hivi ya ukodishaji. Hata hiyo nyumba ukiwa umekodi miezi sita inawezekana ikawa kila baada ya miezi sita akienda mwenyewe anaongeza tena kidogo kidogo, sasa ardhi zetu imekuwa kama shamba la bibi ukishapewa wewe umepewa tu, wewe na hiari yako, hivi ndivyo inavyoonekana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nisogee katika ukurasa wa 98 kwenye ujenzi wa *Jet*. Hili suala Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, alilizungumza kidogo hapa, lakini na mimi nataka nilikazie tena.

Mhe. Spika, imeonekana kuna mapungufu saba katika ujenzi ule wa zile *Jet*. Kwanza huwa hawafuati taratibu wale wajenzi, maana yake inaelekezwa kabisa wanapotaka ujenzi wa aina ile kwanza kuna mambo yakafanyike kule kwa watu wa mazingira, hakuna kinachofanyika, lakini mimi nazungumzia hili suala la ardhi. Kwa sababu katika ile sheria ya ardhi mpaka ile bahari unayoiona Mhe. Spika,pia inaitwa ardhi, maana yale maji yamekaa juu ya ardhi nayo pia inapaswa ikodishwe, lakini cha kushangaza au cha kusikitisha sana kabisa hakuna hata mwekezaji mmoja ambaye amejenga zile *jet* ambaye anakodishwa ardhi. Ukiuliza hakuna majibu.

Sasa huku sisi tunahangaika tunatafuta fedha ndio pale aliposema Mhe. Hamza Hassan Juma, uchumi tunao lakini tunaukalia. Maana yake fedha zile zipo lakini hatuzikusanyi, na ukiangalia haya maeneo yako mengi kabisa. Lakini vile vile, maeneo haya nafikiri ukodishwaji wake ungekuwa tofauti na ile ardhi ambayo iko huku juu maana yake hata na wawekezaji, soda inayouzwa kule kwenye Jeti bei yake tofauti na soda unayokunywa katika

hoteli hii hii moja huku kwenye baa za juu, kama huku shilingi 3,000 kule soda yake itakuwa moja shilingi 5,000. Sasa na sisi ardhi zile tungeweza kukodisha kwa bei nzuri zaidi ili serikali ikaweza kupata fedha, lakini matokeo yake zimeachwa tu, wawekezaji wale wanafaidika hakuna kinachopatikana.

Lakini mimi sikubaliani na hilo Mhe. Spika, kwamba hakuna kinachopatikana. Mimi nina hakika wanajua lakini watu wanafanya kwa makusudi, nini kinaendelea hapo nakuachia mtihani huo Mhe. Spika.

Nikiendelea nije katika ukurasa wa 105 kwenye….

Mhe. Spika: Bado dakika tano.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Sawa Mheshimiwa, ingawa kidogo naumia maana hii ripoti ya serikali nzima Mhe. Spika, sasa ukitupigapiga hivi kidogo kama zile za wizara mbili tatu tunaumia, lakini nakubali Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kuna suala la eneo lililohaulishwa kutoka *Mawimbini Hotel Village Ltd* na kupewa mwekezaji mwengine bila ya kufuata sheria. Kuna mwekezaji amepewa eneo pale iliyokuwa Hoteli ya Mawimbini. Eneo lile kwa mujibu wa sheria limerudi serikalini lote, kwa sababu wale wenyewe walilitelekeza, lakini kuna mtu tu kwa ubabe wake kaamua kwenda kumkatia kipande mzungu akampa, kwa ubabe tu, maana hakufuata sheria.

Sasa watu wa ardhi wapo amefika mpaka kumeanzwa kujengwa kumefanywa nini, mimi nashangaa sana inakuwaje, kwetu huku ukichimba ile karo tu wamefika, aa umeingia eneo si lako, kule inakuwaje mtu anafika pahala mpaka anajenga? Lakini ukiuliza unaambiwa kapewa kibali na *ZIPA*, ardhi sio ya *ZIPA*.

Tulipolifuatilia suala hili Mhe. Spika, ukiitizama vizuri hii *story* humu *ZIPA* hakumpa ardhi, yeye alimpa uwezo wa kujenga tu, ruhusa ya ujenzi wa *extension* ya hoteli yake, lakini matokezeo yake yeye kaenda kujenga *villa* katulia *bukheri khamsa wa ishirini*, lakini kuna mbabe tu ndio kaamua. Mimi nafikiri serikali iangalie mapendekezo ambayo yamependekezwa na kamati iweze kuyafanyia kazi vizuri na kwa muda ambao umewekwa na kamati.

Mhe. Spika, nisogee mbele katika ukurasa wa 129 Pemba kule, kuna Kampuni ya *Mpapindi Holiday and Diving*. Mhe. Spika, huyu anaitwa mwekezaji mwenye kampuni hii, kuna mzungu na mke wake kule wamepewa eneo na serikali tangu mwaka 2004 sehemu za Makangale kule. Lakini kutoka mwaka huo wamekodishwa ardhi na serikali mpaka hii kamati ilipokwenda

hajawahi kulipa kodi ya ardhi hata siku moja. Lakini Mzungu yule hana kodi ya aina yoyote anayolipa katika serikali hii, anaishi hapa halipi kodi ya ardhi, hajajisajili *ZRB*, hayuko Kamisheni ya Utalii, lakini anaitwa mwekezaji na *Immigration* wamempa *class 'A'* ile *permit* yake, yaani yule wa juu kabisa.

Lakini nikaridhika kidogo na watu wa Idara ya Kazi, walimpa kibali cha kufanyia kazi alipoomba lakini ilipofika mwaka 2007 wakasema sisi hatumpi tena kwa sababu hatumuoni kazi anayoifanya, lakini ukienda *ZIPA* mpaka leo anatetewa huyo kwa kuonekana mwekezaji mkubwa kweli. Mimi niulize uwekezaji wa aina gani anaoufanya pale, hauzi hata kahawa ile ya kikombe shilingi 150 anaitwa mwekezaji, shughuli anayoifanya haionekani.

Mhe. Spika, aliomba ujenzi wa kujenga mahema maana kapewa katika eneo la Msitu wa Ngezi lililokuweko *beach* kule, akaomba ajenge mahema 70 ili aendeshe hoteli ya kitalii. Serikali ikasema hapana, 70 mengi tunakupa ujenge 50, huu mwaka wa kumi na zaidi ana mahema yake mawili ambayo anaishi yeye na huyo mke wake, hakuna mtalii aliyekwenda pale, hakuna mgeni aliyekwenda.Kwa hivyo, hana shughuli yoyote anayofanya, lakini anaitwa mwekezaji. Cha kushangaza kwa vile keshakaa sehemu zaidi ya miaka 10 anaomba na uraia. Sasa nataka nimtahadharishe rafiki yangu Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais keshaleta maombi huku, sasa sisi huku tunamuona sijui kama Mhe. Waziri atampa huo uraia au vipi, maana sasa anataka awe raia kabisa lakini shughuli anayoifanya haipo.

Tulipomwita kwenye mahojiano kwa jeuri kabisa anasema aah, mimi naishi hapa kwa kuomba omba tu, wakubwa wanakuja wakinigaia na watu wengine ndio ninaishi. Sasa hayo ndio maisha ya mwekezaji kweli Mhe. Spika, na vyombo vipo, taasisi zetu zipo hizi zinamuangalia tu kwamba huyo ni mwekezaji, huo uwekezaji wa aina gani? Tukawaita watu wa *ZIPA* kuwauliza oh! Maana yake huyo bwana ameharibikiwa na sisi ndio taasisi kazi yetu kumsaidia tunamuengaenga, tunamsaidia mpaka ajiwezeweze.

Alaa, sisi tunao kule watu wanaanika madagaa tu mbona hamuwasaidii, huyu mzungu katoka kwao kaja huku kwa nia ya kuja kuwekeza huo ndio uwekezaji wa aina gani, ana boti hilo kubwa kweli kweli linashuka siku moja moja, kalitengenezea njia nzuri mpaka baharini, lakini yeye huku anasema hana kazi masikini anaishi kwa kuombaomba hili boti analiendeshaje?

Mhe. Spika, mambo mengine yamezidi, tunaiomba sana serikali mwekezaji huyu arejeshwe kwao hawezi kuishi hapa. Hana sababu ya kuishi hapa, maana angekuwa mwekezaji angewekeza tukawa tunakusanya kodi serikali yetu inafaidika, lakini serikali haifaidiki chochote zaidi ya yeye anasema anaomba kwetu sisi, hee! Mimi sijawahi kuona hii Mhe. Spika, na inasikitisha sana

kabisa kama ndio taasisi zetu zina watu wa aina hii. Kumuuliza Mkurugenzi wa *ZIPA* anasema aa, wewe unamuona huyo mmoja tunao zaidi ya mia hawa. Aka! Nikasema sasa tumekwisha.

Sasa ndio maana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati alipokuwa akisoma hotuba yake aliiomba serikali imuagize *CAG* akaikague miradi yote 547 iliyokuweko kule *ZIPA* kama kweli inafuata yale masharti ya uwekezaji. Kwa sababu kama uwekezaji wenyewe wa aina hiyo tutakuwa tuna rundo la wageni ambao tunawaita wawekezaji lakini kumbe kuna rundo la wababaishaji hakuna kitu ambacho serikali itakuwa inapata.

Mhe. Spika, naona unataka kunihimiza, mimi naomba niishie hapo kwa hayo niliyoyasema. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kutia baraka zangu tu, maana yake hii ripoti nzuri na mimi naikubali mia juu ya mia. Lakini kwa sababu ni muumini wa Kamati ya *PAC* hata kama mara hii hukunichagua tena kuwemo katika kamati ile, lakini uzalendo Mhe. Spika, unanifanya niwe na hamu na haya mambo ambayo yanaripotiwa na *PAC*.

Mhe. Spika, malengo yetu na nadhani ndio malengo ya kila nchi ni maendeleo ya nchi pamoja na watu wake. Na maendeleo Mhe. Spika, hayawezi kupatikana bila ya kuwa na fedha, fedha ni muhimu sana katika maendeleo. Sasa sisi kama kawaida ya nchi nyengine yoyote inakuwa na vyanzo vyake vya fedha na ndio humo humo kupitia kodi za wananchi tozo nyengine, lakini pamoja na misaada na mikopo ya nje ndio vyanzo vyetu vya fedha.

Sasa tukishakupata hizo fedha Mhe. Spika, na tukawa tunazitunza vizuri ndizo hizi ambazo zinatusaidia kuboresha maendeleo ya nchi yetu, lakini na kuboresha maisha ya wananchi wetu ambao kwa kiasi kikubwa ndio wanaochangia hizo fedha zenyewe kwa sababu wao ndio wanaolipa kodi.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya *PAC* ukisoma huu muhtasari wao aliousoma Mwenyekiti pale lakini na ukisoma na ripoti yenyewe hasa na ripoti hii chanzo chake ni Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Kuna mapungufu mengi Mhe. Spika, na fedha zetu zinapotea sana na kuna njia kama tatu hizi ambazo ndizo zinazotumika kutupotezea hizi pesa.

Kwanza ni udhaifu wa wakusanyaji wa pesa hizi. Sijui ni ukosefu wa nyezo, sijui taaluma ndogo au ni uvivu wetu sisi wazanzibari, lakini kwa kifupi fedha hazikusanywi kwa mujibu wa mipango ambayo tumeipanga, pesa nyingi tunaacha bila ya kukusanya. Hilo ni tatizo moja.

Lakini tatizo la pili kuna udhaifu mwengine katika ukusanyaji na huu Mhe. Spika, unatuathiri sana kwa sababu ni kutokuwa waaminifu hawa wakusanyaji wa mapato, akikusanya kumi anasema kakusanya tano, tano anatia mfukoni. Sasa hili ni jambo la pili ambalo linatuathiri.

Na jambo la tatu ambalo ndilo Mwenyekiti amelipigia kelele sana ni matumizi. Zishakusanywa zishapelekwa Hazina sasa zinatumiwa kwa maendeleo ya nchi yetu, sasa hazitumiki kwa mujibu wa sheria. Mtu anatumia atakavyo tu, na tumeweka utaratibu wa kuwa na wahasibu na tunawasomesha sana ili wapate kutumia fedha kwa mujibu wa zile sheria ambazo tumezitunga hapa, lakini inasikitisha sana Mhe. Spika, Wahasibu wetu hawafanyi hivyo.

Nimeangalia ukurasa wa tano na sita kwa muhtasari ambao Mwenyekiti katusomea ame-*quote* Ripoti ya *CAG* kuna pesa nyingi sana Mhe. Spika, za wananchi zinatumiwa kiholela sana. Kuna shilingi 2,234,880,487.92 hizo zimetumika kinyume na utaratibu wa sheria za fedha. Na sheria yetu Nam. 9 ya mwaka 2005 wanapaswa wahasibu wetu watumie fedha kwa mujibu wa sheria ile, lakini inasikitisha Mkaguzi kila akienda kukagua matumizi ya fedha anakuta kuna makosa ya pesa nyingi kama hizi zinatumika kinyume na utaratibu, wakati huo wahasibu tayari tushawasomesha wana kila aina ya taaluma na nyenzo za kutumia vizuri hawatumii.

Lakini ukisoma ukurasa wa sita kuna shilingi 2,410,226,559 + *US$* 354 hizo zimetumika bila ya vielelezo au kuna vielelezo pungufu. Nayo pia ni kukiuka utaratibu wa matumizi ya fedha.

Mhe. Spika, zote hizo ukizikusanya ni shilingi 4,645,673,446.92 kwa mwaka zimetumika kinyume na utaratibu pesa za walipakodi wa nchi hii. Sasa hebu na tujiulize sisi kama ndio wasimamizi wa fedha za umma, hivi wananchi watatufahamu vipi? Wananchi watakuwa na moyo hata wa kulipa hizo kodi zao? Maana zile kodi wao ndio wanaichangia serikali, matarajio yao serikali inakusanya halafu inafanya maendeleo katika nchi yanayowarudia wale wale wananchi, lakini katika kiwango hiki cha fedha Mhe. Spika, kinatumika kinyume na utaratibu. Sasa hawa wananchi wetu tunawapa picha gani na suala hili linajirudia kila mwaka, kila mwaka wahasibu wetu hivi ndivyo wanavyotufanyia.

Sasa mimi nafikiri Mhe. Spika, ushafika wakati wa kumchukulia hatua kali kweli kweli Mhasibu Mkuu wa Serikali maana hawa ni watu wake, hawa wote wanawajibika kwake, lakini madhambi haya yanafanyika na ripoti anapewa Mhasibu Mkuu wa Serikali, lakini sijaona mhasibu yeyote kuchukuliwa hatua katika nchi hii, maana yake nini? Maana yake wao wana-*appreciate* labda wafanye hivi. Hatuwezi kufika Mhe. Spika, hata siku moja,

kama utaratibu ni huu, wewe unajua umuhimu wa risiti unakwenda kutumia unapewa risiti unashindwa kuhifadhi risiti ndio mfanyakazi gani wewe unayetufaa katika nchi hii, jambo dogo tu kama hilo.

Mhe. Spika, huko mbele ya safari tutapeleka hoja binafsi ya kutaka Mhasibu Mkuu wa Serikali aachie ngazi kazi imemshinda hawezi kuwadhibiti wahasibu wake, maana wale wanawajibika kwake yeye.

Jambo jengine niliona humu ameeleza Mwenyekiti wa Kamati kwamba moja katika matatizo ambayo yanaipotezea fedha nyingi sana serikali ni kutofanyiwa mapitio ile sera ya ukodishwaji ardhi kwa mujibu wa soko la sasa. Sasa hiyo nilipojaribu kuangalia hiki kitabu ukurasa wa 89 nimeangalia miradi sita tu ambayo kamati wameelea humu. Mkodishwaji huwa anajaza mkataba kwa kiasi fulani, lakini hatimaye wakati wa utekelezaji hicho kiwango hatoi anatoa chini ya kiwango na sijui anakubaliwa kubaliwaje, maana yake mkataba unasema hivi lakini yeye analipa hivi. Mimi hapa kwanza sifahamu, tumejaza mkataba mwekezaji alipe kwa mfano imeelezwa hapa alipe *US$* 9,000 kwa mwaka lakini mwekezaji huyo analipa *US$* 5,000 kinyume na mkataba. Serikali ndio iliyojaza mkataba huo, serikali ndio inayolipwa, kwa nini serikali ikubali kulipwa *US$* 5,000 badala ya *US$* 9,000 kwa sababu gani?

Mhe. Spika, hapa mimi napata mashaka na ndio ile niliyosema udhaifu wa ukusanyaji kutokuwa waaminifu wale wakusanyaji. Picha inayojengeka ni kwamba huyu mwekezaji amekubaliana na mtendaji fulani anayehusika na mapato bwana wewe lipa hiki mimi changu kitakuwa hiki, kuna wizi unatendeka humu. Sasa miradi sita hii nimejaribu kuangalia kwa haraka haraka zaidi ya shilingi 166 milioni kwa mwaka zinapotea kwa sababu ya upungufu tu, kajaza mkataba halipi kwa mujibu wa mkataba, na kama ni *ZRB* au ni nani anaridhia hilo na hii ni *sample* tu, miradi sita hii. Miradi katika nchi hii kama hii ya wawekezaji ipo zaidi ya mia ngapi. Kwa hivyo, kama utaikagua yote hiyo utakuta pesa nyingi sana Mhe. Spika, hazikusanywi na kumbe ndio tunakwenda na hiyo nakisi katika bajeti.

Kwa sababu wakati wa kufanya bajeti pesa zote hizi zinakuwa zimo katika matarajio na ndio maana tunapanga bajeti. Katika yale makadirio yetu hizi tunazihesabu kuwa zimo, lakini leo katika kulipwa zote zinakuwa pungufu, na hapa mimi nadhani watu wa *ZRB* kama ndio wao wanaohusika na kukusanya mapato haya basi na wao wanapaswa kuwajibishwa. Kwa nini hawakusanyi kwa mujibu wa mkataba, kama mikataba ile imepitwa na wakati kwa nini serikali haikai ikaandaa mikataba ambayo itatupa *figure* ambayo ndio itakayokuwa sahihi.

Sasa Mhe. Spika, mimi nakata tamaa sana kwamba ikiwa utaratibu wetu utakuwa ni huu, basi sidhani kama huko tunakokusudia kwenda tutafika, sidhani. Ameeleza hapa Mwenyekiti wa kamati, anasema ni asilimia 25 tu ya kodi ya ardhi ndiyo inayoingia serikalini ya makadirio ya kodi ya ardhi. Sasa ndio maana tunapita huko mawizarani tunakagua utekelezaji wa bajeti kila unapopita unaambiwa *OC* haziingii, sjui zinaingia kwa asilimia 20 sijui ngapi, matatizo ni haya Mhe. Spika, pesa hazikusanywi, inaonekana tuliowapa dhamana ya kukusanya pesa hawafanyi ipasavyo, na kama kazi hii hawajaiweza kuifanya, basi tusitarajie kwanza siku zote tutakuwa tunadanganyana tu hapa, waziri wa fedha atakuja na bajeti yake ina mabilioni mangapi, tunatarajia hayo ndio yatumike kwa maendeleo ya wananchi na wananchi wakisikia hivyo wanafurahi lakini *at the end of the day* inayopatikana hata *40 percent* haikamiliki. Kwa hivyo, ni bajeti iliyokuwa si ya kweli.

Mhe. Spika, mimi hata ningesema hapa mpaka asubuhi itakuwa ni kazi bure, nimejaribu ku-*highlight* haya ili wananchi huko wanaosikiliza wajue kwamba haya ndio matatizo tuliyonayo na ndio sababu ya umasikini wetu. Haiwezekani hata siku moja kisiwa chetu Mhe. Spika, tukawa masikini mpaka leo.

Juzi moja nilikuwa kule Uchina tulikuwa na *International Conference* mwezangu tuliyefuatana kule tukapata bahati sisi kuwasilisha *paper* katika ile *conference*. Katika *paper* yetu tukajaribu kuelezea umasikini tulionao na kwa hivyo tunajaribu kuuza pale ili wale watu wa kimataifa walioko pale watuonee huruma ikiwemo Serikali ya China yenyewe, basi kuna waziri mmoja kutoka Yemen bahati nzuri keshakuja hapa Zanzibar mara nyingi anaijua hii Zanzibar, akanivuta pembeni, akanambia nyinyi mnalilia umasikini nyinyi sio masikini, nyinyi pesa mnazo ukipata wakati nialike nije nikwambie pesa zenu ziko wapi, kabisa kabisa, na mimi sikuwa na hoja ya kumjibu kwa sababu wazembe Mhe. Spika, tunakwenda kama tulivyozoea tu, hatuwezi kuibadilisha nchi hii kwa kwenda hivi, lazima tubadilike.

Mhe. Spika, ahsante nakushukuru.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku ya leo kufika hapa katika hali ya afya njema. Lakini pia nichukue nafasi hii nimpongeze tena Mwakilishi wa Jimbo la Kiembe Samaki kwa kumuapisha hapa rasmi leo kwamba amekuwa mwenzetu katika Baraza lako tukufu, kuwa ni Mheshimiwa.

Mimi Mhe. Spika, maana hata sijui nianzie wapi, kwa kweli kwanza nimpongeze mwanamama huyu ambaye tumepata mtu mzuri, anafanya kazi zake vizuri. Sasa niombe serikali tusimbeze huyu mwanamama afanye kazi vizuri sana, kuhakikishia kwamba fedha serikalini zipo na mimi nathubutu kusema Mhe. Spika, sisi sio masikini pamoja na yote.

Lakini kuna watu maalumu wanaofanya serikali iwe masikini. Na kama tutakwenda katika hili Mhe. Spika, basi ni kweli basi hizo bajeti tunazozipitisha hapa itakuwa ni za bure. Tunapitisha bajeti kwa mintarafu ya kuhakikisha kila wizara inapata mafungu yake ipasavyo, lakini matokeo yake kwa ripoti hii bajeti haitokidhi haja. Sasa niwaambie tu usile na kipofu mpaka akakukamata mikono si vizuri.

Mimi nasema Mhe. Spika, jana nilizungumza kuhusu habari ya wawekezaji. Nilizungumza suala hilo kwa uchungu na leo nalizungumza tena. Hivyo, jamani kweli sisi hatuoni kwamba tunaitia hasara nchi hii? Maeneo yote yaliyoelezwa na humu tumetajiwa maeneo 119. Hakuna linalofanywa tujiulize kulikoni.

Kwa nini hatujachukua hatua? Amesemwa sasa hivi mwekezaji hapa ana boti kajenga kati kati ya mwitu hana kazi anayoifanya. Lakini kwa taarifa zisizoaminika Mhe. Spika, sasa juzi tumesomeshwa mambo ya TAKUKURU hapa wanisikilize vizuri hao TAKUKURU maana wanasema wanatusikiliza na sisi humu. Huyu mtu mimi nina wasi wasi kama haleti madawa ya kulevya bahati wasi wasi wangu mkubwa kwamba anatoka na boti usiku mkubwa hajulikani anakokwenda na halafu anarudi na boti.

Naiomba sana serikali na mimi nataka kumwambia Mhe. Waziri wa Fedha sisi tunamsaidia yeye lazima tuwe wakali humu. Wanasema kwamba serikali yetu fedha haina lakini fedha zipo. Mhe. Spika, kama unakumbuka kulikuwa na Kamati Teule na mimi nilikuwa miongoni, na tuliibua mambo mengi sana na ndio maana hata ile Bajeti ya Serikali ikaweza kupata fedha kidogo. Hebu na haya tuyafuatilie Mhe. Spika.

Naomba sana serikali jamani kuna siku hapa itakuwa "Kinakamsewe" kwa maneno yetu ya Kipemba. Kwa sababu tunasema lakini wanasema kuwa waache wapige kelele tu wale, kelele zao za bure tu. Ndivyo tunavyoambiwa Mhe. Spika, lakini sisi tumeletwa humu na wananchi lazima tuwatetee wananchi waliotuleta humu, kusema tutasema lakini kuna siku tutasema kweli. Maana tutakuja kufanya mambo humu ndani ya kushtumiana.

Mhe. Spika, nizungumze hayo hayo, mimi kila nikisimama hasa wakati wa bajeti jamani kuna matatizo gani ya kuweka kituo kimoja tu *one stop centre*.

Wenzetu wanaokuja wawekezaji wakajua tunakwenda hapa mambo yetu yote yatakamilishwa hapa. Lakini kila mmoja kajiweka ofisini kwake anangoja "njwenjwe njwejwe" sivyo. Mimi kwenye bajeti hii inayokuja kama sikuja kupata nikaambiwa kuwa *one stop centre* ni nani na nani kwa ajili ya wawekezaji wetu nitakuwa mgumu sana.

Mhe. Spika, nikitoka hapo ubora wa daftari la kudumu la Mali za Serikali. Tulikuwa tunatembelea maofisini hamna watu wanajinunulia vifaa haviingizwi katika daftari, ukiwauliza risiti ziko wapi hamna. Mimi nashanga jamani huu ndio Utawala Bora na mwenyewe Mhe. Waziri unasikia ndio Utawala Bora. Hebu tufanyie semina uje utwambie utawala bora na watendaji wako wote wawepo. Tujue Utawala Bora ni kitu gani.

Lakini leo mambo yanayofanyika maofisini Mhe. Spika, ni ya kusikitisha. Hebu jamani Mhe. Spika, naiomba serikali tubadilike ili tuendeshe kazi zetu kwa ufanisi. Lakini si hili tu Mhe. Spika, tumepitisha sheria za manunuzi humu kama ilivyosema ripoti ya Mwenyekiti. Lakini tujiulize nani na wangapi wanaoifuata? Ukiangalia maofisini haifuatwi na ndio maana ukaona upotevu mwingi wa fedha.

Nije katika suala la Mradi wa *TASAF*. Nishukuru tumepata tena huu mradi wa *TASAF*. Lakini nitoe indhari miradi mingi ya *TASAF* iliyopita na mwenyewe waziri kakiri humu kwamba fedha zilikuwa zinatumiwa kiholela. Watu wanapanga bajeti yao lakini ule mradi haufiki hata nusu mwaka fedha zimeshamalizika zimeshatiwa pua hii zikatokea mdomoni, na mdomoni tena zikaenda zake. Mhe. Spika, niiombe sana *TASAF* imerudi lakini kwa kweli tuitumie *TASAF* kwa manufaa ya wananchi si kwa manufaa ya watu binafsi. Nilisema na hilo nilizungumzie.

Lakini nije katika madeni ya taasisi mbali mbali ambazo wanadaiwa, hasa ya umeme. Hivyo kweli kuna taasisi zinadaiwa milioni mia mbili na tatizo la umeme Mhe. Spika, ukisema nitalipa mwezi unaokuja hulipi pesa zinaongezeka. Sasa niombe Waziri wa Fedha afanye utaratibu maalumu wa kuhakikisha kila taasisi pesa za umeme zinalipwa. Serikali haiendeshwi namna hiyo Mhe Spika, serikali ina mipango, inaendeshwa kwa mipango na taratibu na sheria.

Lakini niseme kwamba zamani kabla hatujajitawala nakusudia Mapinduzi bado. Tulikuwa tunaendeshwa na Wakoloni ukimuona tu mzungu anakuja wewe unatetemeka, kwa sababu alikuwa hana masihara. Mahospitali yalikuwa safi, makaro huyaoni ya nje. Lakini leo tuna wafanyakazi tukiwahesabu Mhe. Spika, tukipita humo majiani tunaona uchafu uliokithiri.

Niombe serikali wale *inspectors* wa zamani warudishwe kwa sababu kulikuwa na *inspectors* wanapita majumbani wanaangalia uchafu kama kuna watu wengine wamekaa tu tuwarudishe wafanye hiyo kazi. Haidhuru huko nyuma tulikuwa watu laki mbili mpaka laki tatu ndio, sasa dunia imekuwa watu wanazaliana, lakini utendaji wa kazi tujipangie kwa mujibu tulivyojiwekea.

Mhe. Spika, wezangu wamezungumza mengi lakini haya yote mimi nadhani taaluma yetu ndogo. Na sheria hazitumiwi ipasavyo, ingekuwa sheria zetu tunazitumia ipasavyo kwa mujibu wa taratibu basi yasingekuwepo haya. Lakini niseme hivi uwajibikaji hamna, pamoja na usimamizi tunakaa maofisini tunalegalega miguu tunatizama *TV* na ma-*internet,* lakini kufuatilia kazi zetu hatuzifuatilii. Hilo ndilo tatizo linalotupata, hatufuatilii kazi zetu ipasavyo, utakuja hapa kama ni Waziri utapewa na Katibu Mkuu au Mkurugenzi yanayoandikwa mle wewe mwenyewe hujayaona wala huyajui utayasema yale yale.

Niombe serikali utekelezaji na usimamizi ndio ufanisi wa kazi Mhe. Spika. Lakini kama tutakuwa na sisi tunakaa humu tunaambiwa kuwa waache waseme wale si watasema mambo yamekwisha. Natoa tena indhari Mhe. Spika, na sisi tulikuwa wafanyakazi tulianzia huko na yeyote anayeipenda kazi yake basi hakubali kufeli, lakini siku hizi hatupendi kazi tunapenda pesa. Mhe. Spika, niwaombe watendaji wote wa mawizara yote hebu tubadilikeni tufanye kazi kwa ufanisi na usimamizi wa hali ya juu. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, niseme sijui niunge mkono, na kama sikuunga mkono hayo mapendekezo tuliyoyatoa ndio yatafanyiwa kazi.

Niunge mkono ili haya maelezo yaliyoelezwa humu waende wakayafanyie kazi, lakini naiomba tena serikali bajeti hii inayokuja wajitayarishe Mwenyezi Mungu akitupa uhai na uzima wajitayarishe vizuri sana. Tusije hapa tuta, tuta tuta. Matuta hayo hayazai muhogo wala hayazai viazi ni tuta tu, tuta tu. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na nafasi ya kujadili ripoti hii muhimu.

Mhe. Spika, vile vile, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi kwa sababu mara nyengine hutokeza nikaomba kwa kusisitiza, lakini bahati mbaya sipati bahati ya kuchangia. Kwa hivyo, leo nakupongeza sana kwa kunipa nafasi hii.

Vile vile, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* na Kamati yake kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mhe. Spika, sasa nataka nianze mchango wangu katika ukurasa wa 4,5 na 6 wa kitabu cha ripoti ya *PAC* inayoelezwa ukiukwaji mkubwa wa nidhamu ya matumizi katika Kikosi cha KMKM.

Mhe. Spika, mfano hoja namba 19 ukurasa wa 4 kuna malipo ya shilingi 196 milioni yamefanywa kinyume na kanuni.
Mfano wa pili Mhe. Spika, kuna hoja namba 19.4 ukurasa wa 5 kuna ununuzi wa zaidi ya shilingi 113 milioni umefanyika eneo la Kantini kinyume na utaratibu.

Mfano wa tatu hoja namba 19.5 ukurasa wa 6 kuna malipo zaidi ya shilingi 135 yasiyokuwa na vielelezo.

Mhe. Spika, ukifanya hesabu hoja hizo tatu ni shilingi milioni 444 zimetumika vibaya na zimefujwa au zimeliwa na kikosi hiki cha KMKM. Mhe. Spika, msingi mkuu wa kikosi chochote cha askari ni nidhamu, na nidhamu kwa matumizi ya fedha za umma ni jambo muhimu sansa.

Ikiwa Mhe. Spika, yaliyogunduliwa na kamati ya *PAC* ni ya kweli na hatuna sababu ya kutilia mashaka kwa sababu ni kamati makini inayofanya kazi vizuri. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili ni lazima Baraza liondoe muhali hali hii.
Mhe. Spika, maoni ya kamati ni kwamba Ofisa Muhasibu wa kikosi hiki achukuliwe hatua za kinadhamu.

Mimi Mhe. Spika, kwa upande wangu nashauri kabla ya kuidhinisha Kikosi cha KMKM cha 2014/2015 basi Baraza liarifiwe hatua ambazo Ofisa huyu amechukuliwa. Vyenginevyo Mhe. Spika, tutapitisha bajeti na pesa hizo zitumiwe vile watu wanavyojua kinyume na sheria.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumzie liko ukurasa wa 7 hoja namba 20.4 inaelezea kwamba kikosi cha Valantia hakina utaratibu wa kukusanya mapato kisheria, kwa maana hakuna vitabu vya risiti vya mapato na pia hakuna daftari la fedha taslim.

Mhe. Spika, maelezo haya ya kamati yanashtusha sana. Kwa hivyo, utaratibu huu unaweza kuleta hisia mbaya na masuala ambayo majibu yake wanafanya aibu kubwa kwa kikosi hiki. Mhe. Spika, inaonesha hakuna *account* ya pesa zile. Je, matumizi yake yakishafanywa yanakaguliwa vipi hayo yote ni masuali Mhe. Spika, ambayo majibu yake ni magumu kwa mujibu wa nidhamu ya mapato na matumizi ya fedha za umma. Mhe. Spika, hoja hii inahitaji kufafanuliwa na kurekebishwa haraka.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 32 kuna hoja namba 31.2.1 inayohusu upotevu wa risiti za kukusanya mapato ya Halmashauri ya Kaskazini A. Mhe. Spika, tatizo hili la baadhi ya risiti katika Ofisi ya Halmashauri kupotea au kuchanwa halikufanywa kwa bahati mbaya. Mhe. Spika, waliofanya tendo hili walikuwa na dhamira mbaya ya kuficha ukweli juu ya usahihi wa makusanyo ya fedha na wapi makusanyo hayo yamepelekwa. Hili ni kosa kubwa la jinai.

Na hatua zilizochukuliwa Mhe. Spika, wanaohusika kuhamishwa sehemu moja na kupelekwa sehemu nyengine ni hatua hafifu, na hatua za namna hii haziwezi kutoa funzo kwa wale wengine waliokuwa wana tabia mbaya kama hii.

Mhe. Spika, serikali inapaswa iwe makini na mazoea ya aina hii, hizi ni pesa za umma za walipakodi hazifai kutumiwa namna hii. Mhe. Spika, utaratibu kama huu wa kupeana adhabu hizi ni utaratibu wa kuleana. Mhe. Spika, hii sawa sawa na kumwambia mtu wewe umeshapata chako kaa upande utumie ulichopata aje mwengine na yeye akusanye chake. Mhe. Spika, kwa hiyo, naomba serikali iwe makini sana.

Vile vile, Mhe. Spika, katika ripoti kuna maelezo yanayohusu ukodishwaji wa vituo vya mafuta vitatu vilioko chini ya mamlaka ya Mkoa wa Kaskazini Pemba ambacho ni kituo kimoja na vile vile Kusini vipo viwili. Mhe. Spika, ukodishwaji wa vituo hivyo haukuwa kwa mujibu wa sheria za fedha. Pia, mapato yanayohusiana na ukodishwaji huo yanafanywa kinyume na sheria.

Kwa vile Kamati ya *PAC* imeshagundua mapungufu hayo ninashauri ukodishwaji wa vituo hivyo visitishwe na baadae taratibu za wazi zifanyike kwa mujibu wa sheria. Mhe. Spika, hapa nina imani kubwa kama serikali itapata fedha nyingi zaidi kwa utaratibu huo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ni la mwisho naomba nimalizie ni ukurasa wa 67 mpaka 73 kuna hoja nyingi zinazohusu kasoro za Idara ya Majenzi na Utunzaji wa nyumba. Mhe. Spika, kwa kweli hoja zote zinasikitisha sana, lakini hoja mbaya zaidi ni hoja namba 58.5.4 ukurasa wa 69 inayoeleza:

" Hati zilizokosekana kwa ukaguzi wenye jumla ya zaidi ya shilingi milioni 340"

Mhe. Spika, kwa kweli kiasi hiki ni kikubwa wala haikubaliki, na kwenye ripoti ya *PAC* kwenye idara hii ya majenzi inaonesha idara hii imekubuhu katika kukiuka taratibu na sheria za fedha. Ikiwa serikali haitachukua hatua basi tutakuwa tunaleana na hatufiki tulipokusudia.

Mhe. Spika, naiomba sana serikali iwe makini, vyenginevyo miaka 50 imemalizika na 50 mingine itakuja tutabakia pale pale na kauli kwamba serikali ni changa. Lakini wanaozaliwa katika nchi hii wanazeeka na kufa serikali bado haijasimama dede. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ikiwa hapa serikali haitajipanga vizuri katika kuchukua hatua basi nadhani siku zote baada ya kusimama dede mwisho itarudi kitako na itambae kwa matako. Mhe. Spika, nakushukuru. (*Makofi*).

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia machache katika ripoti hii ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali.

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametulaza na kutuamsha tukiwa salama na afya njema na kuja katika Baraza lako Tukufu. Pia, naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Mwenyekiti wa kamati wa *PAC* pamoja na Wajumbe wake wote jinsi wanavyofanya kazi zao kwa umakini sana katika kutafuta jinsi fedha za serikali zinavyotumika.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze katika kikosi cha JKU ukurasa wa 10 hoja namba 21.1.2 ulipaji wa milioni 50. Mhe. Spika, kikosi cha JKU kwa maelezo ya kamati yanasema yamemlipa bwana Naushad milioni 50 baada ya kutamka kwamba kaibiwa pesa na vifaa vinavyofikia thamani hiyo ya milioni 50 wakati walinzi wa JKU ndio waliokuwa wanalinda katika nyumba yake.

Mhe. Spika, ripoti ya kamati inasema uongozi wa JKU mara tu baada ya bwana huyu kutamka kama kaibiwa pesa taslim pamoja na vifaa vinavyofikia milioni 50 walikurupuka tu moja kwa moja na kumlipa milioni 50 bwana huyo bila ya kufanya utafiti na kuthibitisha na kuhakikisha kwamba pesa hizi ni kweli zimeibiwa na bila ya kufuata tararibu za kisheria.

Mhe. Spika, hata kama huyu bwana kweli kaibiwa pesa hizi, lakini walikuwa hawana haja uongozi huu wa JKU kuchukua hatua tu ya moja kwa moja kulipa bila ya kufanya utafiti. Ripoti ya kamati inaonesha kama bwana mwenyewe huyu ndiye aliyefanya uchunguzi na kufanya hesabu zake mwenyewe na akawaambia tu kama mimi nimepotelewa na vitu vyenye thamani ya shilingi milioni 50 bila ya kujali na kufuata utaratibu wa kisheria. Sasa Mhe. Spika, katika hili kama uongozi wa JKU hivyo ndivyo unavyofanya kazi basi Mhe. Spika, serikali inatakiwa kuliangalia sana jukumu hili katika kutafuta viongozi wanaovisimamia vikosi.

Mhe. Spika, hizi ni pesa za serikali si pesa za mtu binafsi, kwa sababu mtu binafsi anapodaiwa tu na mtu wakati wowote ule basi ana haki tu ya kumpa

mwenyewe pesa zake anazomdai, lakini hizi pesa za serikali zinatakiwa zifanyiwe utafiti na zifuatiliwe kwa kina.

Mhe. Spika, nije kwenye hoja ya Chuo cha Mafunzo kwenye ukurasa wa 17 hoja namba 23.5 naomba nitoe maelezo hapa kidogo.

Ripoti ya Kamati inasema kuna matumizi ya zaidi ya shilingi milioni 140 yamefanyika bila ya kufuata utaratibu wa kisheria. Mhe. Spika, pesa hizi ni nyingi na ingelikuwa pesa hizi zilitumika kinyume na utaratibu, lakini angalau kwa mambo maalumu, kwa mfano ingelikuwa zilitumika pesa hizi kwa sababu ya kukosekana kwa chakula kwa wanafunzi walioko Chuo cha Mafunzo, jambo ambalo tunalipigia kelele kila siku tungelitetea.

Pengine zingetumika pesa hizi Mhe. Spika, kwa kujenga ukuta tuchukue mfano ukuta wa jengo lile la wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo umevunjika. Sasa ikawa wanahofia wanafunzi wale kutoroka labda na kuingia mashaka mengine pia tungetetea. Lakini la kusikitisha sana Mhe. Spika, pesa hizi zimetumika milioni 140 bila ya kufuata utaratibu kwa kununua gari la Kamanda. Mhe. Spika, hili jambo naona tunalifanyia masihara.

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alisema tuache kufanya kazi kwa mazoea lakini naona bado tunafanya kazi kwa mazoea. Kwa hivyo, huu ni mzaha, huu ni mchezo na hapa ripoti ya kamati inatakiwa kuheshimiwa kwa kuchukuliwa hatua zinazofaa waliohusika na matumizi haya bila ya utaratibu.

Mhe. Spika, nataka nije kwenye sehemu nyengine ukurasa wa 40, 41,42 kwenye suala la wazee wasiojiweza hoja namba mbili 16.2. Katika hoja hii kuna hoja ya kutupiana mpira baina ya viongozi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na viongozi wa Mkoa wa Kusuni Pemba juu ya ongezeko la matumizi ya shilingi milioni mbili na elfu kumi.

Mhe. Spika, uongozi wa Mkoa wa Kusini Pemba unasema pesa hizi haziwahusu hawajaziona hazijaingizwa, na uongozi wa Kaskazini Pemba wanasema haziwahusu sasa hapa wanatupiana mpira hajulikani nani katumia nani hajatumia. Lakini kwa bahati mbaya au bahati mzuri Ofisi ya *CAG* inathibitisha usahihi wa matumizi na uingizwaji wa pesa hizi. Hapa kidogo nimefanya wasiwasi Mhe. Spika.

Wasi wasi wangu ni maamuzi, ni maamuzi ya Kamati ya *PAC* kusema kama Ofisi ya *CAG* irudie tena katika kuthibitisha hili. Wakati Ofisi ya *CAG* tayari imeshathibitisha usahihi wa matumizi yake na fedha hii. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti, atakapokuja hapa anithibitishie ni kwa nini aelekeze kama

Ofisi ya *CAG* ifanye tena uchunguzi kwa matumizi ya shilingi milioni 2.1, wakati *CAG* wenyewe wameshathibitisha.

Mhe. Spika, naomba nije ukurasa wa 84 kwa hoja namba 2, ukarabati wa nyumba za maendeleo Wete. Ripoti ya Kamati inasema kwamba zaidi ya shilingi milioni 110 zilitengwa na kuingizwa kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za maendeleo. Mhe. Spika, ripoti hiyo hiyo ya Kamati inasema pesa hizi hazikutumika kwa lengo lililokusudiwa.

Mhe. Spika, nataka niseme nyumba hizi za maendeleo za Wete na hata katika bajeti iliyopita nililizungumza, zile nyumba ni mbovu na zinahatarisha maisha ya watu, lakini bado Serikali naona haijataka kuliona hili. Sasa Mhe. Spika, naomba nikuthibitishie kama wiki mbili za nyuma sehemu ya nyumba hizi imekatika na kuanguka na kuleta mtarafuku mkubwa, na ni hatari kwa watu wanaoishi ndani ya nyumba zile na wapita njia.

Sasa ushauri wangu Mhe. Spika, katika hili naomba sana Serikali iwahamishe haraka wananchi wanaoishi katika nyumba zile kabla halijatokezea jengine. Kawaida yetu tumezoea kila siku tusubiri maafa tupite kwenye majumba tukiwahani watu. Mhe. Spika, natoa indhari sana kwa Serikali walione hili. Ile nyumba iko katika hali ngumu sana, kwa sababu majumba ni makubwa, ya zamani, mabovu na ni ya kutisha kiukweli. Sasa Mhe. Spika, tusisubiri tukaunda Tume, haya mambo ya kuunda Tume hayatusaidii isipokuwa tunawatonesha vidonda wananchi wetu kila leo.

Mhe. Spika, kidogo niingie katika Soko la Tumbe katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Soko hili la Tumbe lilijengwa kwa umadhubuti sana katika hatua za mwanzo. Na katika ukaguzi aliokwenda kukagua Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika sherehe na wale aliofuatana nao walilisifu sana lile jengo kwa umadhubuti wake. Lakini Mhe. Spika, inaonesha jengo hili katika umaliziaji wake yaani *finishing* umeripuliwa na umetumiwa visivyokuwa.

Sasa Mhe. Spika, jambo linalotusikitisha katika jengo hili la Tumbe kwanza hapa pamefanyika mambo mawili. Jengo lilikuwa likabidhiwe matarajio yalikuwa Agosti/Septemba, 2011. Na wakati huo huo palikuwa tayari pameshanunuliwa majokofu kwa ajili ya kuhifadhia samaki pale, lakini majokofu yale hatujui yamepelekwa wapi na jengo hilo mpaka hivi juzi Kamati inapitia bado halijakabidhiwa. Sasa hapa naomba niulize swali. Ni lini jengo hili litakabidhiwa na majokofu yale yapelekwe kwa jinsi walivyokubaliana mwanzo?

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kusema kuna Sheria ya Manunuzi na Matumizi ya Fedha za Serikali. Lakini kwa bahati mbaya sana katika taasisi

nyingi za Serikali sheria hizi hazifuatwi na inapelekea uharibifu au kupotea kwa pesa nyingi za Serikali. Wawakilishi wanakuja hapa, Kamati ya *PAC* inafanya kazi zake kikamilifu, tunapiga makelele, lakini matokeo yake pesa zinapotea tunabakia omba omba, wakati nchi yetu hii ni ndogo sana hatuna haja ya kupita tukiomba. Hizi fedha zinazopotea Mhe. Spika, ni nyingi kuliko hizo tunazopita tukiomba. Kwa hiyo naiomba sana Serikali iwachukulie hatua wale wote wanaoonekana wanatumia pesa kinyume na utaratibu ili nchi yetu iende mbele, tusibakie kila siku kusema sisi maskini, wakati sisi ni matajiri wa kila hali.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nasema naunga mkono hotuba hii na ripoti hii ya Kamati ya *PAC* asilimia mia kwa mia.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kwenye Kamati hii ya *PAC* ambayo nafanyia kazi nikiwa kama Makamu Mwenyekiti.

Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii nimpongeze Mhe. Mwenyekiti kwa kuwasilisha ripoti yetu hii kwa ufasaha na uwezo mkubwa. Vile vile, nimpongeze Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, kwa kuapishwa rasmi leo hii kuwa Mjumbe wa Baraza lako tukufu kupitia Jimbo la Kiembesamaki.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja ambayo imewasilishwa mbele yetu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Spika, niende kwenye udanganyifu ambao unatokana na viinua mgongo. Ni kweli ripoti hii imo katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo ni moja ya changamoto zinazoikumba Serikali yetu.

Mhe. Spika, vile vile, kumejitokeza kutokufunga mahesabu kwa taasisi za Serikali. Pia, hili ni tatizo kubwa kwa nchi yetu kwamba taasisi zetu zinashindwa kufunga mahesabu mwisho wa mwaka na kila kitu kipo wazi. Sheria inataka kwamba kila ifikapo tarehe 30 Septemba basi hesabu hizi ziwe zimeshakamilika na kupelekwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Lakini taasisi zetu zinakwenda kama alivyosema mwenzangu sasa hivi tuondokane na ile kufanya kazi kwa mazoea. Kwa sababu tunafunga hesabu zetu mwisho wa mwaka Juni, lakini watu wanakuwa bado wanangojea. Kwa kuwa *deadline* imesema kwamba ni tarehe 30 Septemba hesabu hizi ziwe zimeshapelekwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini bado kunakuwa na taasisi anangojea mpaka ile siku ya mwisho. Wakati binadamu tunatakiwa tusijiweke hivyo, ufanye kazi zako mapema kwa sababu linaweza likatokea lolote. Na ndio huwa tunaambiwa sana mtu ukiamka

asubuhi basi upate japo kile kikombe cha chai, kuwa linaweza likatokea jambo usiweze tena kuendelea.

Vile vile, nikienda na hoja ya 58 (5.3) Idara ya Utunzaji wa Nyumba. Mhe. Spika, kuna fedha hizi zilikuwa zina tofauti baina ya vocha zenyewe husika na fedha ambazo zimetolewa benki. Kwa kweli hili ni tatizo Mhe. Spika, na niseme kwamba huu ni wizi wa macho macho. Na niwatake Makatibu Wakuu, Wakurugenzi kwa sababu hili suala linakuwa linahusu Wahasibu. Kuna Wahasibu wale ambao si waadilifu na tumeyaona kwamba pesa zile karibuni milioni 163,580,000/= zimeibiwa na hawa Wahasibu.

Kwa kweli niwatake Makatibu Wakuu wawe na tahadhari na hili kwa sababu hapa mtu anamuandikia kwa makusudi. Tena wazingatie kweli ile cheki anapopelekewa Katibu Mkuu au Mkurugenzi basi asiwache hata kinafasi kidogo, kwa sababu hapa ndio panapocheza mchezo. Tumeona kwamba pale mtu anaandika *8 million* na baadae akirudishiwa Mhasibu mwenyewe anatia ile *18 million.* Kwa hivyo, hapa nawasisitiza Makatibu Wakuu wawe makini sana kwa sababu hapa inaonekana Wahasibu wenzangu kidogo wanakuwa wanacheza mchezo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, na hii *internal control* inatakiwa. Kwa sababu baada ya kuwa hivyo ile *internal control* yenyewe inakuwa haipo.

Vile vile, kuna taasisi zetu nyingi ambazo zinakosa kitengo kile cha manunuzi ambalo ni tatizo na ndio maana tunapiga kelele wakati wote kwamba hatuoni kitu gani kinaendelea, bado tunajikuta tupo katika matatizo. Na Kamati yetu hii inafanya kazi kwa muda mkubwa ambao kama alivyosema Mwenyekiti wangu kwamba hatujali wakati, wala hatujali posho. Hata tunapokwenda kubadilishana uzoefu na wenzetu, Kamati hii inafanya kazi sana. Ni lazima taasisi zetu zibadilike kwa kufuata sheria hizi za manunuzi.

Nikenda kwenye ukaguzi yakinifu, kuna wawekezaji ambao wamepewa maeneo, lakini bado hawajayaendeleza. Mhe. Spika, niseme kwamba kuna wengine hawa kwa kweli wanakuwa si wawekezaji. Hawa ni madalali, wanachukua ardhi kwa lengo la kuziuza ambapo kisheria haikubaliki.

Mhe. Spika, tumekwenda maeneo mengi ambayo tumeyakuta katika kadhia hizi. Ni imani yetu kwamba maeneo haya kama yatafanya kazi kama yalivyoombwa, basi tungekuwa na maendeleo makubwa katika nchi yetu. Kama walivyosema wenzangu kwamba ardhi ni mali, na ardhi mpaka yale maeneo ya maji pia tunahesabu kwamba ni ardhi. Lakini vile vile tunakuta kwamba kuna jeti zimejengwa na hizi zitakuwa zimejengwa kinyume cha sheria kwa sababu hazilipi ile kodi ya ardhi.

Mhe. Spika, wenzangu wamesema kuhusu hii Hoteli ya *Manta Reef* yenye chumba cha chini ya bahari. Na bado kama zile jeti zilivyokuwa zimekosa uhalali na nasema na chumba hiki pia kimekosa uhalali wa sheria.

Na tulipokwenda pale kuuliza kwanza ile *process* ya *EIA* haijachukuliwa na vile vile kibali ardhi wenyewe hawajatoa. *ZIPA* imetoa kibali wameshirikiana na *PECA* ambaye si mmiliki wa ardhi. Mhe. Spika, kama sheria zimeshaanza kukiukwa hapa, na hii ni uwekezaji ambao matarajio yangu kwamba hata wageni watakwenda kutembelea maeneo yale. Je, Mhe. Spika, kama litatokea lolote kwenye chumba kile, mfano mtetemeko kule chini ya ardhi, kama kutakuwa na wageni mashuhuri tumewapeleka, hatuoni kwamba tutakuja kushindwa kujibu mbele ya mataifa.

Na kwa sababu ninavyojua mimi kwamba jambo lolote unapolianzisha kunakuwa na taasisi ambazo zinasimamia kitaifa na kimataifa. Je, haitokuja kuwa ni mzigo kwetu sisi, ikiwa sisi wenyewe ndani tumeshakiuka zile taratibu na sheria. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili ni jambo ambalo la kuzingatiwa, tutahadhari kabla ya athari.

Mhe. Spika, kuna mambo mengi ambayo yamo katika Kamati hii yameelezewa katika ripoti hii. Na kwa sababu mimi mwenyewe ni Mjumbe wa Kamati hii nisingetaka kuzungumzia sana kwa sababu mengi yameshazungumzwa. Naomba kuwaachia Wajumbe wenzangu ili waichangie ripoti hii na waikubali. Na vile vile, Mawaziri wasikilize sana hizi changamoto ambazo tumezileta hapa. Sisi nia yetu kama Kamati ni kuisaidia Serikali, na wao Serikali wayatizame yale matatizo ambayo tumekuja nayo basi wayafanyie kazi.

Mhe. Spika, baada ya hayo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Amani naunga mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nitazungumza mawili matatu pamoja na kidogo sauti yangu haiko vizuri lakini naamini itasikika.

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tena leo kukutana hapa katika Baraza letu la Wawakilishi kwa ajili ya kujadili Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika *(PAC).* Kwa hivyo nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Omar Ali Shehe pamoja na Wajumbe wake wote wa Kamati kuweza kufanya shughuli hii ngumu. Shughuli ya uchunguzi Mhe. Spika, ni shughuli ngumu na pevu na inahitaji ujasiri na umakini wa kweli kweli.

Kwa sababu binadamu ndio sisi, tunaochunguzwa ni binadamu, tungekuwa tunayachunguza makundi ya wanyama basi tusingepata shida, lakini binadamu wana kila aina ya mbinu. Na hawa tunaowachunguza ni wataalamu wamesomea, wengine wana madigrii, wana mashahada mbali mbali. Kwa hivyo, tunaamini kwamba wanafanya kazi ngumu na kwa sababu hatimae wanakuja na ripoti hii ambayo ina mambo mengi yaliyojaa vielelezo vingi sana. Kwa hivyo, hatuna budi kuwapongeza.

Lakini pia, tuwapongeze wenzetu wa *CAG* nao kwa kufanya shughuli hizi ambazo kwa pamoja wanashirikiana ili kuandaa ripoti hii na kuwasilishwa kwa Mhe. Rais hadi sasa inafika hapa kwetu kwa ajili ya kuijadili.

Mhe. Spika, kabla sijasema chochote nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Mwakilishi mpya wa Jimbo la Kiembesamaki, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, kwa kuchaguliwa kuwa Mwakilishi katika uchaguzi uliopita juzi. Naamini wananchi wa jimbo lile wameangalia, wamesikiliza na wameona kwamba iko haja ya kumchagua Mwakilishi kutoka Chama cha Mapinduzi na kwa sababu bado ana imani na chama hicho na inaonekana bado sera zake zinakubalika na wananchi. Sera zetu bado hazijapitwa na wakati, bado zinakwenda na wakati.

Mhe. Spika, ripoti hii imesheheni mambo mengi ambayo kwa upande mmoja unayakuta ni mambo yanayojirejea rejea. Makosa yaliyokuwemo humu ni makosa ambayo kila siku yanajirejea rejea. Sasa sijui wenzetu hawa inakuwaje. Tunaona humo malipo yasiyokuwa na stakabadhi, malipo yasiyofahamika. Mhe. Mwenyekiti, alipokuwa akitoa taarifa pale alitueleza kwamba karibu shilingi bilioni 2 kwa jumla hazieleweki zilitumika vipi. Kiwango cha shilingi bilioni 2 kwa nchi maskini kama yetu ni kiwango kikubwa sana ambapo mahesabu yake, na matumizi yake hayaeleweki.

Kwa wenzetu nchi tajiri bilioni 2 si chochote, si lolote. Lakini kwenye nchi kama hii ambayo makusanyo yake ya mwaka bilioni 300, basi kama bilioni 2 zinapotea hazijulikani zilipo wala hazieleweki mahesabu yake jambo hili sio la kulipuuza. Inahitajiwa Serikali iwe makini katika suala hili, ilifanyie kazi na kuona kwamba ripoti ijayo basi kusijitokeze mambo kama haya. Na sisi tunawaambia wenzetu tunaoongoza Serikali na chombo hiki kwa pamoja, lazima tuwe na mashirikiano makubwa kupambana na hali hii.

Fedha hizi ni za walipa kodi, tunahangaika, tunakusanya kwa tabu, tunapigishana kelele, lakini hatimae wale watumiaji sasa hawataki kufuata taratibu za matumizi, na matumizi yana sheria zake. Na hili ni jambo la kusikitisha kuona bado makosa kama haya yanawasilishwa kila mwaka. *PAC* wanapotuwasilishia ripoti hizi, basi kila mwaka ripoti hizi zinajirejea rejea.

Sasa hili ni jambo ambalo linasikitisha sana. Mimi naamini kama Serikali itakuwa *serious* katika kusimamia jambo hili lisitokee, inaweza. Lakini inaonekana bado hakujawa na hatua madhubuti juu ya kupambana na jambo hili.

Mhe. Spika, fedha hizi ni kodi za wananchi na zinakusanywa kwa ajili ya maendeleo yao, na si kwa ajili ya maendeleo ya mtu. Na bado nchi yetu inahitaji ina matumizi mengi ya muhimu na ya lazima. Juzi tu hapa tulikuwa tunazungumzia suala la Wizara ya Afya fedha wanazoingiziwa na umuhimu wa afya katika jamii, maji, elimu. Sasa pesa zenyewe tunazozizungumzia ndio hizi ambazo kama zingetumika vizuri zingetusaidia kuona zinatumika kwa ajili ya manufaa ya watu wetu. Sasa mimi niiombe Serikali, nimuombe sana Mhe. Rais wa Zanzibar ambapo hatua ya kwanza inapitia kwake asimamie kuhakikisha makosa kama haya yanapigwa vita, ili kusiwe na marejeo ya taarifa kama hizi.

Mhe. Spika, nilikuwa namuuliza hapa Mjumbe mmoja wa *PAC.* Mbona ripoti hii inaonekana baadhi ya maeneo hayakuguswa? Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati imeguswa guswa, hivyo maeneo mengine ndio yapo safi, yapo salama? Akanambia kwamba hawakupata muda wa kutosha. Kwa sababu katika ule muda waliopewa walijaribu kuangalia katika maeneo haya ya ardhi zaidi. Kwa hivyo hawakupata muda wa kutosha kwa kumalizia kuangalia ripoti za Wizara nyengine.

Sasa kwa kweli Mhe. Spika, kuna haja ya kuwapa muda zaidi wenzetu hawa ili waangalievya kutosha. Kwa sababu maeneo haya ni muhimu, kama hayajakaguliwa ipasavyo maana yake mambo haya ya ubadhirifu kwa mali za umma yataongezeka. Sasa hizi tunakagua na matokeo ndio haya. Kama tukiacha kabisa kufanya shughuli za ukaguzi, basi tena mambo yatazidi kwa sababu itaonekana kwamba fedha hii haina mwenyewe. Kwa hivyo wapewe muda zaidi ili wakamilishe kuzipitia ripoti hizi za Mawizara mengine, ili nao tuone hali ya utendaji wao na shughuli zao za kila siku zinavyokwenda.

Mhe. Spika, ripoti ilizungumzia zaidi katika maeneo ya ardhi ambapo inaonekana kwamba fedha nyingi katika maeneo ya ardhi hazikusanywi. Lakini pia, imeonekana kwamba hakuna taarifa sahihi juu ya matumizi ya ardhi. Sitaki kufafanua eneo baada ya eneo, ningependa niyazungumzie haya kwa ujumla. Kinachoonekana kuna watu wamepewa ardhi, lakini hawaeleweki, hesabu zao hazieleweki, kinacholipwa hakieleweki. Kuna wengine wanafutiwa hati za umiliki wanapewa watu wengine lakini hakuna kumbukumbu zilizokuwa sahihi zinazoonesha kufutwa kwao zile ardhi na kupewa watu wengine. Yaani imekuwa kama vile sijui tuko kwenye karne ile ya zamani.

Mambo haya kwa kweli kwa wakati huu tuliokuwa nao ukielezwa basi unapatwa na kigugumizi. Kwa sababu katika karne ya leo huwezi kwenda kwa utaratibu huo. Zama hizi za sayansi na teknolojia, hivi leo mtu anapewa ardhi basi haeleweki, taarifa zake hazifahamiki, kapewa nani, kalipa nini, kalipa kwa utaratibu gani, sheria inasemaje. Ni mambo ambayo hayakubaliki katika karne hizi na haya yanaonekana ndio mengi.

Kwa mujibu wa ripoti za *PAC* hayo ndio yaliyotawala. Na kama wao wameweza kugundua haya basi kuna mangapi ambayo yapo. Wenzangu hapa wamesema kwamba nchi yetu hii haina umaskini wa kiasi hicho, fedha zipo nyingi lakini tatizo ni namna ya kuzifuatilia hizi fedha zilipo. Kinachopatikana ni kidogo kuliko ule uhalisia wa kilichopo. Sasa kwa kweli hii inasikitisha sana.

Naiomba serikali kupitia taasisi mbali mbali, taasisi ya ardhi ambayo ndio imetajwa hapa, basi ifuatilie hiyo rasilimali hii ya nchi. Wageni wanakuja hapa wanahodhi maeneo wanajinufaisha, wanaweka biashara zao lakini zile kodi zinazostahiki kulipwa kwa manufaa ya wananchi wa nchi hii hawalipi. Na hawa wanatusoma sisi juu ya *seriousness* yetu tuliyokuwa nayo. Wamekuwa wakitusoma wanaona hawa Waafrika hawapo *serious* katika kufuatilia mapato yao.

Kwa hivyo, na wao wanaitumia *loop hole* hiyo kubabaisha-babaisha. Mtu anakwenda kupewa kijieneo kidogo, anapewa hati pale lakini baadae anafungua *extension* anakuwa na eneo kubwa lakini kodi anayolipa ni ile ile. Wengine wanamilikishwa ardhi kwa muda mrefu hawajaanza kuwekeza, hawalipi chochote, ardhi wanaendelea nayo miaka kumi mpaka kumi na tano. Kwa hivyo, mambo haya ni lazima Wizara ya Ardhi Mhe. Waziri anayehusika na masuala ya ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, waone kwamba mambo haya yanashughulikiwa ili rasilimali hii iweze kutumika kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar.

Sisi Mhe. Spika, nchi yetu haina rasilimali nyengine, hatuna madini sisi, dhahabu wala almasi wala wanyama pori. Rasilimali yetu ni hii ardhi na masuala ya uwekezaji. Uchumi wetu unatakiwa utokane na ardhi na uwekezaji kwa ajili ya kuendeleza nchi yetu. Lakini sasa kama tutakuwa tunapuuza, tunaachia, hatujui kitu gani kinalipwa, nani kalipa, kwa kweli tutakuwa hatuwafanyii vyema wananchi wetu.

Wananchi wametukabidhi hii nchi ili tuzisimamie raslimali zilizopo, tusimamie mapato yao, tusimamie kila kitu kwa manufaa yao. Sasa kama sisi tuliopewa dhamana hiyo na wananchi kwa kusimamia hii, wenzetu huko wamekaa wanashughulika na yao. Sisi Wawakilishi tumepigiwa kura

wakatwambia hebu nendeni mukaisimamie serikali. Tumekuja hapa kwa ajili ya kuisimamia serikali na tunatakiwa tuisimamie hasa, tuhakikishe kwamba serikali inatimiza wajibu wake.

Lakini na serikali nayo sasa itimize wajibu wake. Inakuwa si vizuri kila wakati Mhe. Spika, tuwe tunasukumanasukumana. Leo asubuhi umeshuhudia pale benchi ya mbele yote haipo. Hiyo inaonesha *how serious* tulivyokuwa, benchi yote haipo. Kwa hivyo, wanatuangalia na wanatuona.

Sasa mambo haya ripoti hizi za *PAC* ambazo zimewasilishwa kwa serikali, zinatakiwa zifanyiwe kazi kisawa-sawa. Haipendezi hata kidogo kuona kwamba ripoti hizi tayari zimesomwa, zimeelezwa lakini hatimae makabrasha haya tunayafungia samaki. Ripoti hizi zinatakiwa zifanyiwe kazi, na Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu tuisimamie kisawa sawa kupitia ripoti hizi. (*Makofi*).

Vyenginevyo tutakuwa hatutimizi ule wajibu wetu. Wajibu wetu ni kuhakikisha tunaisimamia serikali, serikali nayo inasimamia watu wao ili kuona shughuli zote zinakwenda vizuri kwa manufaa ya watu wetu. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nisitumie muda wako mwingi, nimejadili ripoti hii kwa ujumla na baada ya kuona mambo mengi yanajirejea rejea nisingependa kuchukua kifungu baada ya kifungu. Ni mambo ambayo ni ya kawaida yanakuja siku zote lakini ninasema kwamba hayapendezi, kwamba hayapungui.

Lakini eneo moja Mhe. Spika, la mwisho ningependa kulizungumzia humu, nimelitafuta sikuliona, sijui hawakwenda. Sasa hivi tuna athari kubwa juu ya ongezeko la bei ya umeme nchini. Ongezeko hili Mhe. Spika, linatisha na itafika pahala wananchi watashindwa kulipa umeme, watarejea kule nyuma wanakotoka kwa kutumia vibatari. Ni hatari.

Juzi tumepandishiwa umeme lakini tumetolewa tahadhari nyengine kwamba ikiwa *TANESCO* watapandisha tena, shirika (*ZECO*) litapandisha tena. Eneo hili linahitaji kufanyiwa kazi kwa sababu bado tuna wasi wasi. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali inaonekana halifanyii kazi shirika hili.

Taarifa tulizokuwa nazo, makusanyo yao ya mwezi ni zaidi ya bilioni tano. Lakini leo nimesikia kwenye redio asubuhi imenitisha, *EWURA* kupitia Shirika lake la *TANESCO* limetishia kwamba itaikatia umeme Zanzibar. Watatukatia umeme kwa sababu hatulipi.

Hivi taarifa kama hizi za kupuuza! Makusanyo yanayokusanywa na Shirika la Umeme nayo si madogo ni makubwa. Kwa nini fedha hizi zisipelekwe kunakostahili? Matumizi tunayotumia kwa mwezi tunaambiwa ni bilioni tatu, tunakusanya bilioni tano, maana yake zile bilioni mbili zilizobakia ndio *cost* za shirika.

Hapa panatakiwa ofisi ya *CAG* wafanye kazi. Bado tuna wasi wasi juu ya kodi zinazokusanywa lakini bado tuna wasi wasi na matumizi yanayotumiwa na Shirika la Umeme. Hivyo, Ofisi ya *CAG* sasa hivi ielekeze nguvu zake kuona fedha zinazokusanywa na Shirika la Umeme ni kiasi gani, na matumizi yake.

Mhe. Spika, kwa mfano kuna fedha ambazo zinatolewa, wenyewe wana utaratibu wao. Pemba zinatolewa kwa siku milioni mbili na Unguja milioni mbili kwa ajili ya matumizi ya dharura. Kwa hivyo, Pemba karibu milioni sitini na Unguja milioni sitini. Lakini unapoingia *deep* unakuta yale matumizi yenyewe yalivyotumika na milioni hizo sitini huyaoni. Ni pesa tu ambazo zinatolewa, pakiharibika pakitengenea, kila siku milioni mbili zimetumika. Kwa hivyo, matumizi ya Shirika la Umeme ni lazima yachunguzwe. *Unless* tutalala giza hapa, kama hiyo ni hali yetu tuliyokuwa nayo, kuoneana aibu, kuoneana haya, kuoneana muhali iko siku tutalala giza. (*Makofi*).

Umeme unalipwa, wananchi wanalipa pamoja na ughali, fedha zinapatikana, kwa nini tushindwe kulipe gharama za umeme. Mbona za majumbani mwetu tunalipa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Waziri wa Ardhi anayesimamia Shirika la *ZECO* tusioneane muhali, tusione taabu kulisimamia hili. Hizi *units* tunazogaiwa, zisitufanye kushindwa kusimamia. Kwa sababu tunapata taarifa huko kuna *units* huwa zinagaiwa, sijui kila mjumbe wa bodi kwa mwezi anapewa sijui *units 200*, sijui anapewa *cash*, munapeanapena huko *units* tu! Na haya ndio yanayosababisha mushindwe kulisimamia hili shirika, kwa sababu tayari wanakufadhilini hawa kwa kuwapa umeme bure. Hii ni hatari.

Kwa hivyo, lazima shirika hili lisimamie matumizi yake. Haturidhiki kabisa kama Wawakilishi wa wananchi, haturidhiki kabisa juu ya mwenendo wa Shirika la Umeme. Tumeyasema huko nyuma na tutaendelea kuyasema, japo wapo wanaokasirika lakini wajibu wetu ni kusema. Mimi kwanza sipo hapa kwa ajili ya kumfurahisha mtu Mhe. Spika. La ukweli tutasema tu. Kama hili lina ukweli, hili lina uwongo. Tupo hapa kwa ajili ya kutimiza wajibu wetu ambao wananchi wametutuma huko. Anayefurahi atafurahi, atakayeudhika mwache audhike. Lakini tuhakikishe kwamba nchi hii inakwenda vizuri kwa ajili ya manufaa ya wananchi walio wengi. (*Makofi*).

Baada ya maelezo ya hayo Mhe. Spika, mimi ninaunga mkono ripoti hii ya mwenyekiti pamoja na kamati yake na niiombe serikali iifanyie kazi. Na kama alivyozungumza Mhe. Hamza Hassan Juma, kwamba ripoti hii sasa tutaifanyia kazi wakati wa bajeti *Inshaallah* tukijaaliwa kufika siku hiyo. Mimi ni mmoja wapo kuhakikisha imetekelezwa kwa manufaa ya watu, hatuwezi tu kutumia kutengeneza vitabu kama hivi, hiki kitabu chenyewe kimetengenezwa kwa gharama, hizi ripoti zilizomo nazo zimegharimu pesa nyingi.

Kwa hivyo itakuwa ni jambo la kipuuzi kuona kwamba yameletwa hapa, hatuyafanyii kazi, wananchi wanatutegemea sisi, itakuwa jambo hilo hatuwafanyii haki na hata kwa Mwenyezi Mungu basi tutapata dhambi.

Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa ripoti hizi tusizipoteze tukazisome kuanzia leo, ilimuradi itakapofika wakati wa bajeti sisi ndio wakati wetu. Tutaikamata wizara inayohusika na mambo haya na Mhe. Spika, tunakuomba mwaka huu tuachie. Tunamaliza mwaka wa tano wa mwisho, itakuwa si vyema kwamba tunamaliza hatujamkamata koo mtu hapa.

Kwa hivyo, hata lile teke la mwisho linakuwa lina hatari, ni lazima limtoe mtu roho. Kwa hivyo, na sisi tutakwenda na mtu. Mambo haya hatuwezi kuyaachia kwamba yaendelee tu, yanavuruga uchumi wa nchi, hakuna hatua zinazochukuliwa. (*Makofi*).

Mhe. Spika, ninakushukuru. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Salmin. Ulivyosema nikuachieni nikasema sasa kura ya kutokuwa na imani na mimi hiyo inakuja. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa na kama muda utakuwepo Mhe. Mohamed Haji Khalid. (*Kicheko*).

Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa mchana huu kunipa fursa na mimi ya kuweza kuchangia mawili matatu kabla ya kuungana na wenzangu kwenda kwenye sherehe ya kumsherehekea Mwakilishi wa Jimbo la Kiembesamaki, ambaye leo hii ameapishwa hapa kuwa ni Mwakilishi halali halali wa jimbo hilo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe binafsi lakini pia nichukue fursa hii vile vile kumshukuru sana mwenyekiti makini wa Kamati ya *PAC* kutokana na ripoti yake ambayo ametuwasilishia hapa. Lakini vile vile nipongeze majibu pamoja na maelekezo ya hoja ambazo zimekuwa zimejibiwa hapa na Mhe. Waziri au Kaimu Waziri wa Wizara ya Fedha ambapo asubuhi ya leo alikuja kujibu maelekezo ya kamati zilizopita.

Mhe. Spika, nilikuwa nikimsikiliza sana mwenyekiti alipokuwa akitoa hotuba yake hapa. Na kimsingi kabisa hotuba yake imetoa picha halisi ya ripoti ambayo walikwenda kuifanyia kazi katika kipindi chetu hichi cha mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, katika maelezo ambayo mwenyekiti amekuja kuyazungumza hapa, kwanza kabisa mwenyekiti alianza na ukiukwaji wa sheria za matumizi ya fedha za serikali. Kusema kweli Mhe. Spika, tungeliiomba na kuitaka serikali, watakapokuja hapa kuja kutusaidia kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo, watueleze basi ni namna gani hii kadhia ilijitokeza na pesa zaidi ya shilingi milioni mbili kutumika kinyume na utaratibu.

Tukiondoka hapo Mhe. Spika, tunakwenda katika ukurasa wa 38 wa kitabu chetu hiki ambapo kuna fedha ambazo hazikukusanywa inavyotakiwa. Kuna mapungufu hapa ya fedha katika vituo vidogo vidogo hivi ambapo vimeanzia upande wa Pemba huko. Hebu tunaomba maelekezo katika hili.

Nikiondoka hapo naomba vile vile kupata maelekezo juu ya malipo ya kodi ya ardhi yaliyolipwa pungufu, dola za Kimarekani 98,209.50 sawa na pesa za Kitanzania shilingi 152,224,725/- . Mhe. Spika, hili ni tatizo, ni tatizo kwa sababu tuna mambo mengi ambayo yalikuwa yanaendelea kukwama kwama kutokana na kukosa fedha.

Makusanyo yetu baadhi ya maeneo hayafikii malengo. Na ripoti zilizoanza kusomwa hapa Mhe. Spika, za kamati mbali mbali, zilikuwa zinaelezea jinsi gani ambavyo wizara za serikali zilivyokosa *OC* zake kutokana na kwamba hakukuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kuweza kukamilisha mambo hayo. Wakati kuna fedha nyingi huku tu ambazo hazijakusanywa kwa mujibu wa taratibu.

Tukiondoka hapo ninakuja katika ukurasa wa 89 mpaka 90 hapo, 'wafanyabiashara kulipwa mara mbili. Mhe. Mwenyekiti alipokuwa akitoa maelekezo ya hotuba yake hapa, alisema kumekuwa na taratibu za kijanja ambazo zinafanywa na wafanyabiashara wanalipwa mara mbili mbili. Huku katika wizara wanalipwa, lakini na katika maeneo ya matokeo vile vile wanakuwa wanakwenda kudai malipo na wanakuwa wanalipwa tena kwa kazi au kwa jambo ambalo limefanywa kwa mara moja. Hili nalo ningeomba ufafanuzi wake.

Halafu jengine ningependa kupata ufafanuzi na maelekezo zaidi ni kwa nini wale watu wanaokuwa ni wadaiwa sugu, wanapoona kwamba tayari kuna matatizo au kuna kamati zinazokwenda kufuatilia masuala katika mawizara yao, au wale wasimamizi wanakwenda kufuatiliwa masuala ya madeni, wao

kesi huzichukua na kuzipeleka Mahakamani, ili kamati zishindwe kwenda kufuatilia na kuweza kujua uhalali wa kadhia ambayo ipo mbele yetu.

Mhe. Spika, katika hili ningelipenda kupata ufafanuzi kutoka kwako vile vile, ni utaratibu gani unaoweza kuchukuliwa na kamati zako kwa watu ambao wanaotumia janja za namna kama hii.

Baada ya hapo nielekee katika maeneo ambayo katika Mkoa wa kwetu Kaskazini huku, ninaambiwa kwamba kuna fedha za wazee hawakuzipata kwa mujibu wa taratibu. Ningependa vile vile nifahamishwe ni sababu zipi zilizosababisha wazee hawa wanyonge, wastaafu, wanamapinduzi asilia ambao wamefanya kazi ya kukomboa nchi hii, sasa leo inafikia hadi pesa zao zinakuwa zinaliwa na hawazipati katika utaratibu ambao ulikuwa umepangwa. Hali ya kwamba serikali imekwishakuzitenga fedha zile kwa ajili ya kuwasaidia wazee. Ningependa kupata ufafanuzi vile vile.

Mhe. Spika, jengine ni katika ukurasa wa 145 mpaka 156 juu ya hoja ya kuondosha *lease* bila ya kufuata taratibu. Mhe. Spika, Baraza lako hili katika mwaka uliomalizika tulitengeneza utaratibu hapa wa kuweza kumpa meno zaidi Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha, ili ahakikishe kwamba hizi *lease* zinalipwa kwa taratibu zinazopaswa na wizara inayohusika kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha. Wanachunga pamoja na kutengeneza utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba fedha zinadhibitiwa na zinakuwa katika mikono salama na zinakuja kwa mujibu wa taratibu tulizoekeana.

Jengine Mhe. Spika, ni migogoro ambayo Mhe. Mwenyekiti hapa amekuwa ameizungumza baina ya wizara inayoshulikia na hawa wawekezaji wenyewe. Mhe. Spika, si jambo la busara wizara kuingia katika migogoro na watu ambao wanakuwa wanawapa huduma. Ningeliiomba serikali kupitia Baraza lako hili tukufu watengeneze utaratibu ulio makini, na unaofaa, ili kuhakikisha kwamba wizara na wawekezaji hawana mtafaruku wa namna yoyote. Na hili ninapenda kuelekeza kwamba kubwa hapa la kufanyika, kama hatuna sera basi tuzitayarishe na kama tunazo basi tuzisimamie kwa lengo la kuwalinda hawa *investors* ambao wanaoingia katika nchi yetu.

Jengine nilikuwa ninapenda kuzungumzia suala la chumba kile kilichopo chini ya bahari kule Pemba. Mimi ningelipenda nifahamishwe Mhe. Spika, taratibu zetu zilivyo katika masuala ya ardhi, ninavyofahamu mimi ni kwamba kuna utaratibu wa mita 30 kabla ya bahari, maeneo yale yanakuwa ni *free zone*, hayatumiki kwa ajili ya hawa *investors* kuweza kuyahodhi yakawa ni maeneo yao.

Lakini hapa nimekuta kwamba kuna kadhia ya kwamba chumba kilichokuwa kimejengwa baharini kinadaiwa kodi na kinadaiwa kulipia gharama za lile eneo ambalo walikuwa wametumia. Ningelipenda kupata uelewa zaidi katika hili ili na mimi niweze kukubaliana na hoja ambayo mwenyekiti na kamati yake walikuwa wamei-*raise* katika maelekezo yao.

Jengine Mhe. Spika, ni mapitio ya kodi za ardhi kwa sheria ya miaka 3. Mhe. Spika, hapa ningelipenda vile vile kuona kwamba hizi sheria tulizonazo katika masuala ya ardhi na kwa mujibu wa kesi zilivyo nyingi na migogoro pamoja na mambo mengi yanayohusu mambo ya ardhi, turejee kama ambavyo mwenyekiti alikuwa amependekeza. Tuzifanyie mapitio hizi sheria zetu, ili tuweze kuona namna gani tunaweza kukabiliana na changamoto ambazo zinatukabili mbele yetu.

Mhe. Spika, nikimaliza hapo ningelipenda sasa nije katika hii Mamlaka ya *ZIPA*. Mhe.Spika, migogoro mingi ambayo imekuwa-*raised* katika Baraza lako hili tukufu inatokana na wawekezaji. Wawe ambao wanaoendelea na shughuli zao, wawe ambao wanatakiwa kuja au wale ambao wameagiza, ili waweze kutumia maeneo haya.

Mimi ninashangaa, hebu Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie. Ni sababu zipi za msingi zinazopelekea ikawa katika hii sehemu ya *investors*, ikawa matatizo mengi ya ardhi pamoja na migogoro inatokea kule kwao. Wakati wale wanafuata taratibu ambazo sisi tunawapangia na sheria ambazo wao wamekuja kuzikuta kwetu. Ni jambo lipi la msingi linalosababisha matatizo kama haya, kila siku kuwa yanaongezeka siku hadi siku. Mhe. Waziri utakapokuja hapa nitaomba utusaidie vile vile.

Jengine ambalo humu halikuwemo lakini jana lilikuwepo na kwa vile muda ulikuwa hautoshi kwa siku ya jana, tukafanya majumuisho ya jumla jumla tu. Ningependa vile vile kupata maelekezo pamoja na mambo tuliyokuwa tumeambiwa jana kwamba deni la serikali katika Shirika la Umeme lipo milioni arobaini na tatu. Ningependa kupewa taarifa vile vile juu ya zile pesa za *payee*, bilioni kumi na nane zipo katika fungu gani.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima ninaunga mkono ripoti hii na ninaiomba sana serikali kuyachukua mambo ambayo yamo humu kwenda kuyafanyia kazi kwa lengo la kuendeleza ufanisi katika nchi yetu kwa ujumla wetu.

Baada ya hayo Mhe. Spika, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe naona muda uliobaki hautotosha kumpa Mhe. Mohamed Haji Khalid ili naye achangie. Kwa hivyo nimuombe basi yeye achangie jioni pamoja na wengine ambao wanaweza wakahitaji kufanya hivyo.

Niwashukuru kwa mashirikiano makubwa na sasa ninaahirisha kikao hiki hadi saa kumi na moja jioni leo.

(Saa 6.55 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi jioni hii kuwa ni kiranja katika kuchangia majadiliano yaliyo mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa kuendeleza kazi zetu za kawaida na mimi kuweza kupata nafasi hii ya kwanza.

Mhe. Naibu Spika, kijitabu hiki tulichonacho cha *PAC* kina kadhia tupu za serikali, kila sentensi iliopo inaonesha kutofanikiwa kwa taasisi mbali mbali zilizokaguliwa na *PAC* katika kipindi kilichopita.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ilifanya Mapinduzi yake mwaka 1964, kwa lengo la kuwakomboa Wazanzibari katika kutawaliwa. Chama cha *Afro*-Shiraz kilichokuwa na mwenyekiti wake marehemu Mzee Abeid Aman Karume na Katibu Mkuu wake wa mwanzo ni Sheikh Thabit Kombo Jecha, hawa ndio waasisi wa *Afro*-Shiraz. Sheikh Thabit kabla ya kuwa *Afro*-Shiraz alikuwa na taasisi yake ikiitwa *Shiraz Association* na Sheikh Karume alikuwa na *African Association*, hii ina maana Sheikh Thabit Kombo alikuwa ni Mshiraz.

Hatimaye *Shiraz Association* na *African Association* wakaungana wakapata chama kinachoitwa *Afro-Shiraz Part*. Chama hiki katika maendeleo yake walianza kuchanga pesa kidogo kidogo ili kutafuta afisi yao kuu ambayo ndio ile pale Kisiwandui. Katika kila mkutano wa hadhara ilikuwa wanapita na kikapu mwenye pesa nne au pesa mbili wanatia. Nikisema lugha hiyo, kuna watu pesa nne wala pesa mbili hawazijui, lakini wako wanaozijua pesa nne na pesa mbili.

Kwa hivyo, afisi ile ilianzwa kujengwa kwa mchango wa aina hiyo. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hata mimi nimo. Sasa lengo la Mapinduzi ni kuwakomboa Waafrika, kwa nini ardhi ilikuwa ni yao lakini ilikuwa

imetawaliwa na wachache, wachacha waliokuwa ni watendaji wa serikali walikuwa wanalipwa malipo duni hayakidhi mahitajio yao na mengine kadhaa yaliyokuwepo.

Mhe. Naibu Spika, sasa tuje katika ardhi ambayo ilikuwa ikimilikiwa na wachache. Baada ya Mapinduzi ardhi iligaiwa kwa Wazanzibari wenyewe, waliobahatika heka tatu tatu. Lakini malengo hayo Mhe. Naibu Spika, pole pole yanaanza kupotea, kwa sababu ardhi baada ya kuwanyang'anya wale waliotutawala, sasa sisi kwa hiyari yetu tunahaulisha kwa watu wengine wageni, tena kwa kima kikubwa, watu ama kwa kutojua wanapokea fedha chache. Kama Wapalestina walivyofanyiwa na Waesrael walikuwa wananunua kidogo kidogo hatimaye ardhi yote ikachukuliwa na Wayahudi, na sisi pole pole tunatoa *lease*. Mashamba au viwanja vilivyotajwa ni vingi sana, ardhi hii ambayo iwe ni ya Mzalendo leo tunaihaulisha kwa wageni.

Ingelikuwa Mhe. Naibu Spika, mtu akifa anafufuka, basi Mzee Karume mwenyewe hili asingelikubali, tunalifanya sisi tu. Halafu wafanyakazi wachache waliokuwepo wakati huo walikuwa wanalipwa malipo duni ambayo yalikuwa hayakidhi mahitajio yao. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, mfanyakazi anavyotakiwa kazi anayoifanya basi imlishe, imvishe, kama ana watoto basi awasomeshe watoto wake na apate tiba hospitali, kwa wakati ule ilikuwa hawamiliki hivyo. Je, leo wafanyakazi wetu wa kawaida tunavyowalipa wana miliki kufanya yote hayo.

Kama wana miliki sawa na kama hawamiliki bado tunapiga mguu, kwa sababu kupiga mguu sio kwenda mbele, ni kunyanyua tu mguu kushoto kulia, kushoto kulia uko pale pale hujenda popote. Wakati ule ilikuwa mfanyakazi hamiliki na mpaka leo mfanyakazi wa kawaida unachomlipa hamiliki kujikimu mahitaji yake ya lazima. Hata tukisema tuna nyumba nzuri, barabara na kadhalika, lakini *so far* mtu *individual* wa chini kabisa, mahitajio yake hayakamiliki, bado tunapiga mguu pale pale kushoto kulia, kushoto kulia tuko pale pale.

Kwa hivyo, bado katika baadhi ya sehemu Mapinduzi tunayarudisha nyuma, tunayapeleka mbele baadhi ya sehemu na sehemu nyengine tunayavuta nyuma. Hili Mhe. Naibu Spika, sio jambo zuri. Nani waliofanya hivyo ni serikali, kwa sababu sisi tulikuwa nyuma huku tunasema sana, lakini wao wanasema hewallah, halafu baada ya hewallah wanatia pamba za masikio. Hatua wanazochukua zile za marekebisho yale tunayoyasema ni machache sana. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, hii sio hali nzuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze na Kikosi cha Volantia. Mhe. Naibu Spika, kikosi hiki ni vema kikabadilishwa jina, kwa sababu neno Volantia ni neno la

Kiingereza ambalo tumelitohoa tu. Volantia ni kazi ya kujitolea, huko nyuma palipokuwa na *Afro*-Shiraz walikuwa hawa ni Volantia wa kweli, walikuwa wana rungu yao na wanafanyakazi kwa imani tupu ya kujitolea, lakini leo tumewatia katika mpango wa serikali wana bajeti ya serikali na tunawapa mishahara ya watumishi wa serikali, huo Uvolantia uko wapi.

Huo Uvolantia nahisi umepotea.Kwa hivyo, kwa kuwa umepotea sisemi kikosi kiondolewe hapana, lakini kikosi kibadilishwe jina. Kwa hivyo, hivi sasa sio Volantia tena ni wafanyakazi kama walivyo JKU, Zimamoto, walimu na wafanyakazi wengine, kwa sababu hawa sio Volantia tena, kwa sababu hawa hawajitolei tena tunawalipa. Ningeiomba serikali itafute jina jengine badala ya hili.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 7 kwenye hii hoja 20.3. Hoja hii inaelezea madai yanayodaiwa kikosi hiki kwa wafanyabiashara wanaotoa huduma mbali mbali. Ningependa kujua ni huduma gani hizo ambazo wafanyabiashara wanatoa katika kikosi hiki, hatimaye ikafika kuwa na deni kiasi hicho na hii ni kwa hao Volantia na Zimamoto. Kama ni madeni ya kupelekewa huduma za vyakula kama mboga mboga, kama ni huduma hizo nasikitika kuwa vikosi hivi kazi hizi ingekuwa wafanye wenyewe, wasipelekewe mapapai na mboga mboga, kama ni huduma hizi za vyakula, kwa sababu hapa haikuainishwa ni huduma wa aina gani wanazodaiwa na wafanyabiashara.

Kwa hivyo, ningeomba nijulishwe ni huduma gani hii ambayo inatolewa na wafanyabiashara hao hadi kufikia deni hilo ambalo linasemekana ni la muda mrefu na bado halijalipwa. Mhe. Naibu Spika, hilo ni moja.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni hoja ya 21.1.2 iliopo katika ukurasa wa 10. Suala hili kaligusia Mhe. Salma Mohammed na miminitaligusia kidogo. Kuhusu shilingi milioni 50 zilizolipwa kwa mtu ambaye alidai kuwa palikuwa na walinzi wa JKU na hatimaye akaibiwa na uongozi ukahisi kuwa umlipe huyu.

Mhe. Naibu Spika, hili linanitia wasi wasi, kwa sababu na mtu mwengine akiona kuwa JKU iko doro kiasi hicho, basi na yeye anaweza kuomba ulinzi wa JKU, halafu akafanya anavyojua mwenyewe kisha akenda kudai kuwa anataka kulipwa. Mhe. Naibu Spika, hata kama iwe JKU walikuwa ni walinzi na bahati mbaya wameshiriki katika kufanya uhalifu, malipo yake taasisi itowe pesa kumlipia mhalifu, iwe hawakushiriki lakini umetokea uhalifu ikiwa wao wapo ili kuwalinda wao ni kuwa taasisi itumie pesa kwa ajili ya kumlinda mtu aliyekuwa mlinzi. Mimi nahisi suala hili Mhe. Naibu Spika, kwa muono wangu mimi haikuwa sahihi sana.

Mhe. Naibu Spika, nielekee kwenye ukurasa wa 82 kwenye soko la mboga mboga Mombasa. Mhe. Naibu Spika, soko hili lilijengwa kwa ajili ya kuwapatia wananchi mahitaji yao muhimu, limekuwa halitumiki kwa muda mrefu na limekuwa lina matatizo yafuatayo. Matatizo ni manne lakini ni mengi sana.

Kwanza mazingira yasiyoridhisha, hali inayofanya wafanyabiashara wengi kushindwa kutumia eneo la ndani la soko na kupelekea kujenga vibanda pembezoni mwa soko hilo bila ya ridhaa ya Baraza la Manispaa. Sasa kwa nini wawache soko ndani halafu watoke nje. Mhe. Naibu Spika, kiuzoefu mtu akipata matatizo nje basi anakimbilia ndani, leo ndani kuna matatizo unakimbilia nje na huko nje kukoje. Ni hatari mtu kutishwa ndani utakimbilia wapi, lakini ukitishwa nje unakimbilia ndani.

Mhe. Naibu Spika, hawa wafanyabiashara wameliacha soko ndani kutokana na ripoti hii wamekimbilia nje. Tuchunguze huko ndani kuna nini, kubovu, kubaya, malipo makubwa na hatimaye mpaka wakajenga vibanda vidogo vidogo nje ya soko na bila ya ridhaa ya manispaa. Hivi ni kweli Mhe. Naibu Spika, manispaa ni korofi kiasi hicho, maana manispaa imechachamaa wanafanya watakavyo, wakiamua kumchukulia mtu mali yake wanachukua, wakiamua leo wampige wanampiga, wakiamua leo wamfukuze sehemu wanamfukuza. Ndio pale wanapojenga vibada bila ya ridhaa yao. Sijui hata kidogo, hilo ni tatizo moja. Limejengwa soko ndani ili litumike, lakini watu wanakuja nje je, kuna nini?

Jengine Mhe. Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu suala la uungaji umeme kinyume na taratibu, hili ni tatizo. Ni nani anayewaungia umeme na kwa nini iwe ni kinyume na taratibu wakati ni soko la serikali. Je, huu umeme unaoungwa bila taratibu shirika linajua, na kama linajua linachukua hatua gani. Kwa sababu shirika lenyewe Mhe. Naibu Spika, lina madeni, sasa ikiwa unaunga bila ya utaratibu, basi inawezekana ikawa vibanda hivyo au soko hili halilipi matumizi ya umeme. Kwa hivyo, wanaliongezea shirika mzigo wa lazima. Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo kubwa tena ni lazima hatua za kurekebisha zichukuliwe.

Mhe. Naibu Spika, kumezungumzwa hapa vile vile kuhusu ukusanyaji wa mapato na halafu uchafuzi wa mazingira. Mhe. Naibu Spika, tumebahatika Wazanzibari tumekuwa *immuned* na magonjwa mbali mbali. Kuna mambo sisi hayatuathiri tena, vyenginevyo kwa vyakula tunavyokula basi ingekuwa siku zote tunadayaria, lakini *Alhamdulillah* miili yetu imekuwa *immuned*, kuna magonjwa mengine yakiingia katika miili ya Wazanzibari kwa hiyari yake yanaghairi yanaondoka, huwa ni dawa kweli kweli.

Lakini kwa mazingira machafu ya masoko yetu na vitu tunavyonunua sokoni pale, wengine tunakula vyakula pengine pale pale nje na bukheri hamsa ishirini hatuna athari yoyote tunayoipata. Matumizi yale kama angetumia mgeni Mhe. Naibu Spika, basi angelazwa, kwa sababu mazingira machafu ya masoko yetu na ni uchafu uliokithiri. Sijui kwa nini ikawa tunashindwa kulinda mazingira yetu yaliyotuzunguka. Ukisema serikali, itakuambia hapana, kazi hii sio ya manispaa peke yao, hapana ni yao peke yao. Si kuna watu tumewaajiri kwa kazi hiyo, sasa sio peke yao vipi.

Mhe. Naibu Spika, je daktari anaposhindwa kufanya kazi fulani ya kidaktari aseme sio kazi yake peke yake, kutibu ni kazi yake peke yake, kuelimisha ni kazi ya sote, lakini kutibu ni kazi yake peke yake. Kwa hivyo, kila taasisi imepewa dhamana fulani kutekeleza kazi ile ni kazi yake iliyokabidhiwa.

Mhe. Naibu Spika, serikali kama utakaa nje ya Zanzibar ukasikia taarifa za serikali zinavyotolewa, basi mtu anaweza kuhisi hakuna pahala pazuri na serikali nzuri kama ya Zanzibar. Lakini ukija ndani ukaona tunavyoishi, ukaona watu wanavyoendeshwa, kumbe baadhi ya wakati maneno yetu hayalingani na vitendo vyetu. Mhe. Naibu Spika, serikali ni lazima ijirekebishe, Tumeshaboronga sana na baada ya kuboronga tunajipongeza, lakini mwananchi kukosa huruma muhimu anayohitaji, halafu tukajipongeza kuwa tumefanya vyema. Hapa huwa tunasema jambo ambalo halina ukweli ndan yake.

Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Naibu Spika, serikali ijirekebishe ili wananchi walio wengi wajenge imani na serikali yao, kwa sababu serikali hii ipo kwa ajili ya watu na imewekwa na watu.Kwa hivyo, hawa walioiweka tuwaenzi, tuwatunze na tuwaheshimu na yale ambayo wanastahili wapate serikalini basi wapate na yale ambayo wao waisaidie serikali basi tuwatake na wao wafanye ili kuisaidia serikali.

Mhe. Naibu Spika, ripoti hii kama walivyosema wasemaji waliotangulia ni nzuri na inahitaji sisi tuichukuwe, tuipitie na pengine itatusaidia wakati wa kujadili tukijaaliwa bajeti ya serikali ya mwaka unaokuja wa fedha. Serikali au Baraza linatumia pesa nyingi kuunda kamati mbali mbali kwa ajili ya kuisaidia serikali, lakini serikali haijui kuwa abebwaye hujikaza. Wao tukiwabeba sisi basi wao wanalegea ili tuanguke sisi. Kwa hivyo, tunaiomba serikali yale mapendekezo ambayo yana nia ya kuisaidia serikali, basi wayachukuwe na wayafanyie kazi, vinginevyo Mhe. Naibu Spika, itakuwa kila siku tunasimama na tukisema hili na lile, lakini matokeo yake hatuna tunalotekeleza.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache niseme naiunga mkono ripoti hii ya *PAC* kwa asilimia kubwa sana, sisemi kwa asilimia 100, kwa sababu kwa asilimia 100 ina maana hakuna kosa lolote, hakuna mwanadamu aliyekuwa hana kosa lolote. Kwa hivyo, naiunga mkono kwa asilimia kubwa sana. Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Molla mtukufu kwa kutujaalia kuwa hai na wazima na kuendelea na shughuli mbali mbali zinazohusu chombo hiki kitukufu cha Baraza la Wawakilishi ambalo ni ngome ya wananchi.

Pili nikushukuru na wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia pamoja na kuwa nimeleta taarifa punde tu, nashukuru na ninathamini sana nafasi uliyonipa. Mhe. Naibu Spika, nitakuwa sitendi haki kama nitakuwa sikuipongeza Kamatiya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika *PAC*, kwa kazi kubwa na nzito ambayo wameifanya. Nadhani tofauti na kamati nyengine, kamati hii inakuwa na kazi ya ziada kwa sababu ni kazi inayoshughulika na nambari kwa maana ya hesabu na sio kazi nyepesi.

Mhe. Naibu Spika, moja ambalo nataka niliseme kabisa kabla ya kuingia katika undani wa ripoti, mimi naunga mkono sana hoja ambayo mara nyingi imejitokeza kwamba Kamati ya *PAC* ni tofauti na kamati zetu nyengine zote. Kwa hivyo, kuna haja ya kuongezewa muda wa kufanya shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia sisi wengine tuna wizara labda mbili au tatu, lakini *PAC* inapokabidhiwa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, huwa mara nyingi imekusanya wizara zote, mashirika yote, idara zote na zote hizo zinapaswa kupitiwa kwa undani kabisa. Kwa sababu wao ndio jicho la Baraza hili katika kuingia kwa ndani ya hesabu zile, sisi wengine hatupati fursa kama zile. Sisi wengine huwa tunapata nafasi ya kuchangia baada ya kuwasilishwa ripoti. Kwa hivyo, niungane kabisa mkono na hoja ya kwamba wanahitaji kufikiriwa katika taratibu za kanuni zetu kuongezewa muda.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu ya uchache wa muda naomba uniruhusu niende moja kwa moja katika hoja ambazo nimetaka kuzizungumzia. Mhe. Naibu Spika, kwa jumla ripoti hii imegawika sehemu mbili. Kuna ripoti ambayo inazungumzia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi kuhusiana na ukaguzi wa hesabu kwa mawizara, mashirika na taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na ya pili inahusu ripoti ya ukaguzi yakinifu kwa miradi ya taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2011/2012, pamoja na ripoti ya ukodishwaji wa ardhi kwa wawekezaji.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze na hii ya kwanza inayohusu Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali. Jambo moja ambalo linasikitisha Mhe. Naibu Spika, ni kwamba ukiangalia sehemu ya kwanza takriban mikoa yote ambayo imetembelewa na halmashauri zote za wilaya pamoja na Baraza la Manispaa kwa Mji wa Zanzibar, basi hazikuwa zimewasilisha hesabu zake kwa ajili ya ukaguzi. Suala hili Mhe. Naibu Spika, linasikitisha sana kwa sababu kila mwaka Baraza hili likipokea ripoti linasisitiza juu ya haja ya serikali kujipanga ili taasisi zake ziwe mfano kwa wengine katika kuwasilisha mahesabu zake.

Sasa suala hili kuwa linaripotiwa kila mwaka Mhe. Naibu Spika, sio picha nzuri na ukilinganisha na kiwango kikubwa cha fedha ambacho kinaidhinishwa hapa kwenda katika ofisi za mikoa, kwenda katika ofisi za wakuu wa wilaya, kwenda katika halmashauri za wilaya na Baraza la Manispaa kama ni ruzuku ni kiwango kikubwa sana cha fedha.

Mhe. Naibu Spika, katika suala hili nataka nizungumzie hususan Baraza la Manispaa la Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, Baraza la Manispaa liliundiwa kamati teule ya kwenda kuchunguzwa na tulipokuja kutoa ripoti na mimi nilikuwa mjumbe wa kamati ile teule tuliwataka wasawazishe suala hili. Mwaka jana tuliambiwa kwamba tayari utaratibu wa kuwasilisha mahesabu ili kukaguliwa unafanyika, lakini bado tunapokea ripoti kwamba Baraza la Manispaa haliwasilishi hesabu zake, hii sio picha nzuri Mhe. Naibu Spika. Kama ilikuwa inahusu mwaka huu tu wa fedha na baada ya hapo imerekebishwa, nitashukuru sana. Lakini kama bado utaratibu huu uko vile vile Mhe. Naibu Spika, hiyo sio picha nzuri.

Suala la pili, Mhe. Naibu Spika, kila mwaka tunalalamika kwamba kumekuwa na utaratibu mmoja ambao mimi siuwafiki hata kidogo, kwamba mawizara au maidara au ofisi mbali mbali za serikali, zinapofanyiwa ukaguzi na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, basi zinakosa vielelezo vya matumizi. Lakini *PAC* ikifika vielelezo vimepatikana. Sasa mimi huwa najiuliza Mhe. Naibu Spika, ikiwa matumizi yamefanyika kwa wakati, bila shaka unapofanya matumizi unapata na stakabadhi, kwa nini unapofanyika ukaguzi wa Mdhibiti stakabadhi isiwepo, lakini ikifika kamati stakabadhi iwepo.

Mhe. Naibu Spika, tafsiri yangu ni kwamba stakabadhi hizi zitakuwa ni za kughushi, kwamba zinakuwa hazipo katika ukaguzi, halafu kwa sababu zimesharipotiwa ni kama vile wamegutushwa wanakwenda kuzitafuta kwa njia zao, halafu inapokuja kamati inaziona.

Mhe. Naibu Spika, nitowe mfano. Katika ukurasa wa 63 wa ripoti hii ya *PAC* ambao unazungumzia ofisi ya usajili na kadi za utambulisho, hoja nambari 42.2 Mhe. Naibu Spika. Malipo yasiyokuwa na vielelezo, nyaraka pungufu jumla shilingi 219,390,619. Mhe. Naibu Spika, kwa wananchi wanyonge maskini wa Zanzibar ambao wanakwenda hospitali wakakuta hakuna dawa, wanaambiwa kila mwaka wachangie skuli, mabuku ya watoto wao, vitabu vya kiyada, wakute kuna shilingi 219,390,619 hazina vielelezo, huu si utaratibu mzuri wa kutumia fedha za walipa kodi wa nchi hii Mhe. Naibu Spika.

Sasa imesemwa hapa majibu ya Ofisi,Ofisi imekiri kutokea kwa kasoro hiyo katika ukaguzi ingawa wakati wa kamati vilikuwa vimeshapatikana na kuitaka kamati ivikague. Sasa Mhe. Naibu Spika, hili linajitokeza kila mwaka na kwa taasisi tofauti, mimi tafsiri yangu tukiridhika utaratibu huu maana yake tunabariki matumizi mabovu ya fedha za walipa kodi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kama hilo halitoshi ukenda katika Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Nyumba, Mhe. Naibu Spika, hii Idara bahati mbaya sasa niseme imetia fora katika matumizi ambayo hayana vielelezo na mimi nasema ni upotevu wa fedha za walipa kodi na matumizi mabaya. Mhe. Naibu Spika, nisome haraka haraka tu kwa sababu ya muda. Kuna hoja ya kukosekana kwa marejesho ya masurufu jumla ya shilingi 79,750,000 kwa Idara moja tu ya Majenzi na Utunzaji wa Nyumba.

Lakini nikiondoka hapo kuna hoja nyengine katika Idara hiyo hiyo malipo yasiyokuwa na vielelezo ndio kama ile kadi za *ZID* kuna jumla ya shilingi 17,137,000, kama hiyo haitoshi Mhe. Naibu Spika, kuna hoja nyengine malipo yaliyotofautiana na *bank statement*, jumla ya shilingi 163,580,000 Idara hiyo hiyo moja ya Ujenzi na Utunzaji wa Nyumba.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ni hati zilizokosekana kwa ukaguzi katika Idara hiyo hiyo ya Ujenzi na Utunzaji wa Nyumba shilingi 340,450,600. Mhe. Naibu Spika, haijamalizia hapo kuna hoja nyengine kuhusiana na matumizi ya fedha yaliyokosa maeleze, jumla ya shilingi 65 milioni 168,212 na senti 41. Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ya Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa nyumba ni malipo yanayofanyika kinyume na taratibu kwa kukosa hati za malipo shilingi 33,182,100.

Halafu kuna hili moja nataka nilitolee maelezo hasa Mhe. Naibu Spika, hoja iliyokuwepo katika ukurasa wa 72 kuvunjwa kwa hundi ya shilingi 127,128,848.Hapa kamati inatwambia kwamba hii ilikuwa ni hundi ilipaswa ikawekwe katika akaunti, lalini ikavunjwa *cash* na baadhi ya matokeo yake Kamati na Mkaguzi wameshindwa kuthibitisha matumizi ya fedha hizi 127,128,848 Mhe. Naibu Spika. Wakati taratibu za kiserikali zinataka mambo

haya ya fedha yende kwa njia za kibenki kwa nini fedha hii ivunjwe iwe *cash*. Halafu hoja yenyewe maelezo ukisoma inasema kwamba ulikuwa na *file* limepotea. Mheshimiwa katika taratibu za serikali *file* linapoteaji, mimi ikisema kama halikupotea limepotezwa nitakuwa ninakosea Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kuna mafedha yote hayo, hii ni Idara moja tu. Idara hiyo hiyo Mhe. Naibu Spika, kuna hoja nyengine malipo yanayofanyika bila kuidhinishwa na Mkurugenzi jumla ya shilingi 3,400,000.

Na mwisho, Idara hiyo hiyo Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna malipo yaliyofanywa kinyume na Kanuni na taratibu za manunuzi jumla ya shilingi 25,000,000, tukifanya hesabu sijui kama hazitafika bilioni moja hizi Idara moja tu ya Ujenzi na Utunzaji wa Nyumba ambapo bila shaka pengine walipata nafasi kupitia, kwa kina Kamati ya *PAC*. Sasa Mhe. Naibu Spika, wananchi wanyonge wa nchi hii tunaojidai kukaa katika majukwaa tukasema tunawatetea na tunawatumikia wao, huduma za msingi hawazipati huku mamilioni yao yanatafunwa na watu bila ya kufuata taratibu, huu Mhe. Naibu Spika, si utaratibu mzuri wa matumizi wa fedha za walipa kodi, maskini wanyonge wananchi hii.

Lakini Mhe. Naibu Spika, jengine hili la masurufu, unapochukua *imprest*, utaratibu urejeshe mahesabu. Yametajwa humu Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuna jumla ya shilingi 15,450,000 na Idara yake ya Majenzi imetaja hapa 79,750,000. Mhe. Naibu Spika, hii ndio iliyokaguliwa nina hakika hali hii tukenda tutaikuta katika kila wizara katika kila Idara.

Sasa tuambiwe na serikali mpaka lini Baraza hili liendelee kuidhinisha fedha halafu ziwe zinatafunwa namna kama hii Mhe. Naibu Spika. Kwa sababu mimi unaponambia kwamba hakuna marejesho, maana yake huna maelezo ya kuridhisha matumizi ya fedha hizo, kama unayo ukimaliza kutumia kawaida vielelezo, maana yake Mhe. Naibu Spika, hutumii fedha leo ukaambiwa njoo uchukuwe risiti baada ya mwaka, hakuna utaratibu huo duniani. Sasa kwa nini risiti au stakabadhi ikosekani katika ma-*files* ya matumizi ya fedha hii, bila shaka fedha hizi hazitumiki zinavyopasa.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nimesikitishwa zaidi na maelezo ambayo yapo katika ukurasa wa 40, watendaji wetu Mhe. Naibu Spika, hawawaachi hata wazee wanyonge maskini kuzitafuna fedha zao. Naomba nisome kwa umuhimu wake Mhe. Naibu Spika. Ukurasa wa 40 wa ripoti unasema, taarifa za ukaguzi maalum malipo ya msaada kwa wazee wasiojiweza. Naomba nisome;

> "ukaguzi umebaini kuwa fedha za misaada ya wazee wasiojiweza kwa kipindi cha miaka 3 kilichoanzia Juni 2008 hadi *March* 2012,

ulifanyika kupitia mikoa yote 5 ya Zanzibar ambapo mapungufu mbali mbali yaligundulika" Baadhi ya mapungufu hayo ni kama yafuatayo:

Kuendelea kulipwa wazee ambao wameshafariki dunia, kulipwa watu wasiostahiki kupata msaada, kulipwa kwa wazee ambao majina yao hayamo katika orodha ya malipo, kutokufuata sheria za fedha wakati wa ulipaji na upokeaji wa fedha. Mhe. Naibu Spika, hii inatisha, tumetoka katika mishahara hewa, tumeripotiwa kuwepo kwa viinua mgongo hewa sasa mpaka malipo ya wazee wanyonge wasiojiweza nao kuna malipo hewa ndio maana ya maelezo haya yaliyokuwepo hapa Mhe. Naibu Spika.

Hawa ndio tunokaa tukadai kuwa tunawatetea na kuwatumikia Mhe. Naibu Spika, lakini pesa zinatumika kwa migongo yao, kwa majina yao kumbe zinaliwa na wajanja wachache. Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa namna hii hauvumiliki hata kidogo.

Tunaomba serikali ikija hapa ije itutosheleze kwa kina, kwa nini kila mwaka tuendelee kuidhinisha matumizi ambayo vielelezo vyake havipatikani, masrufu hayarejeshwi, risiti hazipatikani mpaka kamati inapokwenda, kwa nini Baraza hili liendelee kuidhinisha fedha nyingi. Na hii niwageukie Wawakilishi wenzangu Mhe. Naibu Spika, mimi hili nasema wa kujilaumu ni sisi hapa, tusijidai kama tunawatetea wanyonge, sisi Wawakilishi Mhe. Naibu Spika. Kwa sababu tunaposimama baadhi yetu badala ya kuchukua hatua tunarudi nyuma, wengine humu ndani.

Sasa wewe unakauka kifua, unatetea hoja, halafu mwisho unapitisha fedha nyengine zikatume, utawambiaje wananchi wanyonge wa nchi hii kwamba wewe unawaonea huruma? Tunasema huduma zitakwama, lakini kwa maelezo haya Mheshimiwa fedha hizi haziendi kutumikia wananchi, si huduma zao, zinaingia mifukoni mwa watu, hili liwe fundisho Mhe. Naibu Spika, na tutapima maelezo haya wakati wa bajeti ukifika hapa, kwamba je, tunaidhinisha tena kwa Mikoa na Halmashauri wakatafune fedha halafu waturejeshee mahesabu. Je, tunaruhusu fedha za ma-*imprest* zikatumika bila ya kurejesha mahesabu tena tutakuja kulizana hapa Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya muda naomba kwa uchache nigusie eneo moja kwa sababu niliizungumza katika bejeti ya mwaka jana Mhe. Naibu Spika, suala la miradi ya maendeleo inavyotumika kunufaisha watu binafsi. Na niliitaja hasa mradi wa *MACEMP* humu ndani Mhe. Naibu Spika. Nikasema kuna haja ya kuutizama nikatoa hoja katika bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi humu ndani Mhe. Naibu Spika, kwamba inafikaje Idara ina *account* yake mbali ambayo Wizara haifikii.

Leo Mhe. Naibu Spika, kwa uchache tuangalie ukursa wa 86 na 87 wa ripoti hiyo ya *PAC*. Mhe. Naibu Spika, katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuna hoja nambari 11 mradi wa Ofisi ya Uvuvi Pemba, sina muda wa kuisoma yote, lakini pamepewa fedha za kigeni dola za kimarekani 1,614,504 kujenga Ofisi ya Uvuvi Pemba na kamati imethibitisha kwamba imejengwa chini ya kiwango na mpaka leo matumizi yake ni ya kubahatisha.

Lakini isitoshe Mhe. Naibu Spika, ukurasa namba 87 kuna hoja namba 11.3 mradi wa ujenzi wa sehemu ya kuuzia samaki Tumbe Pemba jumla ya shiligi 263,824,666.87 na wao wenyewe wakithibitisha kwamba fedha zimelipwa, lakini soko halijakamilishwa mpaka leo na hilo lilojengwa sehemu ndogo kamati inatwambia liko chini ya kiwango. Mhe. Naibu Spika, tukisema kwamba fedha za wahisani tunazitumia, waliopewa dhamana hizi tunakuwa tunasema kwa maelezo yake Mhe.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nadhani hii iwe ni kengele ya kuiamsha serikali tunaposema mambo humu ndani huwa tuna ushahidi hatusukumi tu Mhe. Naibu Spika, ushahidi huu hapa. Hizi ni hoja mbili za *MACEMP*, lakini mimi nina hakika miradi mingi tuliyokwenda kuitizama ilivyozungumzwa hapa mambo kama haya tunayakuta.

La mwisho, Mhe. Naibu Spika, naomba kwa uchache sana na hili naomba nilizungumze kwa jumla kwa sababu sitaki kulizungumza moja moja kutokana na kwamba kwanza sitolimaliza suala la ardhi, lakini Mhe. Naibu Spika, hapa kwanza mimi niseme suala moja na niliwahi kulizungumza pia Barazani humu, nawaomba mawaziri wasitumie dhamana zao vibaya hasa mawaziri wenye dhamana masuala ya fedha. Mhe. Naibu Spika, sheria zinapotoa mamlaka ya kusamehe kodi huwa inaelezwa siku zote kwa maslahi ya umma. Mimi nilikuwa na ushahidi wa barua hapa mtu hata ile *land rent* mtu anapewa *exemption* tumeona wapi duniani.

Mhe. Naibu Spika, leo zimetolewa kesi mbali mbali humu ndani, wawekezaji wakija hapa tunategemea watupe manufaa, kuna nchi za wenzetu Mhe. Naibu Spika, kwa mfano nchi za Arabuni, sheria pale ni kwamba ardhi hapewi mgeni akiitaka ardhi inabidi akamtafute raia wa pale, yule raia ndio dhamana wa ardhi ile inakuwa ni sehemu yake ya kuingia katika mradi ili raia anufaike pale. Sisi sheria zetu ninafikiri umefika wakati zitizamwe upya, sisi tunawapa *lease* baada ya kuwapa *lease* hata ile kodi ya ardhi tunawasamehe yamo humu Mhe. Naibu Spika, nasema sitaki kutoa moja moja kwa sababu yapo mengi yametajwa.

Kwa mfano imetajwa humu kesi ya Hoteli ya *the Residence* ambayo ilikuwa ilipie dola 83,000 unamteremshia mpaka dola 37,000 huyu ni tajiri kaja

kuwekeza hapa, anafanya faida, unapompunguzia kutoka dola 83,000 mpaka dola 37,000, wewe waziri umepata tija gani humu ndani? Maana mwananchi wa Zanzibar hakufaidika, kala hasara.

Mhe. Naibu Spika, tuambiwe sisi tunapata faida, mawaziri hasa wenye dhamana ya fedha wasitumie madaraka yao vibaya, wazingatie kwamba wanapoambiwa wasamehe kodi iwe kwa maslahi ya umma na maslahi ya umma, maana yake ni mwananchi mnyonge wa Zanzibar ambaye anategemea mapato yale yamsaidie yeye anapokwenda hospitali apate dawa, anapopeleka mtoto wake skuli apate vitabu, apate madaftari asiambiwe changia hiki, changia kile, anapotaka maji yafike nyumbani kwake, yote hayo anayakosa kwa sababu sisi tunasamehe kodi.

Na la mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, katika suala la ardhi sitaki kutoa mfano mmoja mmoja nimeona kesi humu ndani, kwamba kuna watu fulani wengine ni raia kwa maana ya wazanzibari wamepewa ardhi chini ya msingi kwamba wamekodishwa ni *lease* ili waendeleze kwa mradi fulani, wameshindwa kuendeleza ripoti ya kamati inatwambia kwamba badala yake wamepewa *right of occupancy*, yaani haki ya matumizi ya ardhi.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nikisema kwamba ni njia nyengine ya kujilimbikizia ardhi kwa watu wachache kwa gharama ya wananchi wa nchi hii, nitakuwa ninakosea kwa sababu ardhi kama umeomba kwa ajili ya kujenga kuna utaratibu wake, ardhi kama uliomba upewe *lease* kwa ajili ya kuendeleza kwa mradi kwa utaratibu wake, vipi ardhi ambayo umepewa kwa *lease* kwenye huu mradi halafu igeuzwe upewe *right of occupancy*, upewe haki ya matumizi na Mhe. Ali Mzee Ali, nimshukuru sana mzee wangu katika kikao kilichopita alipotuwasilishia ripoti ya Kamati Teule kuhusu masuala ya ardhi katwambia hapa sheria ziko wazi kwamba mtu anapaswa kila raia ana haki ya ardhi mbili tu moja katika eneo lake analotoka na jengine kwa ajili ya kujenga.

Leo humu kuna watu wamekusanya ardhi wameorodheshwa majina hayo kwa hayo yanajirejea Mhe. Naibu Spika, sheria ndio zile zile, kwa nini ukiwa na dhamana kubwa katika ofisi ya serikali au ya chama fulani uwe na hadhi zaidi na haki zaidi kuliko raia mnyonge wa nchi hii ushindwe kuendeleza halafu ubadilishiwe upewe *right of occupancy*. Kwa nini Mhe. Naibu Spika, halafu sisi tunakaa tunasema tunawaonea huruma wananchi wanyonge si kweli Mhe. Naibu Spika.

Na Mhe. Naibu Spika, mambo haya ndio yaliyopelekea katika baadhi ya nchi wananchi wanapochoka na wanapoona viongozi wao hawapo kwa ajili ya kuwatumikia wao, lakini wapo kwa ajili ya kujinufaisha wao na matumbo yao na familia zao, wanapofika kuchukua sheria mikononi. Mhe. Naibu Spika,

tusiombe Zanzibar ikaja ikafika huko tusiombe. Kizazi cha leo Mhe. Naibu Spika, ni tofauti na vizazi vilivyopita, kizazi cha kuhoji, kizazi cha vijana wa leo hiki tusiwafikishe hapo Mhe. Naibu Spika.

Naomba sana serikali ichukuwe ripoti hii, ifanye kazi na badala ya majibu yaliyozungumzwa jana hapa katika mjadala ya kila siku kwamba tunawafanyia kazi wafanyakazi mpaka Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, yeye mwenyewe alipokuja kufanya *winding up*, akasema kwamba ni kweli ikiwa kila siku tutasema maneno tu, lakini utendaji hauonekani, watafika pahala watu watachoka. Watachoka wawakilishi, watachoka wananchi. Mhe. Naibu Spika, naomba sana serikali katika hili itupe majibu ya kina kama si hivyo tutawapelekea wananchi wakahukumu. Ahsante sana.

Mhe. Waziri Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru na mimi kunipa nafasi ndogo sana ya kuchangia hoja hii na ripoti ya Mwenyekiti wa *PAC*. Lakini kwanza kabla sijachangia niruhusu Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, kwa kurudi tena katika Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, katika Baraza hili si mgeni na mimi nimshukuru kwamba katika kipindi hichi ambacho hakuwa mjumbe wa Baraza nilikuwa naye karibu sana kwa sababu yeye kazi yake ya mwisho kabla hajakaa upande kidogo alikuwa Naibu Waziri Habari Utamaduni na Michezo.

Sasa mimi nilipopewa dhamana hii Mhe. Naibu Spika, nilimtafuta kwa makusudi kabisa nikamuomba msaada anisaidie uzoefu wake katika kuisimamia Wizara na ninashukuru kwamba hakuwa na hiana amenisaidia sana, ninamshukuru sana. Lakini pia, ninafurahi kwamba Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, ni kada mzuri sana wa Chama cha Mapinduzi, lakini pia, anaipenda nchi yake, sasa ninampongeza kwa hayo na kwa sababu mimi alikuwa akinishauri sana naomba nimpe indhari moja. Kule Kengeja Pemba ni eneo ambalo kulikuwa na wahindi wengi ukiachilia mbali mijini, sasa kuna wakati Mzanzibari mmoja mwenye asili ya kihindi alifanya kosa akapelekwa Mahkamani enzi za ukoloni, na siku zile enzi za ukoloni ukipelekwa Mahkamani ilikuwa ni jambo kubwa.

Kwa hivyo, wapemba wakapata msemo wakasema ‘yaliyomfika mtoja yasije yakamfika mpemba mmoja’. Kwa hivyo, Mhe. Mahmuod Thabit Kombo, karibu tuko pamoja katika jahazi hii.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mwenyekiti wa *PAC* na kamati yake Mhe. Omar Ali Shehe, Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake kwa namna ambavyo anafanya kazi zake. Mimi kabla ya kuwa waziri

nilipokuwa mwakilishi wa kawaida *backbencher*, kamati yangu ya mwisho niliyoifanyia kazi ni Kamati ya *PAC* na niliifanyia kazi katika vipindi viwili tofauti na katika kipindi cha mwisho nilifanya nae kazi Mhe. Omar Ali Shehe, akiwa Makamu Mwenyekiti wangu.

Kwa hivyo, ninajua uwezo wake wa kufanyakazi vizuri sana ninafurahi kwamba anaendelea na jukumu hili hadi leo na ninafurahi kwamba katika mawizara ambayo tunayaongoza tunayasimamia wakisikia *PAC* inakuja watendaji wanakuwa na hofu kubwa sana kuwaona, loo ile kamati inakuja inakuwa mtihani mkubwa.

Lakini *PAC* Mhe. Naibu Spika, katika mabunge ni miongoni mwa kamati kongwe sana katika Bunge la *House of Common* la Uingereza, Kamati ya *PAC* iliundwa miaka 1800 na ushei kuliko kamati nyengine zote, *PAC* ni miongoni mwa kamati kongwe sana. Na hadi leo bado ipo katika *House of Common,* Bunge lile la Uingereza na inafanyakazi vizuri sana. Kwa hivyo, ninakusudia kusema kwamba kamati hii ni muhimu katika Bunge au Baraza lolote lile na umakini wake inaisaidia sana serikali katika kusimamia mambo hasa yanayohusu fedha na manunuzi.

Kwa hivyo, sisi binafsi mimi ninashukuru namna ambavyo kamati hii inaanza, tulipoanza nilipokuwa mara ya mwanzo mjumbe wa Kamati ya *PAC* miaka ya mwanzo ya 200 katika Wizara mlikuwa na *query* nyingi sana Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na *volume* ukenda katika wizara ilikuwa hatari kubwa.

Lakini leo ninashukuru sana kwamba kamati hii imefanya kazi nzuri katika wizara zimo *query* na wala hazitamalizika kwa sababu ndio binaadamu tulivyo, lakini zinapungua kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hivyo, hii maana yake ni kwamba kamati hii inafanya kazi nzuri na serikali yenyewe inazingatia yale ambayo kamati hii inaelekeza, kwa sababu kamati hii imeisimamia serikali. Kwa hivyo, tunashukuru kwamba yale ambayo wanaelekeza kwa kiwango fulani yanapungua sana. Vilevile, nilivyokuwa mimi mjumbe mwaka 2000 kwa kweli sio ilivyo leo. Nimekiona kitabu hiki nikaona *alhamdulillahi* kwa kweli tumekwenda katika hali nzuri.

Na sisemi kwamba tutafika pahali iwe hakuna *query* hiyo, haiwezekani hata siku moja kwa sababu binaadamu ni binaadamu, lakini kwa ufupi kwamba *query* hizi ambazo zimetolewa na ripoti hii sisi serikali tuzifanyie kazi ili tuweze kutekeleza ule utawala bora. Na hili Mheshimiwa, mimi wenzangu tutahakikisha kwamba katika serikali kubwa tunazingatia maelekeo na maoni ya Mhe. Mwenyekiti na kamati yake.

Mhe. Mwenyekiti, jambo ambalo nimesimama kulizungumza baada ya hayo ni suala ambalo limetajwa linalohusu chumba cha chini ya bahari. Ninafurahi kwamba kamati na alizungumza Mwenyekiti kwamba uanzishwaji au uundwaji wake wa chumba kile, kilikuwa kinyume na utaratibu. Kilicho nifariji ni kwamba maneno hayo ya Makamu Mwenyekiti hayapo katika ripoti hii ya *PAC, ni* jambo zuri. Kwa hivyo, ushauri wangu kwa kamati ya *PAC* irudi *ZIPA* ikapate usahihi wa suala ambalo lilizungumzwa, mimi ni mdau mkubwa katika suala hili na nina taarifa nyingi ambazo zinahusiana na upitishwaji wa mradi huu.

Mradi huu umepitishwa rasmi na *ZIPA* na pale *ZIPA* pana maafisa mbali mbali, kuna maafisa wa ardhi, wa utalii, wa mazingira, wa uchumi na fedha na maafisa wengine. Kwa hivyo, ninachohakikisha ni kwamba maafisa hao kwa pamoja wameupitisha mradi huu, mradi huu ulipitishwa rasmi Septemba, 2012. Na tathmini ya mazingira *environmental impact assessment* ilifanywa Januari, 2011.

Sasa tukiambiwa kwamba mradi huu haujafanyiwa tathmini ya mazingira, napata mtihani kidogo. Mimi taarifa niliyonayo kwamba *EIA* ilifanywa Januari, 2011na hii ndio iliyosababisha *ZIPA* ipitishe huu mradi na taasisi zote husika, kwa taarifa niliyonayo zilishirikishwa vizuri katika kutoa maoni yao na katika kuifanya *ZIPA* iupitishe mradi husika.

Mhe. Naibu Spika, chumba hiki hivi sasa kinautangaza utalii wa Zanzibar kwa kiwango kikubwa sana, hakuna eneo ambalo utalii wa Zanzibar unatangazwa kwa kiwango kikubwa hivi sasa kuliko chumba hiki. Dunia nzima mashirika mbali mbali ya habari yanazungumzia chumba hiki kwa kiwango kikubwa sana, imekuwa ni fakhari kubwa kwa nchi yetu na inatusaidia sana.

Chumba hiki kilizinduliwa tarehe 4 Januari, 2014 mwaka huu, kina mwezi mmoja kamili na tangu kizinduliwe hakijakaa bila kupata mteja, bei yake ni dola 1500 kwa siku. Kwa hivyo, Waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanaotaka kwenda kulala pale ruhusa, pesa ni ndogo sana ni dola 1500, utapata usiku wako mmoja. Mhe. Mweyekiti wa kamati kama umeona umechoka hutaki kulala Chake Chake, basi tukufanyie *booking* uende ukapumzike katika chumba cha chini ya Bahari.

Mhe. Naibu Spika, chumba hiki hakiko chini ya ardhi ya bahari kama ilivyozungumzwa, wala hakikukaa juu ya ardhi ya bahari isipokuwa chumba hiki kinaning'inia baina ya juu ya bahari na kwenye ardhi ya bahari. Kitanda chake kiko kama mita nne hivi ndani ya maji. Na ili chumba kisiondoke kimezuiwa na nanga 4 zilizotengenezwa mfano wa matumbawe ya kuunda

ambazo nanga zimegeuka nyumba za samaki ya matumbawe hivi sasa. Zile nanga 4 za kile chumba hivi sasa kwa kiwango kikubwa kinasaidia mazalia ya samaki.

Kwa hivyo, ioneshe wazi kwamba badala ya kuharibu mazingira chumba hiki kinasaidia mazingira zaidi ya samaki na kwa kweli ni eneo ambalo hivi sasa kumegeuka kuwa na mazalia mengi sana ya samaki kwa sababu ya nanga zile ambazo zimetengenezwa kiufundi kabisa kwa kuangalia mazingira ya bahari. Eneo lile lilipo ni eneo la hifadhi ya mkondo wa *PECA* ambao nao wako makini katika masuala ya mazingira. Kwa hivyo, Mhe.Naibu Spika, nilitaka niseme haya kwa sababu taarifa hizi zinazozungumzwa katika chombo hiki kikubwa zinasikilizwa na watu wengi. Na *promotion* ya chumba hiki inafanywa na vyombo mbali mbali vyetu vya nchini na nje ya nchi na ili ku-*promote* utalii wetu.

Kwa hivyo, zikitoka taarifa ambazo hazikuwekwa sawa kwamba chumba hiki kuwekwa kwake ni kinyume na utaratibu au hakikufuata taratibu za mazingira kwa kweli wanaotusaidia katika ku-*promote* utalii wetu wanaweza kutuona kama hatuko makini na wanaweza kusita katika hilo. Kwa hivyo, mimi ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, taarifa nilizonazo ni kwamba taratibu za sheria zilitekelezwa katika kuunda chumba hiki na athari za mazingira zilizingatiwa sana na kuwepo kwake kunasaidia sana katika kuitangaza nchi yetu kiutalii na pato ambalo linatokana na chumba hiki kwa kweli linatusaidia sana. Chumba kimoja hiki ni dola 1500 kama nilivyozungumza ukizipigia mahesabu ni 2,400,000 ni sawa vyumba 40 vya shilingi 60,000, 60,000.

Sasa utaona chumba kimoja ambacho kiko baharini hakiharibu mazingira, lakini kipato chake kwa kweli kwa siku ni sawa na vyumba 40 vya hoteli vya shilingi 60,000. Sasa utalii wa aina hii ndio ambao sasa hivi ndio tunaukaribisha nchini, kwa sababu ni jambo dogo, lakini lina athari kubwa. Na kila mgeni anayetembelea pale kwa kweli anafurahi kwamba tumefanya jambo kubwa.

Nilimkuta mtu mmoja pale mara moja yeye na mkewe wameshakaa wiki mbili mfululizo, weshaambiwa *booking* yao imekwisha, wanasema tunaomba tuongezwe siku mbili, wanaambiwa imemaliza wapisheni wenzenu, kwa sababu kwa kweli ukifika mle ndani utaona mambo ya ajabu sana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari; Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, nakumbuka aliwahi kukitembelea hiki chumba. Kwa hivyo, niko tayari Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* na kamati yake wakiwa tayari, basi angalau twende pale siku moja tuwapeleke wakakione, waingie mle ndani, kulala tu itakuwa mtihani kidogo, lakini kutembelea kwa

masaa machache tutafanya maarifa ili wakathibitishe kwamba mazingira na hali yake kwa kweli yamewekwa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nikitaka kusema hayo nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi kuzungumza juu ya suala la ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa mara nyengine tena. Wajumbe wanafahamu kwamba Mhe. Mahmoud tulikuwa naye hapa akiwa Mwakilishi wa Mpendae na aliwahi kupewa nafasi ya unaibu waziri wa habari, na tulimuona uwezo wake katika kufanya kazi katika *term* hiyo, ni mtaalamu wa masuala ya *IT* na anayafahamu vizuri mambo ya mawasiliano na mengineyo. Kwa hivyo, Baraza bila shaka itabidi lijivunie kumpata mtu kama huyu kuingia katika Baraza hili kwa mara nyengine tena kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, karibu tena katika Baraza la Wawakilishi na kama kawaida yetu tutaendelea kushauriana kama tulivyokuwa tukishauriana wakati tuko pale Kikwajuni juu ya mambo mbali mbali yanayotokea katika Baraza hili. Kwa hivyo, tuko pamoja kumpa mashirikiano makubwa.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ana uwezo mkubwa kabisa wa kuandika maudhui na akawasilisha pahala na yakaeleweka vyema. Kwa hili nampongeza sana ni kipaji cha aina yake, na kwa kweli anasaidia sana katika kufunua macho watu wanaomsikiliza.

Vile vile, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali namna anavyofanya kazi yake vizuri kabisa na huwa anatoa *samples* katika ripoti zake ambazo zinaleta utanabahisho mkubwa sana katika kujua namna mambo yanavyokwenda serikalini.

Mimi kwa upande wangu Kamati hii na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika wizara hii ya ardhi imenipa utanabahisho mkubwa sana, utanabahisho wa mambo mengi sana ambayo hata ningekaa nikamaliza muda wote kuna mambo mengi ambayo yameorodheshwa katika orodha hii nisingeyajua. Kwa hivyo, imenisaidia sana katika kutambua mambo mengi kabisa ambayo yatanisaidia sana katika kutekeleza majukumu yangu.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi nitazungumza kidogo tu katika baadhi ya mambo sio kwa dhamira ya kujibu hoja, mimi ni mchangiaji wa kawaida, lakini kwa dhamira ya kueleza tu baadhi ya mambo ambayo katika hali halisi na katika sura yake halisi yako vipi katika mambo mbali mbali yaliyotajwa katika Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme wazi kuwa kimsingi nakubaliana na hoja ya kuzilipisha kodi *jet* zote zilizojengwa baharini. Aidha, natambua kuwa teknolojia ya ujenzi wa vyumba vya baharini umeshaanza na tunaupokea kwa hadhari kubwa sana. Jambo lolote jipya linataka tahadhari na halihitaji papara katika kulipokea.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na sababu hizo basi; Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati imeona umuhimu wa kutunga sheria maalum na baadae kanuni ziandaliwe ili zitoe muongozo katika utoaji wa kodi za ardhi yaani *special lease rent for jets and under sea water rooms*. Hili ni suala muhimu lazima tulifanyie kazi katika wizara yangu.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni kwamba ni kweli kuwa kodi za ardhi hazijafanyiwa mapitio kwa muda mrefu, lakini hata hivyo hapa napenda niseme kwamba, Wizara yangu ilibaini kasoro hizo na kuunda kikosi kazi cha kufanya kazi hii. Ada ya kodi mpya ya ardhi zimetengenezwa na zimeanza kutumika rasmi kwenye bajeti hii ya mwaka 2013/2014. Zimepelekwa Wizara ya Fedha na ndio zilizoweza kuwekwa katika bajeti ya mwaka huu wa 2013/2014. Pia, suala la kuzipitia sheria na kanuni zake ni kwamba, katika wizara yangu kuna programu maalumu ya kufanya marekebisho ya sheria za ardhi pamoja na kanuni zake. Hatua ya mwanzo ilikuwa ni kuziorodhesha sheria zote zenye kuonesha kasoro.

Hatua ya pili Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tumeajiri mtaalamu wa kimataifa wa sheria ili aishauri wizara namna bora ya kuziboresha biashara hizo, kazi hiyo itakamilika mwezi wa Oktoba mwaka huu wa 2014.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi nimekuwa nikizungumza katika Baraza hili juu ya matatizo na changamoto mbali mbali zilizomo katika Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mara nyingi nazieleza hapa na narejea tena kuzieleza, na ninakumbuka mara ya mwanzo niliposimama katika Baraza hili kuzungumzia juu ya wizara hii nilisema kwamba, kuna kazi tunalazimika kuzifanya katika wizara hii. Na kwa kweli Mhe. Naibu spika, tumeanza kuzifanya hizo kazi, imekuwa ni sawa sawa na kwamba nimekusanya rundo la nguo mtoni ninafua akaja mtu akanambia nguo zako mbona chafu hizo, ndio ninazifua na ndio maana niko hapa niko katika kazi hiyo ya kuzifua hizi nguo kwa sababu ni chafu. Sasa ndivyo ilivyotukuta hii Kamati ya *PAC*

katukuta tuko kazini, sasa astahamili kwamba sisi tuko kazini tunafanya ile kazi ambayo tunatakiwa tuifanye.

Mhe. Naibu Spika, wamesema hapa kuna uchache wa wafanyakazi katika Idara ya Ardhi, ndio kweli, lakini nawaambia walikuwa wengi lakini hawapo ndio tuko katika kusafisha huko. Kuna wengine wako katika maeneo mbali mbali, wako wafanyakazi vile vile hawapo na aende sasa hivi kama atawakuta. Kwa sababu unamuonya mtu, unamtahadharisha mtu, unamrekebisha mtu harekebishiki, akirekebishika huna tatizo utaendelea kuwa naye, harekebishiki utaendelea kubakia naye? Huwezi kubakia naye Mhe. Naibu Spika. Sasa hii ndio hali halisi.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyofahamu kuwa serikali ilichukua uamuzi wa kuiteua taasisi ya *ZRB* kuwa ni wakala wa ukusanyaji kodi za ardhi. Hii haina maana kuwa wizara yangu haina dhima katika suala hili, dhima ninayo. Nasema kwamba tutazidisha jitihada za kutoa mashirikiano ya karibu sana na ya kitaalamu na kiutawala ili kuhakikisha kuwa hapatokei mwanya wa ukwepaji kodi, pamoja na kuziba mianya inayovujisha mapato yatokanayo na kodi za ardhi. Hii kazi Mhe. Naibu Spika, ndio tunayoendelea nayo hivi sasa kuifanya katika wizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la sheria za uwekezaji ambazo zile kusema kweli zinaelekeza kuwa mwekezaji anapoingia nchini kwanza anatakiwa kufika *ZIPA* ili atambuliwe kwa kupatiwa *internal certificate*, *certificate* hiyo inamuongoza mwekezaji kufika kwa Waziri wa Ardhi ili apewe eneo linaloendana na azma yake ya uwekezaji kama ni kiwanda, kilimo au hoteli. Hivyo, mahusiano ya *ZIPA* na ardhi katika masuala ya uwekezaji ni ya karibu sana. Najitahidi sana kufanya kazi kwa ukaribu na tunashauriana kwenye mambo mbali mbali kabisa, lakini ndio nasema wamekuja wametukuta tuko katika hiyo kazi yenyewe.

Sasa tutapokea hii ripoti, tutapokea maagizo tutakayopewa kama tulivyoyakuta katika ripoti hii, na kuna maagizo mengine tushayapata kutoka katika serikali kwa ripoti hii ya *CAG* kwa sababu hii katika serikali pia imeshajadiliwa hii ripoti na kuna maagizo mengi kabisa yameshatoka katika serikali ambayo tumepewa mawaziri mbali mbali, tutayafanyia kazi haya pamoja na hayo tuliyoyapata kutoka serikalini katika kuona kwamba tunafanikiwa katika kutekeleza kazi hii.

Mhe. Naibu Spika, kuna ardhi ambazo hazitumiki limezungumzwa sana hapa. Nataka kusema kwamba ardhi hizo ziko aina tatu; kuna ardhi ambazo hazina hati yoyote lakini zimezungushwa ukuta na zinaambiwa zina mwenyewe. Mhe. Naibu Spika, ardhi hizi hazina mwenyewe, ardhi hizi ni mali ya serikali

na nimekwishakusema hapa tunazirejesha serikalini na narejea tena nazirejesha serikalini. Anazungusha ukuta tu mtu anasema ardhi hii hapa yote ni yangu hajafuata sheria yoyote hajaiomba, ameiweka pale, huyu ni *speculator* kama alivyosema Mjumbe mmoja hapa amekusanya ardhi ili akatafute mtu amuuzie, uchumi hauendeshwi hivyo, lazima twende kwa mujibu wa sheria kujua kanuni na taratibu.

Sasa ardhi ya aina ya pili ni ardhi ambazo zina *lease*, lakini zina kesi Mahakamani, hizo bila shaka itabidi zisubiriwe kesi imalizike mahakamani, maana kitu kikiweko Mahakamani huwezi tena ukakifanya mambo mengine mengine pale.

Ardhi ya aina ya tatu ni zile ambazo zimepewa *lease* lakini hazina tatizo lolote, hizi tunazifuta kwa sababu zimekaa pale hazina kazi yoyote, mtu kaziweka tu pale na *lease* kapewa lakini hazitumii. Ndio maana katika kitabu hiki kuna orodha ndefu huku mwisho hii ni kazi ambayo Mhe. Naibu Spika, tumeshaifanya katika wizara yangu, na nadhani kamati wameikuta iko tayari hii kwa sababu ninazo kopi zake, zote hizi zilizoorodheshwa huku ni kazi ambayo tumeifanya ndio tunafua hizo nguo chafu, na ndio maana wakatukuta tunazo hati hizi tayari katika ofisi, tayari tumeshazitafuta, zilikuwa ziko sehemu mbali mbali tumepeleka watu wamepita kusini kaskazini wamezikusanya hizi na hivi sasa wanaendelea na Pemba katika kuona kwamba ardhi hizi zimekaa hazina kazi, ndio hizo tunazozungumza lakini ziko katika matatu kama nilivyozichambua hapo mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, mimi naipongeza sana kamati, nampongeza tena *CAG* amenitanabahisha kwamba kuna ardhi *lease* imepelekwa nyengine lakini kinacholipwa ni pungufu. Unasaini hati ya *lease* dola 20, sasa mimi najiuliza kwa nini huyu anaruhusiwa kulipa dola 15, 000 wakati anatakiwa alipe dola 20,000? Hii ni tanbihi, namshukuru sana *CAG*, naishukuru sana Kamati wa kulileta suala hili.

Kuna ardhi ambayo inatumika lakini hailipi kodi. Sasa inatumika vipi na hailipi kodi na hili ni tatizo. Nadhani ipo haja ya kupeana taarifa juu ya masuala kama haya. Naishukuru sana kamati kwa kutoa taarifa yenye masuala haya.

Suala la kusamehe *lease* Mhe. Naibu Spika, hili katika kipindi hiki limekatazwa na halitumiki. Ni juzi tu hapa tulipopitisha bajeti kuna vifungu vya ile sheria ya bajeti vinavyoeleza kwamba, Waziri wa Ardhi peke yake hawezi kusamehe *lease* wala hawezi kupunguza *lease* mpaka ashauriane na Waziri wa Fedha. Huu ni utaratibu mpya ambao mimi nimeupenda na ni mzuri kwa sababu sasa hivi tutakuwa tukikubaliana badala ya kuwa kapu lote

analo mtu mmoja sisi tutakuwa tuko wengi tunafanya kazi moja hii ya kuona kwamba hivi sasa huna ruhusa ya kusamehe au punguza *lease* bila ya kushauriana.

Sababu zipi zinazosababisha ile *lease* ipunguzwe? Baraza hili limepitisha uamuzi huo na mimi ninalo na nimeanza kulifanyia kazi, limeanza kunipa shida kidogo kwa sababu bado kuna watu wanasema wewe ndio waziri mwenye *jurisdiction* ya kusamehe mbona unatubabaisha, sikubabaishini, tunakwenda katika mfumo mpya sasa hivi hatwendi katika ule mfumo wa kizamani, lazima tufuate huu utaratibu mpya ambao tumeuweka.

Halafu kuna ardhi ambayo kachukua mtu mmoja, mtu mmoja utamkuta ana ardhi hekta 10, 15 peke yake za nini? Hizi lazima tuzipunguze, hii kazi tunaendelea nayo hivi sasa Mhe. Naibu Spika, ni suala ambalo tunaendelea nalo na tunalifanyia kazi kadiri tunavyoweza.

Mhe. Naibu Spika, ziko hoja nyengine zimezungumzwa hii hoja ya Idara ya Ujenzi ya kughushi *voucher* pamoja na *cheque* za namna mbali mbali. Hii Mhe. Naibu Spika ni kazi yetu wenyewe, tumeigundua sisi wenyewe, *CAG* tumempeleka kwenda kuthibitisha tu ubadhirifu huu, na kwa kweli kaenda na kathibitisha ubadhirifu huu kwamba kweli upo katika idara ile, tumefuata sheria, tumeripoti kunakohusika na tumechukua hatua za kinidhamu watu hawa sasa hivi hawako.

Kuna siku moja waliombewa hawa hapa hapa kwenye Baraza, waliombewa bwana waacheni wanakaa nje hawana kazi sijui mnawaonea aah, ngojea polisi imalize kazi yake, maana polisi nayo ina kazi hii, tungojeni polisi imalize kazi yake halafu tutajua tumefika wapi juu ya suala hili. Hii ni kazi tumeifanya na tumeigundua namshukuru Mwenyezi Mungu *CAG* ametusaidia na ametuonesha suala hili. Ni vizuri sasa zimekuja kwenye ripoti hii kwa ajili ya kuona, hili litasaidia kuziba mianya na wengine wenye mtindo wa kuongeza zero na kuongeza *ten*, na mambo mengineyo kwa sababu ya kutuibia ni pesa nyingi hatuwezi kukubali. Sheria inatwambia tukiiona hali kama hii turipoti kunakohusika, na hii kazi yote tumefanya Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, liliulizwa swali, sikuulizwa mimi aliulizwa Waziri aliyewasilisha mada hii. Limeulizwa swali la deni la umeme. Mhe. Naibu Spika, kuhusu ongezeko la bei ya umeme deni la umeme kwa *TANESCO* matumizi na mapato ya umeme kwa Shirika la Umeme. Deni la umeme la serikali kwa *TANESCO* kwa sasa kwa upande wa Unguja ni shilingi 41,577,982,290.27. Kwa upande wa Pemba ni shilingi 521,518,073.74, ndio maana jumla ya deni inakuja shilingi 42,099,500,364.

Deni hili limepatikana kama jana nilivyosema kwamba, kadiri wanavyozungumza na *TANESCO* watendaji wa *TANESCO* na watendaji wa *ZECO* wakizungumza wakirejea katika makubaliano ambayo walishayafanya zamani hili deni nalo linapungua linakuja katika kiwango kizuri zaidi. Deni hili tumelipangia utaratibu wa kulilipa na nitalieleza baadae.

Kuhusu makusanyo ya umeme. Kwa sasa ni kweli kuwa makusanyo ya shirika kwa sasa yamepanda na kufikia kwenye shilingi bilioni tano, ambapo kupanda huko kumetokana na maboresho au jitihada zinazofanywa na Shirika hivi sasa. Baraza hili limelisaidia sana shirika kukaza buti sasa katika masuala ya kukusanya mapato, huo ndio ukweli. Kwa hivyo, mapato yameongezeka kiasi hicho pamoja na kupanda kwa bei ya umeme. Hii imeliwezesha shirika kuweza kulipa bili ya umeme kwa miezi yote na kugharamia gharama ya uendeshaji wa shirika hivi sasa.

Kwa mfano, mwezi wa Disemba mwaka 2013 mapato ya mwezi ya makusanyo yalikuwa shilingi 5.54 bilioni, malipo kwa *TANESCO* yalikuwa ni shilingi 3.13 bilioni na malipo ya gharama ya uendeshaji shirika ni 1.12 bilioni na gharama ya shughuli za maendeleo ni shilingi 1.23 bilioni. Limeweza kufanya shirika katika mwezi wa Disemba.

Lakini kuna hili deni. Hivi sasa kutokana na uendeshaji wao na wakiendelea kukaza kamba zaidi na kuendelea kukusanya na kuweka mita za TUKUZA katika maofisi anayeweza kuchukua mita hizo, kwa sababu sio maofisi yote yenye uwezo wa kuchukua mita za TUKUZA, kuna maofisi mengine yanachukua umeme mwingi sana na mita za TUKUZA zina kiwango chake zile, ikifika kiwango fulani mita ile haiwezi kuchukua tena. Hii inabidi labda yule mwenye ofisi agawe vile viwango vya umeme katika sehemu mbali mbali ya lile jengo lake. Kwa hivyo, kwa maeneo ambayo yanaweza kuchukua mita za TUKUZA, sasa hivi tumeamua kabisa tuweke mita hizo katika maeneo yale ili kuongeza mapato, kwa wanaodaiwa operesheni katakata tunaendelea nayo na tutaendelea nayo, na hatutaki kuwa na muhali.

Juzi tulikuwa tukizungumza katika shirika tumewaeleza wale na tumekubaliana nao juu ya masuala haya kwamba, hebu onesheni kuwa nyinyi mna-*authority* katika suala la kuuza umeme, msimuonee haya mtu. Wamejaribu kwenda katika maofisi yetu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na katika ofisi za Muungano wamekwenda vile vile, Jeshi, Polisi huko nako tutakwenda na katakata ya umeme walipe. Kwa sababu hatuwezi tukawaachia watu wakatumia umeme bila ya kulipa. Sasa katika kulipa deni tuna utaratibu tumeuweka hapa ndio nazitaja zile.

Hili suala Mhe. Naibu Spika, limeshazungumzwa na Waziri wa Fedha na ndio maana jana nilipo *wind-up* mimi sikulitaja hapa kwa sababu tayari limeshazungumzwa na Waziri wa Fedha. Kuna shilingi 18 bilioni za *PAYE* ambazo Serikali ya Jamhuri ya Muungano imekubali kuzirejesha Zanzibar, fedha hizi zipelekwe *TANESCO*. Na hii tumekubaliana katika kikao cha kero za Muungano Dodoma chini ya Mwenyekiti Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu alikuwepo, Makamu wa Pili wa Rais tulikuwa naye pale katika mkutano ule pamoja na mawaziri mbali mbali tulioshiriki katika kero za Muungano wa kule na wa huku tumekubaliana shilingi 18 bilioni zikalipe deni hili la shilingi 41 bilioni.

Halafu kuna taasisi za serikali mbili zinatumia umeme sana na ukizikatia ni hatari. Hivyo Wizara ya Fedha iliamua kwamba madeni ya taasisi hizo yalipwe na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wizara ya Afya ukiikatia umeme Wizara ya Afya ni hatari pale hospitali na *ZAWA* ambao wanasambaza maji ukiwakatia umeme ni hatari kwenye masuala ya maji. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekubali kwamba pesa hizi itazilipa yeye, sasa hizi zote mpaka sasa hivi jumla yake ni shilingi 12 bilioni. Katika utaratibu huu tumekubaliana kwamba pesa hizi zilipwe kidogo kidogo kufidia deni au kupunguza hili deni. Kwa hivyo, hizo zinalipwa huko hivi sasa tunaendelea na utaratibu huo.

Deni lililobakia *management* ya *ZECO* itakutana na *management* ya *TANESCO* kukubaliana namna ya kulipa hilo deni ikiwemo kupewa muda wa kutosha ili kujipanga kulipa hilo deni, yaani watatengeneza *schedule* ya hiyo iliyobakia, 18 na 12 maana yake 30 bilioni hizo. Kwa hivyo, katika 42 ukitoa 30 *billions* itabakia 12 *billions*, hizo itabidi wakubaliane. Na wanayo *modality* ambayo washakubaliana sasa hivi kwamba watazilipa vipi ili hili deni liondoke kabisa.

Sasa kama itatokea kukatiwa umeme nadhani itatokea kwa uzembe wa utekelezaji wa masuala haya. Haya yakitekelezwa kwa sababu walikwenda wenyewe. Mwenyekiti alipoleta barua wakati ule akasema kwamba tutawakatia umeme Zanzibar, *ZECO* walikwenda *TANESCO* na wakafanya kikao na mwenyekiti na wakakubaliana utaratibu huu ambao nauzungumza hapa, ambao huu utalipunguza deni na utalimaliza kabisa madhali sasa wana uwezo wa kulipa deni la kila mwezi, ile bili inayokuja kila mwezi wataweza kuilipa itakuwa sasa hivi wanapambana na kulipa deni kwa utaratibu mwengine ambao watakubaliana namna ya kufanya ili kukamilisha masuala ya deni.

Mhe. Naibu Spika, kuna mengi lakini nadhani muda hautoshi kuyazungumza yote, yametajwa mengi haya na mimi nayapokea, lakini kuna moja liliulizwa

asubuhi hapa naona hilo nalo nilijibu. Kwani hizi *rent* za ardhi ni kiasi gani? Kwa taarifa ya Baraza ni kwamba katika *review* ya juzi mwaka 2013/2014 kwa mgeni hekta moja analipa dola 5,000 kwa mwenyeji analipa nusu ya dola 5,000 huyu ni mwekezaji mzalendo. Hizo ndio *rent* ambazo zinatumika hivi sasa ambazo ndizo sasa hivi *lease* zote zinaandikwa kwa msingi wa kutizama hizo, hiyo ndio kazi tunayoendelea nayo.

Mhe. Naibu Spika, tuko kazini tupeni nafasi tuendelee na kazi, na ninategemea kwamba tutakwenda kidogo kidogo na tutafika katika masuala haya *Inshaallah* naomba Mungu atuwezeshe tu. Ahsanteni naunga mkono hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niseme machache sana.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana ndugu yangu Mahmoud Thabit Kombo kwa kuteuliwa na wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki kuwa Mwakilishi wa Jimbo hilo. Kwa kweli ndugu yangu Mahmoud Thabit namuelewa vizuri, uwezo wake mkubwa katika kufanya kazi na kwa msingi huo sina shaka yoyote atawasaidia sana wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki na atalisaidia sana Baraza hili na nchi kwa jumla. Kwa hivyo, tumuombee dua Mwenyezi Mungu amsaidie aweze kufanya wajibu wake vizuri sana.

Aidha, nichukue fursa hii kuvishukuru vyama vyote vilivyoshiriki uchaguzi katika Jimbo la Kiembesamaki kwa kufanikisha uchaguzi vizuri kwa salama na utulivu mkubwa.

Baada ya maelezo hayo sasa nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* na Wajumbe wote wa *PAC* kwa kazi nzuri na kubwa waliyoifanya katika kutayarisha ripoti hii ambayo ni ripoti nzuri na mimi sina budi kuwapongeza kwa niaba ya serikali kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Aidha, nimpongeze sana ndugu yangu *CAG* naye kwa kazi zake anavyozifanya vizuri, kwa uadilifu mkubwa, kwa umakini wa hali ya juu. Wanafanya kazi vizuri sana na za kupigiwa mfano nawashukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze na kusema neno ambalo limezungumzwa na baadhi ya Wajumbe hapa, wamesema kwamba serikali inadharau Baraza hili. Mheshimiwa nataka niwahakikishie Wajumbe hatuna nia ya kudharau Baraza, na hata siku moja hatufanyi hivyo na hatutofanya hivyo. Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo hapa

zamani hoja hizi za *PAC* zinapokuja hapa zilikuwa nyingi sana, na ukiona utaona yalikuwa makosa mengi zaidi, lakini sasa hata Mwenyekiti mwenyewe wa Kamati ya *PAC* na Wajumbe wataona namna ambavyo serikali inavyochukua ushauri na mapendekezo yanayotolewa na kamati hii na Wajumbe wa Baraza hili katika kurekebisha kila lile ambalo linatakiwa lirekebishwe.

Nia yetu sio hata kidogo kuwaficha au kuwakingia kifua wafanya makosa, nia yetu ni kuchukua hatua, nia yetu ni kurekebisha, ili tuwe na serikali nzuri, inayowahudumia wananchi vizuri na hatuko tayari hata siku moja fedha za umma hizi zitumiwe visivyo. Nia ni kuhakikisha kwamba fedha za umma zinatumiwa kwa utaratibu mzuri.

Kwa hivyo, ningependa sana kuwahakikishia Waheshimiwa kwamba haya yanayozungumzwa na yanayosemwa sisi tunayapokea na kwenda kuyafanyia kazi kama ambavyo yameelekezwa. Lakini sisi serikali pia ni binadamu na watendaji ni binadamu, kwa hivyo makosa katika utaratibu wa siku zote wa maisha yanatokea, lakini cha msingi nikubali kwamba lile kosa linapotokea kurekebisha kosa na kuweka utaratibu ulio mzuri zaidi wa kurekebisha makosa haya. Nataka nilihakikishie Baraza hili kwamba haya yaliyosemwa mara hii yatashughulikiwa na mwaka ujao *inshaallah* hayatatokea ya namna hii.

Lakini ikiwa yatatokea ni ya kibinaadamu ambayo hatutarajii yatokee, lakini kwa bahati mbaya yanaweza kutokea. Kwa hivyo, ningependa sana Waheshimiwa Wajumbe muelewe kwamba serikali hii ina imani kubwa na wananchi wa nchi hii, na iko tayari kuwatumikia na tusingependa ziweko fedha zinaharibiwa wakati zinahitajika kwa kutoa huduma mbali mbali zikiwemo za elimu, afya na huduma nyengine muhimu. Tunajua umuhimu wa kuwahudumia wananchi wetu. Kwa hiyo, tunataka hata ile senti tano itumike vizuri kwa msingi wa kukidhi haja na malengo ili tuweze kufanya huduma zenye tija na ufanisi wa hali ya juu.

Vile vile, lilizungumzwa suala la kuwa tunabadilisha malengo ya Mapinduzi Matukufu katika suala zima la ardhi. Nataka niwahakikishie Wajumbe kwamba nia yetu ni kuhakikisha tunaendeleza malengo na madhumuni ya Mapinduzi ya mwaka 1964. Na hatuna nia kabisa ya kuitoa ardhi hii kwa wageni, lakini tunatumia ardhi hii kuikodisha kwa wawekezaji kwa misingi ya sheria ili isaidie kupatikana kipato tuweze kutoa huduma vizuri zaidi.

Utaratibu wetu hatuuzi ardhi Mhe. Naibu Spika, tunaikodisha kwa mradi na tunaangalia aina ya mradi na ndio hapo basi tunamkodisha muwekezaji na atafanya shughuli zile za kimradi kutokana na masharti aliyopewa, na hata

siku moja ardhi ya Zanzibar hawatouziwa wageni. Isipokuwa kuna utaratibu maalumu wa kukodishwa ardhi kwa misingi ya kuendeleza Wazanzibari wenyewe.

Na nia yetu kabisa kuona katika uwekezaji huo unawafaa zaidi wananchi wa Zanzibar. Tutachukua kila hatua pale inapowezekana kuona namna gani tunaweza kuweka taratibu nzuri zaidi zitakazowawezesha Wazanzibari kuweza kupata maslahi zaidi kwa uwekazaji unaofanyika nchini. Mwenyezi Mungu atujaalie suala letu la mafuta hili lijitokeze liweze kusaidia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya Zanzibar.

Napenda Waheshimiwa niwahakikishie kwamba nia ni njema kabisa tatizo bado ni uwezo mdogo tulionao wa kiuchumi ndio maana unapunguza kwa njia moja au nyengine kutoa zile huduma ambazo tunazitaka zitolewe kwa kiwango cha hali ya juu. Lakini tutafanya kila jitihada kadiri kinachopatikana kitumike vizuri ili tuimarishe yale yaliyokusudiwa kwa vitendo na yanufaishe wananchi wetu.

Nataka niwahakikishie tu kwamba wale watendaji ambao wataendelea kufanya mambo kwa kutofuata utaratibu na sheria za matumizi zilizowekwa, serikali itachukua hatua kali dhidi yao kwa mujibu wa sheria ili kuhakikisha kwamba hali hiyo inakwenda vizuri. Na mimi nataka niwapongeze sana kamati ya *PAC*. Mhe. Said Ali Mbarouk, alisema sasa hivi ikisikikana *PAC* inakuja basi katika taasisi mbali mbali huwa wanajua kwamba kazi sasa inakuja.

Kwa hiyo, ndugu zangu uzi huo huo muendelee nao, na sisi tunaunga mkono jitihada hizi kwa nia ya kuleta mabadiliko ili tujirekebishe kuhakikisha kwamba sote tunaheshimu fedha za umma, fedha za serikali zinatumika kwa maslahi ya watu. Wasitokee watu binafsi kujinufaisha kwa maslahi yao. Hilo ni jambo ambalo litaendelea kupigwa vita na halitokaribishwa katika serikali yetu. Na yeyote yule atakayetumia nafasi yake ya uongozi katika kujinufaisha binafsi, basi hatua kali juu yake zitachukuliwa. Ndani ya serikali hatutomvumilia yeyote ambaye atakwenda kinyume na mambo yale.

Kwa hiyo, nawaomba tu Waheshimiwa mtuachie tukaifanyie kazi ripoti hii ili *inshaallah* kila taasisi husika ya serikali iweze kuleta majibu yake sahihi. Mnatupa kazi hii na tunakwenda kuifanya kwa misingi ya kurekebisha yale ambayo yametokea.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono taarifa hii ya kamati na niwatakie kamati na Baraza hili tukufu maamuzi mazuri. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora: (Kaimu Waziri wa Fedha): Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa, wasaa huu kwa mara nyingine tena kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Fedha kuja kujibu hoja mbali mbali za Waheshimiwa Wajumbe kutokana na ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika yaani *PAC* kama ilivyowasilishwa asubuhi ya leo na Mwenyekiti wake Mhe. Omar Ali Shehe.

Mhe. Naibu Spika, naomba na mimi niungane na wenzangu kumshukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kwa ufasaha wake, ujemadari wake kama kawaida, kwa kukiongoza kidogo hiki au kamati hii ya *PAC* kwa kipindi sasa, nafikiri kama sikosei cha tatu au cha nne.

Mhe. Naibu Spika, hii inaonesha ni imani kubwa Baraza tulilonalo kwake pamoja na Wajumbe wenzake kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kuisaidia serikali katika kuibua mambo ambayo labda kwa njia moja au nyengine serikali peke yake haiyaoni. Na niseme huu ndio msingi wa Utawala Bora. Misingi ya Utawala Bora leo tunashirikishwa katika kufanya kazi kwa pamoja. Hili ni suala muhimu sana na wote tunawajibika kwa pamoja, tunatoa ushauri na sisi tunaupokea kama walivyozungumza Waheshimiwa Mawaziri, sisi ni serikali sikivu inayokubali kushauriwa na tunajitahidi kuyatekeleza hayo tunayoelekezwa.

Nafikiri katika serikali ambazo zinajenga misingi ya kidemokrasia hakuna serikali inayokataa ushauri au maelekezo hasa yanayotoka kwa Wajumbe wa Kamati kama hii ya *PAC* ambayo mambo haya wameyaibua si kwa kubuni tu, lakini wamekwenda *field*.

Kwa hiyo, mimi namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wote wa kamati na Waheshimiwa wote wengine waliochangia. Kwa kweli michango yao tumeipokea, tumeisikia, tumezingatia na kama walivyosema Waheshimiwa mawaziri walionitangulia kwamba haya sasa yanakwenda kufanyiwa kazi.

Mmeshatupa indhari kwamba kumbuka Mhe. Salmin Awadh Salmin na wengine tumeoneshewa kidole hapa tukifika bajeti kama haya yaliyoibuliwa hayajatekelezwa basi tena tusije kulaumiana. Mimi nakuahidi Mhe. Naibu Spika kwa niaba ya wenzangu kwamba sisi mara moja tutakwenda kuyafanyia kazi haya kama yalivyoelekezwa na kamati hii, na tutaona utaratibu wa kisheria nao unasemaje.

Sisi hatutopinga chochote na tutayagawa nafikiri kama ulivyoweka mwenyewe Mhe. Mwenyekiti kwa kila wizara na sehemu yake. Basi na kila

wizara yamo, huu ndio utaratibu wetu tunawagaiya tena si kwa kuyazingatia, kwa kuyafanyia kazi tumeona mapungufu haya, kwa kweli hayatajirudia tena. Mhe. Naibu Spika, nimezungumza kuna mengine naona yamejirejea rejea mwaka hadi mwaka. Si lengo zuri kwa kweli kama kitu kimesharekebishwa mwaka mmoja tena haina maana itokee mara ya pili au kwa mwaka unaofuata. Kwa kweli, kama kuna watendaji wanaofanya hayo basi na sisi tutakwenda nao sambamba kama alivyoeleza hapa Mhe. Waziri aliyenitangulia kama hatutowanyamazia watu kama hawa.

Kwa hivyo, niwasilishe shukurani zetu kwa Mwenyekiti na Wajumbe waliochangia pamoja na Waheshimiwa Mawaziri waliosaidia kujibu hoja kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli Waheshimiwa wamechangia mambo mengi sana, lakini kwa ujumla mimi naomba niyataje mambo kama manane hivi ambayo nahisi ndio yalizungumzwa na Waheshimiwa wengi sana.

1. Kwanza Ofisi ya *CAG* mwenyewe.

2. *ZIPA*, hasa suala la *One stop center* hili limezungumzwa na Waheshimiwa wengi sana na wameonesha mapungufu yaliopo katika kitengo kile.

3. Waheshimiwa wengi sana wameoneshwa kutoridhishwa kwao na kutofuatwa utaratibu wa sheria ya fedha na manunuzi. Kuna mapungufu mengi sana yamebainika mbali tu na sheria hii tumepaswa sote tuisome, tuifahamu na watendaji wetu wasirejee makosa haya mara kwa mara. Lakini bado Waheshimiwa mmeweza kuibua mapungufu mengi katika utendaji wetu wa kila siku na kuweza kukhalifu sheria hii ya fedha na manunuzi.

Vile vile, masuala ya ardhi nayo yamechukua sehemu kubwa kabisa ya mjadala, na Waheshimiwa wengi wameweza kuchangia. Nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Ardhi,Makaazi kwa kweli kwa maelezo yake ya kina na kufafanua mambo.

Kuhusu madeni ya Taasisi za Serikali hasa umeme. Nalo hili Waheshimiwa wengi wamezungumza lakini pia na taasisi zetu wenyewe na tunashindwa kulipa madeni hayo ilhali *OC* tunatiliwa.

Waheshimiwa wengi wamezungumzia makusanyo machache ya kodi stahiki. Hili nalo limeonekana ni upungufu mkubwa sana kwamba wengi walifika hata kusema kwamba Zanzibar sisi si masikini. Tunao uwezo tukijipinda vizuri tukajipanga vizuri basi kodi ambazo zinazostahiki zikusanywe hizi tunaweza tukazikusanya vizuri.

Pia Waheshimiwa wengi mlizungumzia suala zima la kufunga hesabu za serikali au za wizara au taasisi tena kwa wakati. Hili Mhe. Naibu Spika, naona nilijibu moja kwa moja kwa kweli hapa tumepiga hatua sana. Nilizungumza na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mwaka jana yaani kuishia tarehe ya 30 Septemba amenambia hili limetekelezwa kwa asilimia 99, taasisi zote zimeweza kufunga hesabu japo wengine walichelewa kwa siku tano, sita, lakini asilimia 99 wameweza kufunga mahesabu yao.

Kwa kweli, hii inaonesha wazi kwamba maoni yenu Waheshimiwa yanafanyiwa kazi, na huu ndio ushahidi tosha ambao unajieleza wenyewe. Madeni ya serikali nafikiri nimemaliza. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla serikali inakubaliana na mambo yalioibuliwa na kamati na mapendekezo waliyoyatoa kamati hii ya kuchunguza hesabu za serikali.

Naomba kuahidi mbele yako Mhe. Naibu Spika, kwamba mapendekezo yote yaliyopendekezwa tunayachukua serikalini na tutayafanyia kazi kama vile kamati walivyopendekeza. Katika kuyafanyia kazi mapendekezo hayo serikali itazingatia sheria na taratibu zilizopo kwa madhumuni ya kutenda haki katika kila hoja iliyowasilishwa na kamati. Kwa mfano zipo hoja ambazo zimefafanuliwa zikiwa na makosa yaliyofanana, isipokuwa kamati imejaribu kutoa maoni tofauti kuhusiana na makosa hayo. Tulihisi kidogo kwa mitizamo ya serikali hii sio sahihi, itabidi tukae vizuri kujipanga kuona kwamba kama suala ni moja basi mapendekezo yawe mamoja pia kwa kesi kama hizo zote.

Hivyo, kutokana na mapendekezo yote yaliyowasilishwa na kamati. Serikali kwa upande wake itaitisha mapendekezo hayo yanayowasilishwa katika wizara husika kwa ajili ya kuyafanyia kazi ipasavyo kwa mujibu wa sheria. Nafikiri Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais amezungumza kwa ufasaha kabisa, sisi kama serikali tutawajibika vipi kusimamia haya na nakuomba sana Mhe. Mbarouk Wadi Mussa usiwe na wasiwasi kwamba serikali haiwajibiki, tunawajibika na sisi sote kama binaadamu tunataka kazi zetu.

Mhe. Salma Mohammed Ali, alitoa mfano akasema kama tunakwenda dede basi dede hiyo mpaka tutakaa kitako. Mimi nataka kumwambia kwamba serikali kwa kweli *speed* yake kali sana, na mwenyewe maendeleo yaliomo mjini na vijijini. Vipi serikali inajitahidi kuleta maendeleo. Lakini kupanga ni jambo moja na kutekeleza ni jambo jengine na usipotekeleza huyaoni matatizo yake, lakini unapotekeleza ndio unaona kumbe nilivyopanga nimekosea mimi, moja, mbili, tatu ndio maana wanapitia kuona tumekwenda vipi na tujirekebishe vipi. Hayo ndio mambo ya mipango lazima ujikosoe mwenyewe.

Kwa upande wa hoja ya maslahi ya Ukaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu utekelezaji wake ni kwamba marekebisho hayo ya mishahara *inshaallah* yatakamilika kabla ya bajeti ijayo ya mwaka 2014/15. Kwa sababu nimearifiwa kwamba jana tarehe 03/02/2014 Mhe. Naibu Spika, watendaji wakuu wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wamekaa pamoja na Wizara ya kazi na Utumishi wa Umma kwa ajili ya kukamilishwa suala hili, sasa tayari linashughulikiwa kikamilifu. Serikali imejiweka tayari na pesa zipo hakuna tatizo Wizara ya Fedha kwa sababu nao wamelibajeti. Naamini kwamba watalifanikisha mapema iwezekanavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa suala la kuwachukulia hatua wahalifu. Jambo hili nalo inafaa lifuate utaratibu wa sheria kwa mujibu wa sheria ya jinai. Katika sheria ya jinai viko vyombo maalumu kwa mujibu wa sheria hiyo vilivyopewa mamlaka ya kuwasilisha na kupokewa ushahidi wake mahakamani.

Kwa bahati mbaya Baraza letu la Wawakilishi pamoja na kamati zake si miongoni mwa ushahidi unaoweza kuchukuliwa kwa ajili ya kuanzisha kesi mahakamani. Taasisi yenye mamlaka kwa mujibu wa sheria ya jinai na sheria ya ushahidi ni kwanza ofisi ya *DPP* au mtu aliyeruhusiwa na *DPP*. Pili polisi, tatu Mahakama au mtu aliyeruhusiwa na mahakama, nne taasisi ya kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi. Kwa hiyo, mambo kama haya tunayaibua na mnaoshauri huyu ashitakiwe afanywe hivi sisi lazima tupate taratibu za kisheria.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kwa ufupi tu niguse yale mambo ambayo Waheshimiwa wengi waliyagusa kama nilivyosema na nitaacha yale ambayo Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Utalii na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati tayari wameshayajibu.

Utendaji wa *CAG* naomba nipokee pongezi zenu kwa niaba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa sifa nyingi sana mlizompa mtendaji huyu pamoja na kitengo chake. Kwa kweli, kazi anayoifanya imeonesha mabadiliko makubwa katika kitengo hiki. Zamani ripoti za *CAG* zinachukua miaka miwili au mitatu au tunadaiwa hatuwasilishi kwa wakati. Leo anatudai yeye yaani anatudai sisi tukamilishe ripoti na maelekezo ili achukulie hatua ipasavyo.

Kwa hiyo, naungana na nyinyi kupokea pongezi kwa niaba ya *CAG* na *inshaallah* watazidi kuleta maendeleo zaidi katika kitengo chake. Bajeti yake mlisema kidogo nayo ina ufinyu naomba kuhakikishia kwamba hili nalo tumelipokea na *review* iwe inafanywa kila mwaka kuona kwamba kadiri shughuli zake zinavyokuwa kubwa basi na yeye bajeti yake anaongezewa.

Jengo la Pemba limeanzwa kujengwa na nimearifiwa kwamba liko ukingoni katika kukamilika. Nayo hiyo ni hatua moja wapo, tulikuwa na kilio kikubwa sana kwa nini hakuna jengo Pemba. Kwa hiyo, nakuhakikishieni Waheshimiwa jengo liko katika hatua ya mwisho kabisa kukamilika. Nafikiri wote mnalifahamu ule ujenzi unaondelea pale Wete, lakini tena wanakamilisha.

Kuna suala zima la kujengewa uwezo kitengo cha *PMU* katika kila wizara ili kwenda sambamba na sheria ya manunuzi kama ilivyoelekezwa katika sheria namba 9 mwaka 2005. Nafikiri tunakiri kwamba kweli tunahitaji tuwe na *staff* ambao wanaweza kufanya kazi vizuri ya manunuzi, si kazi ambayo kila mtu tu anaiweza. Nitatoa mfano kama *ZAWA* nimejuilishwa kwamba katika miradi yao pale basi wameajiri watalamu wawili baada ya kutangaza nafasi zile za kazi ili wao waweze kufuatilia vizuri mambo haya ya manunuzi.

Miradi ya *World Bank* sote tunafahamu taratibu zao zilivyokuwa ngumu na wengi tu tunashindwa mara nenda mara rudi mpaka mradi unafika mbali sana na manunuzi hayajafanyika. Kwa hiyo, lazima tupate wataalamu ambao wanafaa kufanya kazi hizi za manunuzi. Kama mapungufu hayo yanatokezea basi tunayachukua tuone kwamba tunawarekebisha vipi wataalamu wetu. Lakini namshukuru sana Mwenyekiti haya yeye kafanya *observation* nzuri tu kwamba kulikuwa na matatizo hayo kwenye serikali za mitaa pamoja na wahasibu huko, lakini sasa kidogo kidogo tumeweza ku-*post* wataalamu wenye sifa na matumaini yetu kwamba wanafanya kazi vizuri.

Hesabu za mwaka kufungwa nimeshalizungumza hilo na zaidi nataka kusema kwamba hii inaonesha vipi tunafuata maelekezo yenu ya kamati.

Kulikuwa na suala zima la ukodishwaji wa vituo vya Petroli kule Pemba. Tumelifuatilia suala hili na tumegundua kuwa hili suala kwa sasa liko Mahakamani. Sasa tunajaribu kuwashauri hawa wakuu wa vituo ambao wamelipeleka lile suala tuone kwamba wanaliondoa mahakamani ili tuweze kuzungumza huku uraiani na tufikie mahala pazuri. Kwa sababu ni sisi wenyewe kwa wenyewe, na hakuna sababu huku wanasema wanapeleka mahakamani lakini huku vituo vinafanya kazi nao wanapata mapato.
Kwa kweli inabidi tuzungumze, tuzungumze tuelewane halafu tulitafutie ufumbuzi wa kudumu kabisa. Kweli limechukua muda mrefu nakiri kabisa Mhe. Naibu Spika.

Madeni ya taasisi za Umma hasa vikosi. Nimezungumza kweli wanadaiwa mengi ya madeni haya yaliwahi kuorodheshwa na yalilipwa na Wizara ya Fedha. Lakini sasa yakajitokeza mengine. Yalipojitokeza mengine haya tukawaambia kuwa hasa sasa ni dhamana yenu. Kwa sababu *OC* mnatiliwa na

mnapanga wenyewe. Sasa kama *OC* mnatiliwa na mnapanga wenyewe tena vizuri Wizara ya Fedha mpange wenyewe mtume wenyewe kwa mujibu wa pesa yenu. Sasa hili nazungumza nao na tunawajuilisha na wanatufahamu sasa ni vigumu.

Kodi za ardhi sipendi kuzungumza hili Mhe. Waziri muhusika amelizungumza kwa ufasaha kabisa na nimekubaliana naye kwamba kweli ipo *variation*, na agizo la Wizara ya Fedha wakati hata Mhe. Waziri mwenyewe wa Fedha katika ripoti yake ya juzi tu alizungumza kwamba au anakiri kwamba inafaa itungwe kanuni maalumu itakayomuwezesha waziri kuweka *rate* mpya za ulipaji. Kwa hiyo ni suala la kanuni ambazo zitamsaidia waziri ku-*review* mara kwa mara zile kodi.
Pia, kumejitokeza suala la kodi pungufu za ardhi hilo nalo Mhe. Waziri muhusika amelizungumza sitaki na mimi niliongezee.

Makusanyo machache ya kodi. Siku moja nakumbuka pale Waziri wa zamani Mhe. Moh'd Hashim, alikuwa anazungumza na mtu anamwambia usifikiri kila mtu anaweza kwenda na kuikusanya kodi ina utaalamu wake. Sasa ushauri wenu wa kutumia vyombo hivi vya *electronic* tumeupokea na ndio unaotumika hivi sasa na tuna *plan* kuanzia kwenye mahoteli ya kitalii kuona vipi vyombo hivi tunaweza kuvitumia, lakini *inshaalla* hata ikija mambo ya *E-Government* zile takwimu ambazo pengine taasisi moja inazitumia kama *airport* tutawasaidia watu wa *ZRB* itamsaidia mtu mwengine, kwa wale ambao watakuwa wanatudanganya itakuwa rahisi kuwakamata. Kwa hiyo, ushauri wenu wa matumizi ya *electronic device* tumeuchukua.

Suala la *One stop centre* Mhe. Naibu Spika, hili nalo Waheshimiwa wengi wamelichangia na kwa kweli lazima tukiri kwamba kuna udhaifu ambao kama mliouona nyinyi na serikali nayo kidogo hairidhishwi. Kwa sababu kama tumemkusudia muwekezaji aende akamalize mambo yake katika *ZIPA*. Halafu kule hakuna watu ambao wanaweza kumaliza mambo pale pale wanatoka waende ardhi, wanatoka waende mazingira, wanatoka waende kwengine kwa kweli haipendezi, wenzetu tunaambiwa kuwa wa Rwanda huko Singapore ndani ya masaa tu kwenye kituo kile kile anamaliza yote.
Sasa kwa nini na sisi tusiyafanye hayo, tulianza vizuri lakini kama nilivyosema kwenye utendaji yanatokea matatizo. Sasa kama serikali tunalichukua hili tuone tutafanya *review* ya haraka sana juu ya utendaji wa *ZIPA* tuone mapungufu haya mliyotwambia kwa kweli hayatatokea tena. Ni kweli maana yake wakati mwengine mpaka wale wawekezaji wanakuja na hamu mpaka hamu inamtoka.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma, alizungumzia mambo ya jana ya uporo yale. Lakini nafikiri haya tena ilivyokuwa yeye ni Mwenyekiti wa

Kamati ya Viongozi Wakuu na Mwenyekiti wa Wenyeviti naamini kwamba watapata muda mzuri wa kuzungumza na taasisi husika kuona kwamba yale mambo tunayamaliza.

Lakini sisi kama upande wa serikali nataka kusisitiza tu kwamba kusiwe na dhana kama Uwanja wa Ndege kuna mtu yeye anaendesha mambo yake kimwenyewe mwenyewe tu si kweli. Tutoe dhana hiyo na sisi kama kuna ushauri wa mapungufu basi ushauri huo tuko tayari, ili tuone vipi tunayarekebisha, hii ni taasisi yetu.

Lakini ninachoomba sana yale maendeleo yaliyopatikana pale Uwanja wa Ndege lazima hilo tukubali, sivyo palivyokuwa pale. Hata ukusanyaji wa mapato sivyo ulivyokuwa, kuna mabadiliko makubwa sana.

Sasa tutoe maoni yetu tuboreshe vipi pale tulipoachia ndio utendaji. Alizungumza hapa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais siku zote unapotenda unajikwaa, na ukijikwaa ndio una-*check step* yake, kumbe *step* ilikuwa *wrong*. Basi ule utendaji wa Kiongozi Mkuu wa Uwanja wa Ndege kwa kweli lazima na yeye tumpe sifa yake kwa kiwango fulani. Kama kuna mapungufu kama binadamu basi hayo tutakaa nae na tunayapokea tuone anajirekebisha vipi.

Mhe. Makame Mshimba nae tunamshukuru sana kuna mengi alizungumza ya upande wa ardhi. Lakini kama walivyozungumza Waheshimiwa Mawaziri walionitangulia kwamba *ZRB* wanayo ripoti yao ya ardhi, *CAG* anayo ripoti yake, Kamati Teule ya Mhe. Ali Mzee Ali, nae alitoa ripoti ya ardhi, *PAC* nayo imeelezea mengi sana.

Sasa ukizichukua hizi ripoti nne na nyenginezo, hizi tukimpa Mhe. Ramadhan, pamoja na timu yake, naamini kama alivyosema ndio yumo anaogelea sasa hivi, kwa hiyo tumsaidie. Kwa hiyo, mimi naungana na nyinyi kwamba haya mapungufu mliyoyaona ni kweli. Na sasa kila mmoja ndio anaona ule uzito au umuhimu wa ardhi nchini mwetu. Kwa sababu ardhi ni ndogo na haikui, lakini kadiri tunavyoitumia matumizi yamekuwa makubwa sana.

Nafikiri Mhe. Asha Bakari Makame na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk pia, walizungumza suala la Mpapindi kule, tukafuatilia safari za yule bwana za usiku usiku tu na ulipaji wake wa kodi tuone kwamba kweli mambo yake yanakwenda vipi. Tutashirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Vijana tuone. Lakini tukiwa na uhakika kidogo kwamba hizo safari zake za usiku usiku kweli ana mambo mliyoyataja anakwenda nayo sambamba, basi kama Serikali tutajitahidi tuone yanakwenda vizuri.

Mhe. Asha Bakari Makame, ulizungumza suala la daftari la kudumu. Kwa kweli kila Wizara imeagizwa hivi na tunashukuru na kuripoti kwamba tumeshaanzisha. Kila Wizara sasa imeshafanya *inventory* au wanaendelea kufanya *inventory* za mali zote kwa kila taasisi halafu tuziweke kwenye daftari.

Suala la madeni ya umeme namshukuru Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati amezungumza vizuri sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, pamoja na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, mlikereka sana na upotevu wa mabilioni ya fedha. Na mlijaribu ku-*quote* hasa upande wa ardhi na kwengineko. Sasa hizi *specific issues* ambazo mumezitaja kwa taasisi kama hizi, haya nasema ndio mambo ya kuyafanyia kazi. Hapa ndio pa kukaa vizuri wakapelekewa wenyewe, jamani kuna kesi hii na hii tunataka muwajibike mtupe majibu ndio kuyafanyia kazi yenyewe. Lakini kwa leo tutoe maelezo hapa, sisi itakuwa vigumu sana, hata Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, mwenyewe kwa kweli amesema hilo tumwachie. Na *Inshaallah* hatutofika huko kama tulivyosema kwenye bajeti, hayo tutayaweka sawa na tutayaleta hapa.

Mwaka jana mimi nakumbuka maagizo yote yale nilifanya kitabu maalum Maagizo ya Kamati ya *PAC*. Kwa hiyo, na wenzangu naamini watafanya utaratibu mwengine, lakini tutaya-*address* tuyashughulikie kabla hatujaingia kwenye bajeti. Tunataka bajeti yetu Mhe. Salmin Awadh Salmin, ipite vizuri ndio tunapanga. Sasa tena mkija mkizuia zuia bajeti kidogo, pesa ukipunguza, tutapata tabu. Hii bajeti yetu sote sio kama tumeifanyia Wizara ile husika tu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kama nilivyosema nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri walionitangulia kujibu zile baadhi ya hoja kwa upande wao. Lakini zile ambazo kama nilivyosema mumehisi kwamba labda hatukuzijibu msione tumeziacha. Zile tunazichukua tutakwenda na kawaida yetu ripoti za *CAG* au ripoti kama hizi za *PAC* tunazijadili hata kwenye Baraza letu la Mawaziri. Na kila Waziri na Makatibu Wakuu wote wapo, na kila mmoja anatakiwa ajibu. Sasa nakuonesheni ile *seriousness* ya Serikali iliyonayo juu ya suala hili. Msifikiri kama Waheshimiwa wengi walivyosema tunachukua tunakwenda kuweka kwenye *shelves* na tunachoma moto. Si hivyo, tunawajibika ipasavyo kweli kweli.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo naomba sasa na mimi niunge mkono hoja ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ili tupate kuyafanyia kazi maelekezo yote waliyotupa. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika): Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena naomba nitumie fursa hii nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kusimama mbele ya chombo chako hiki na kufanya majumuisho juu ya Ripoti ya Kamati ambayo tuliiwasilisha asubuhi ya leo.

Lakini kabla sijasema chochote Mhe. Naibu Spika, kama kawaida yangu nisikitishwe na watendaji. Ripoti hii ya Kamati ya *PAC* kama inavyojulikana inahusu taasisi zote za umma. Na kwa mara hii kwa kweli hatukuweza kumaliza ripoti yote, lakini kuna maeneo ambayo Kamati iliyafanyia kazi. Tulitaraji sana kwa yale maeneo ambayo yaliguswa na ripoti leo, tulitamani sana na ingelifurahisha sana kama watendaji wale wangelikuwepo katika ukumbi huu, ili kusikiliza maneno ya Kamati na kusikiliza michango ya Wajumbe.

Kwa sababu ni wao wanaofika mbele ya Baraza hili kila mwezi wa sita kuomba fedha na vivyo hivyo walitakiwa leo katika kuelezea namna gani wanavyozitumia fedha zile waje wasikie. Maana yake wasiwe ni rahisi tu kunyoosha mkono katika kupokea, lakini pia walitakiwa waweze kuwajibika katika masuala mazima yanayohusiana na kero zao.

Kwa kitendo chao hiki kwa kweli hawalifanyii haki Baraza la Wawakilishi, na wala hawawafanyii haki wananchi wa Zanzibar ambao ndio wanaochangia pesa mbili mbili. Pesa mbili mbili zile zikarundikana ndio wakapewa na Baraza hili kwa ajili ya kutengenezea shughuli zao. Kwa hivyo, naomba Mhe. Naibu Spika, niiambie Serikali kupitia kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais suala hilo alirekebishe. Kwa sababu tulitegemea sana wale Makatibu wa zile Halmashauri ambao kwa mujibu wa sheria wao ni ma-*accounting officer* katika Halmashauri zao, hoja zimewagusa na kwa vyovyote vile leo walikuwa wawepo pale.

Tulitegemea vile vile na Wakuu wa Vikosi, mliona namna gani fedha zinavyotumika vibaya katika vikosi. Na kwa sababu wao ndio ma-*accounting officer* katika vikosi vile ilikuwa nao wawepo ili wasikilize michango hii. Kutokuja ni namna nyengine tunayosema kwamba Taasisi za Serikali wanalidhalilisha Baraza la Wawakilishi mfano wake hai ndio huu.

Mhe. Naibu Spika, niwashukuru Wajumbe wote waliochangia Ripoti ya Mdhibiti. Jumla yao walikuwa ni Wajumbe 16. Lakini kabla ya kwenda kwenye michangio naomba nianze na ile hatua ya kwanza ambayo ilikuwa ni mapitio au yatokanayo na utekelezaji wa ripoti ya mwaka jana.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana Baraza la Wawakilishi lilinipa heshima ya kwenda kuhudhuria katika kikao cha Kamati za *PAC* za *Commonwealth.* Na moja kati ya zawadi niliyokuja nayo ni ripoti niliyoiwasilisha ambayo niliiweka kwenye *kit* moja nikampa Makamu wa Pili wa Rais na moja nikampa Waziri wa Fedha. Niliitoa ripoti ile ili kutoa uzoefu wa wenzetu katika Mabunge mbali mbali ya *Commonwealth* namna Serikali inavyotakiwa i-*respond* na kujibu mapendekezo ya Kamati za *PAC.*

Nilifikiria kwamba Serikali iliyachukua yale na kuyafanyia kazi kwa nia ya kujifunza, lakini uwasilishaji wa leo mapendekezo ya Serikali, utekelezaji wa Serikali kwa kweli imenidhihirishia kwamba inawezekana Serikali makaratasi yale waliyaacha katika madroo ya viti vyao, hawakuyafanyia kazi. Na kama wangeliyafanyia kazi basi leo Serikali wasingelikuja na ripoti ile ya utekelezaji.

Maana yake ukichukua maelezo yaliyotolewa na Serikali katika kujibu utekelezaji wa ripoti iliyopita, kwa kweli inanivunja moyo sana binafsi kama Mwenyekiti wa Kamati. *Tabaan* hata Wajumbe nao watavunjika moyo sana. Kwa sababu mwaka jana ripoti yetu ni hii, maelezo ya Mwenyekiti ni haya hapa.

Mhe. Naibu Spika, katika majumuisho yangu mwaka jana nilisema kwamba iwapo Serikali laitani wangelijifungia na kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyomo kwenye ripoti ingelikuwa ni kazi ya mwaka mzima. Kwa sababu ripoti ilijaa mapendekezo ambayo mimi binafsi naamini na Wajumbe wanaamini kwamba yale ni maeneo ya msingi sana katika Serikali kuyafanyia kazi. Lakini bahati mbaya, kwamba majibu ya Serikali leo kwa Kamati hii nyeti ambayo yanatokana na matokeo ya kazi ya ofisi nyeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, kwa kweli Serikali haikufanya jambo ambalo tulitarajia.

Mhe. Naibu Spika, sitaki nitumie muda wako mwingi, kwa mfano katika ripoti ya mwaka jana katika kipengele kile cha sababu za uvujaji wa mapato. Sababu za uvujaji wa mapato kama tulivyozieleza Mhe. Naibu Spika, Kamati ilitoa mapendekezo nane. Mapendekezo nane yale kama kila moja utalichukua na kulichambua na kulifanyia kazi, mimi niliyekuwa sikusoma uchumi wala mambo ya hesabu naweza nikatoa darasa katika kila pendekezo moja.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na yote lakini Wawakilishi tuko makini sana katika masuala haya. Sasa hivi unavyoona pengine Wawakilishi elimu zao ndogo na pengine watendaji elimu zao kubwa ndio mnafika pahala mnadharau Wawakilishi, si kitu kizuri. Kwa sababu katika mapendekezo nane laitani ningelikuwa na nafasi ningelikwambia sasa hivi moja baada ya jengine

na halafu tuangalie namna ambavyo kila mmoja atakubaliana kwamba hili ni la msingi. Kwa hivyo katika suala la uvujaji wa mapato tulitaja mapendekezo nane, ni bahati mbaya majibu ya Serikali haikutaja hata moja.

Lakini la pili, Mhe. Naibu Spika, kuna suala zima la udhibiti wa mapato. Ile ya kwanza ilikuwa ni uvujaji wa mapato, lakini ya pili, ilikuwa ni udhibiti wa mapato. Kamati ilitoa vile vile mapendekezo nane katika namna gani Serikali inaweza ikazuia suala zima la udhibiti wa mapato.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suala la ukiukwaji wa taratibu za malipo na manunuzi. Katika kipengele hicho tulipendekeza namna ya kuimarisha udhibiti wa ndani. Na katika kipengele hicho Kamati yangu ilitoa mapendekezo matano.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na hoja ile ya ufungaji wa mahesabu. Na katika kipengele kile tulitaja mashirika na taasisi kumi na moja kwa majina, kwamba taasisi hizi zina matatizo ya muda mrefu hazifungi hesabu na bahati mbaya sana ni taasisi za fedha. Kuna *PBZ*, Shirika la Meli, Shirika la Utalii, Shirika la Umeme, Shirika la Maktaba, *SUZA*, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambapo fedha zote za wafanyakazi wa nchi hii zinakusanywa pale.

Shirika la Bima, Baraza la Manispaa, *ZRB* wenyewe ambayo ndio chombo chenye kukusanya. Vyombo hivi havifungi mahesabu. Na Waheshimiwa tunapofika pahala chombo kikiwa hakifungi mahesabu adhabu pengine na tafsiri yake inakuwa ni kubwa zaidi. Ni sawasawa na biashara iliyokuwa ya mfanyabiashara huuza tu lakini yeye haandiki anachouza au anachonunua. Mali bila daftari Mhe. Said Ali Mbarouk, anaweza akatumalizia.

Kwa hiyo, tafsiri ni kubwa sana kwa taasisi kutokufunga hesabu. Na Baraza hili lilitoa maagizo kwamba tunahitaji ufungaji wa mahesabu ya miaka mitatu, kuanzia mwaka 2009/10, 2010/11 na 2011/12. Tulitaraji kwa vyovyote vile Serikali itujie na majibu hapa namna gani wametekeleza pendekezo hilo lakini mpaka leo ni kimya.

Mhe. Naibu Spika, jengine kwa sababu ripoti ya mwaka jana ilihusiana na miradi ya *TASAF*, nashukuru kuwa angalau imegusiwa katika ripoti hii ya leo. Lakini katika hilo Kamati yangu ilipendekeza mapendekezo sita na ni ya msingi sana kwa sababu mfuko wa *TASAF* ule unaendelea kuwepo katika nchi yetu. Kwa hivyo, tulitaraji angalau Serikali ingelikuja na majibu ya kuonesha namna gani tunaweza kudhibiti fedha zile ambazo nchi yetu inapata kupitia mkopo wa Benki ya Dunia.

Mhe. Naibu Spika, jengine tulipendekeza kuhusiana na suala zima la ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Katika suala zima la udhibiti wa fedha katika matumizi ya miradi ya maendeleo Kamati yangu ilitoa mapendekezo matano.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ni suala zima la matumizi ya mali za umma. Tulielezea kwa undani hata matumizi ya vyombo vyetu vya moto na vitu vyengine, namna gani kwa kweli tunaweza tukaokoa fedha nyingi sana iwapo tutadhibiti na tutakuwa na uangalifu sana kuhusiana na suala zima la matumizi ya mali za umma.

Mhe. Naibu Spika, katika kipengele hicho vile vile Kamati yangu ilitoa mapendekezo nane. Na ni kama nilivyosema Mhe. Naibu Spika, kwamba tulitaraji leo Serikali ingelikuja na majibu. Lakini hata yale majibu yaliyokuja ni majibu ya jumla jumla tu, ni majibu yaliyokuwa hayana mashiko. Kwa sababu unapotwambia tunachokitarajia kwamba jamani tuna suala hili, kwa vyovyote vile tunatarajia kwamba utekelezaji wa suala hili umefika katika kiwango hichi, na bado kiwango hichi hatujatekeleza na hatujatekeleza kwa sababu gani.

Sisi sote ni watu wazima, kwa hivyo ikiwa kama ni watu wazima na tunawawakilisha wananchi wa nchi hii tunatarajia hata jibu linalotoka katika Baraza hili kwa kweli liwe ni jibu lililokwenda shule, la kijitu kizima. Lakini mnapokuja na karatasi hoja zinakuwa nyingi, mapendekezo yanakuwa ni mengi, lakini utekelezaji unakuwa ni wa kutupa tupa tu. Kwa kweli mnakuwa Serikali hamtufanyii haki. Na leo nataka niseme kwa upole sana, kwa sababu nadhani kwa vyovyote vile Serikali ni sikivu na kuna siku itasikia katika hili.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, majibu ya Serikali yanakuwa si ya kuridhisha sana katika hili. Na tunaiomba Serikali mara nyengine, mwaka kesho tukijaaliwa na Mungu, kila hoja tunayoitoa katika Baraza hili, kila mapendekezo tunahitaji kupata namna gani Serikali imetekeleza kwa kiwango gani, na kiwango gani hakijatekelezwa na kwa sababu gani.

Mhe. Naibu Spika, na hili ni la msingi sana, na utekelezaji wa Serikali katika mapendekezo ya Kamati ni msingi sana. Kwa sababu Kamati hii inafanyia kazi mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Chombo pekee ambacho kwa mujibu wa Katiba yetu kinatambulika. Na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anafanya kazi takriban kwa mwaka mzima. Kamati nayo kupitia Baraza inapata muda kwa ajili ya kuzifanyia kazi ripoti.

Kwa hivyo, kwa uzito ule ule wa chombo kile cha Mdhibiti, na kwa uzito ule ule wa mapendekezo ya Kamati, ndio tunapotarajia kwamba na Serikali nayo angalau itenge muda kwa ajili ya kushughulikia utekelezaji wa mapendekezo

ya Kamati ya *PAC.* Vyenginevyo, Ofisi ya Mdhibiti itakuwa ni Ofisi ipo ipo tu haina kazi yoyote, anafanya kazi kubwa, nzuri, lakini *output* yake ambayo ni yatokanayo na kazi ya Kamati itakuwa kwa kweli haina maana yoyote.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutaja masikitiko yangu kuhusiana na utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati, sasa naomba niende moja kwa moja katika kuwataja wale waliochangia ambao kama nilivyosema awali wachangiaji walikuwa 16;

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando
4. Mhe. Abdulla Juma Abdulla
5. Mhe. Asha Bakari Makame
6. Mhe. Salma Mohammed Ali
7. Mhe. Farida Amour Mohammed
8. Mhe. Fatma Mbarouk Said
9. Mhe. Salmin Awadh Salmin
10. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
11. Mhe. Mohammed Haji Khalid
12. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
13. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo
14. Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati
15. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
16. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora (Mhe. Kaimu Waziri wa Fedha)

Mhe. Naibu Spika, michango ya Wajumbe iligawika sehemu tatu. Kwanza ilikuwa ni pongezi kwa Kamati kwa kazi nzuri waliyofanya. Kwa niaba ya Kamati naomba nizipokee pongezi hizo na pongezi tuzirudishe kwa Waheshimiwa Wajumbe. Kwa sababu pongezi hizi zimetupa moyo sana na zikatufanya sasa tukaze buti zaidi katika kushughulikia kulinda na kuchunga fedha za wananchi.

Michango ya pili ya Wajumbe ililenga katika kukazia yale ambayo Kamati ilieleza. Waheshimiwa Wajumbe kwa wingi wao takriban waliunga mkono hoja, waliunga mkono maelezo ya Kamati na kwa kweli tunashukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya tatu, kuna hoja mbili tatu ambazo naomba kidogo na kwa ufupi sana nizitolee maelezo. Kwanza hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma alitutaka tuliangalie zaidi eneo lile la Hoteli ya *Crystal* na nataka nimuahidi kwamba Kamati italifanyia kazi suala hili.

Mhe. Naibu Spika, kuna hoja ambayo aliizungumza Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwamba hakuna umuhimu wa wawekezaji kuwaongezea muda. Ni kweli ni hoja ya msingi kwa sababu wawekezaji walioshindwa na ukaona kwamba wawekezaji wameshindwa, kuwaongezea muda ni tatizo. Lakini sisi kama Kamati tulisema angalau hoja si kushindwa na ukamkatia mkataba wake, hoja ya msingi ni unayemkatia mkataba unampa nani.

Kwa sababu katika uchunguzi wetu tuliona watu wengi walifutiwa lakini wakapewa watu wengine nao vile vile wakashindwa. Kwa hiyo, tunaweza tukafika pahala tukawafutia, tukawapa wengine wakashindwa tukawafutia, ikawa sasa mchezo ni huo huo.

Mimi nadhani kwa sababu sote tunakubaliana hapa Serikali ilipotoka kipindi cha nyuma, na kwa vyovyote vile sasa hivi tunaona Serikali inajipanga kidogo katika suala hili. Hoja ya msingi kwa upande wetu ni kuipa muda Serikali katika kusimamia. Kinachoonekana hapa kulikuwa hakuna usimamizi.

Kwa hivyo, hoja ya kwamba tuwape muda angalau miezi sita au mwaka mmoja haikuwa na maana yoyote, isipokuwa tunaipa nafasi Serikali kujipanga vizuri zaidi katika kusimamia. Kwa sababu maeneo yakiwa yapo madalali watakuja tu,. Sasa eneo hili tunaiomba Serikali tuwe makini sana.

Kwa sababu kilichoonekana na ndio maana Kamati ikapendekeza lazima hata sera zetu tuziangalie upya. Inaonekana tunavyofikiria wengi, Serikali inakaribisha wawekezaji kwa maana ya kwamba kuna watu wana uwezo wanakuja kuwekeza lakini sivyo ilivyo. Anafika pahala mtu wa *ZIPA* anatwambia huja wawekezaji vishuka ambao hawana chochote, wakifika ndani hapa wakaanza kusumbuka sumbuka kutafuta pesa, na Serikali sasa ndio inayowatafutia mitaji kama ilivyoelezwa hapa.

Sasa ikiwa mzungu anatoka Italy huko mnakuja kumtafutia nyinyi pesa hapa, kashindwa. Badala ya kuwatafutia watu wa Makunduchi na Tumbatu huko waliokuwa hawana chochote! Kwa hivyo, ni suala sasa la ku-*review* sera zetu hizi za uwekezaji. Inaonekana tunafungua milango hii kuingiza kila mtu, kitu ambacho ni hasara kubwa sana kwa Serikali. Leo mwekezaji kaja na shati yake tu hapa, maana yake pesa imtafutie Serikali ya Mapinduzi, haiwezekani.

Jengine hoja kama ilivyoelezwa na ufafanuzi umetolewa kuhusiana na *jet*. Matumizi ya *jet* ni ghali sana, lakini nataka niwaambie hakuna *jet* hata moja inayolipia. Na kama ilivyoelezwa bia unapoinunua katika hoteli iliyopo juu, tofauti sana na bei ambayo inapatikana kwengine. Kule unanunua bia, maana yake kunywa bia katika maji kuna raha zake Waheshimiwa. Kwa hiyo, kule

kila kitu ni ghali. Sasa tulitegemea matumizi yale ya *jet* kwa kweli yatie fedha nyingi katika Serikali, hakuna hata shilingi inayoingia watu wanajijengea tu, ovyo ovyo.

Mhe. Naibu Spika, suala la Mhe. Farida Amour Mohammed, kuhusu Mkoa wa Kaskazini. Mhe. Farida Kamati inapofanya kazi hufuatana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Inapofika pahala watendaji wakaipinga ile hoja ya Mdhibiti huwa tunatoa nafasi kwa Mdhibiti kuilinda hoja yake. Inapofika pahala Mdhibiti akawa kashindwa kuilinda hoja yake, ndipo pale tunapomwambia Mdhibiti sasa, ama hoja ile Kamati huiondosha au humwambia kwamba afanye utafiti zaidi ili Kamati aipatie hoja ya mashiko.

Kwa hiyo, hoja hii tulipoishughulikia Kaskazini kule ikaonekana kwamba hoja hii ni ya Mkoa wa Kusini Pemba. Tulipokwenda Mkoa wa Kusini Pemba kukawa hakuna jawabu ndipo pale niliposema basi tunampa fursa Mdhibiti ili ajiandae vizuri zaidi aipatie maelezo ya ziada kama kuna maelezo ya ziada. Kama hakuna sisi tunafuta hoja. Kwa hivyo, hicho ndio kisa cha msingi kumtaka Mdhibiti aishughulikie hoja ile.

Mhe. Salmin Awadh Salmin, na hoja yake ya Shirika, ni kweli kwamba ni kitu cha tishio na naomba Serikali iwe makini na suala hili. Tusione ni suala la masihara. Suala la umeme Zanzibar ndio maisha ya watu. Ikiwa *TANESCO* wameshafika pahala na kusema kwamba watakata umeme ni lazima Serikali kwa kweli iwe katika hali ya tahadhari. Na Shirika kama mtazifuatilia hizi ripoti si mara nyingi kugusia ripoti za Shirika la Umeme. Kwa hiyo, Mdhibiti mwenyewe yupo pale juu anasikia tunamuomba akaze buti sana katika kuliangalia Shirika la Umeme.

Mhe. Said Ali Mbarouk, Kamati katika kukishughulikia kile chumba cha chini ya habari tulikusanya wadau wote. Tukawakusanya watu wa Mazingira Pemba na watu wa *ZIPA.* Tukatoka kule hoja hatukupata kwa sababu kulikuwa na malumbano watu wa Mazingira wakatwambia sisi hatujui chochote. Tukawaleta Unguja na tukaja tukaikusanya timu ya Unguja. Ninachotaka kukwambia kwamba mradi ule unasemekana ni mradi wa majaribio. Na hadi sasa watu wa Mazingira wenyewe wametwambia wao hawajatoa hati ile ya Mazingira, hawajatoa ruhusa. Mbele ya watu wa *ZIPA* walituthibitishia hilo. Kwa hiyo, bado suala likawa kwamba kwa sababu walisema ni mradi wa majaribio na ukifeli pale wataurudisha kule kule, sijui wapi kwenye visiwa vyako. Kwa hiyo, hilo suala bado liko hivyo.

Na chengine ikiwa ni kweli mtu mmoja kwa siku anatumia dola 1,500 kwa kulala chini ya maji, sasa hoja si ughali wa chumba. Hoja ni kwamba mwananchi wa Makangale anafaidika kiasi gani? Maana tusiambiwe tu

chumba ni ghali. Haya mimi nina pesa zangu nitakwenda chini ya maji, lakini mwananchi wa kawaida Mzanzibari anapata kiasi gani katika dola 1,500 za kila siku.

Utafiti unaonesha kwamba hakuna kinachopatikana. Sasa ikiwa hakuna kinachopatikana kupitia kodi au hata ile *land lease*, kwa sababu kile kijiboti sijui kichumba hakikuelea tu, kile kinagusishwa na ardhi, ni matumizi ya ardhi. Kwa vyovyote vile ndio Sheria ya Ardhi inavyozungumza. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, ni kusema kwamba mwananchi wa kawaida au Serikali yetu haipati chochote kupitia chumba kile.

Mhe. Naibu Spika, nataka uniruhusu kwa muda huu mchache uliobakia nieleze changamoto. Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu kwa kweli pamoja na Baraza kwa ujumla tuna changamoto. Na changamoto kubwa inayotukumba ni kujirudia rudia kwa hizi ripoti. Ripoti zinakuwa kila siku zinajirudia, pengine leo utakuta taasisi hiyo hiyo hoja ni ile ile. Sasa hili ni tatizo, angalau tungeliona kwamba mwaka huu hoja ile haijitokezi tena. Lakini tunachokishuhudia ni kwamba hoja ile ile, kwa taasisi ile ile inaendelea kujirudia, hayo si maendeleo ya ukaguzi.

Maendeleo ya ukaguzi ni yale unayotatua tatizo moja likaisha, ukenda kwenye tatizo jengine hapo ndio panaonekana pana ile *improvement* katika ukaguzi. Na katika hili mimi nadhani sasa wakati umefika kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, na sisi Baraza kufika pahala kwa kweli kuyapanga haya mambo katika utaratibu wake. Taasisi yoyote ambayo itaonekana na hoja ile ile kwa mara moja au mara mbili, kwa vyovyote vile inafika wakati lazima tuchukue hatua. Kwa sababu hapo ikiwa ni uongozi wa Wizara, au ya kitu chochote maana yake hiyo imeshindwa. Hatuwezi tukafanya siku zote, miaka yote tukafanya kazi hiyo moja kwa taasisi moja tu, maana yake *management* imeshindwa.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyengine tunayoipata ni kwamba sasa hivi Baraza linaanza kuekwa nyuma na Mdhibiti. Kama tulivyoeleza mara hii tuna ripoti mbili katika mkono na hatukuweza kuzimaliza. Ninashukuru sana Wajumbe wako, kila mjumbe aliyekuwa akisimama kwa kweli alikuwa akielezea umuhimu wa kamati kuongezewa muda.

Leo tuna ripoti, lakini bado ripoti zile mbili hatujazimaliza. Kesho na keshokutwa Mdhibiti kwa *speed* yake hawezi akaturuhusu sisi, tutafika pahala kwa kweli Baraza na kamati zitakuwa zipo nyuma. Mdhibiti anakwenda kwa kasi sana. Tatizo lile la *back log* litajirudia si muda mrefu Mhe. Naibu Spika. Na sasa hivi Baraza lako kwa jinsi lilivyojenga uelewa kila mara huagiza Mdhibiti, fanya uchunguzi huu.

Sasa hivi Mdhibiti ana ile kesi ya *ZMA* ambayo ninadhani wakati wowote ataileta Barazani. Sasa hivi kuna yale mambo ya viinua mgongo ambapo ninafikiria wakati wowote na kuna ukaguzi wa kawaida. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hili ni la Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, kwa sababu yeye ndiye muhimili wa Baraza hili. Lakini zaidi Mhe. Naibu Spika, mamlaka hayo unayo katika kiti chako. Tusifike pahala Baraza likaekwa nyuma, mutaturudisha miaka nyuma miaka mingi sana, wakati sasa kila kitu kinakwenda mbele.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyengine tunayoipata ni hii kuambiwa kwamba ripoti hizi za kamati haziwezi kuwa ni ushahidi Mahakamani. Nalo hili ni tatizo, kwamba ikiwa Mdhibiti anafanya kazi kubwa ya kufanya ukaguzi, *PAC* inafanya kazi kubwa, lakini mwisho wa ripoti hizi haziwezi hata kusimama katika Mahakama zikawa kama ni ushahidi, maana yake nini? Mimi ninadhani Mhe. Naibu Spika, kuna haja sasa ya kuzipitia hizi sheria zetu zinazohusiana na kesi za jinai. Kuzifanyia mabadiliko ili ifike pahala ushahidi unaopatikana kupitia ripoti hizi pamoja na ripoti ya Mdhibiti, ichukuliwe kama ni sehemu ya ushahidi katika Mahakama. Vyenginevyo tutakuwa vyombo hivi kazi zake hazina maana yoyote. Maana yake mtu atafanya akipenda, hakupenda kwa kweli ndio basi tena. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, katika dhana hiyo ya utekelezaji wa utawala bora, serikali inatakiwa iwajibike. Na serikali inawajibika katika sehemu mbili tu. Serikali katika chombo hiki cha wananchi au serikali inawajibika kupitia watu wanapopigana mitaani huko au serikali inawajibika kupitia uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, njia hizi mbili sio nzuri sana kwa kweli. Serikali kuwajibishwa na wananchi kupitia uchaguzi sio nzuri sana. Maana yake labda nyote viongozi wa serikali muwe hamna kitu kichwani. Maana yake wananchi wanawaambia Wawakilishi wake, hamtaki kusikiliza, wananchi wanachukua hatua yao siku ya uchaguzi. Hiyo sio nzuri, kwa viongozi wenye busara kama serikali yetu hii tuliyonayo, si jambo zuri sana tukasubiriana kwenye uchaguzi.

Na vile vile, si vizuri sana kusubiri mpaka watu wakaripuka mitaani. Maana yake leo tunakwenda hivi kwa sababu pengine wananchi hawajajenga uelewa mzuri. Lakini leo asubuhi tuliripoti kwamba kuna bilioni mbili, bilioni tatu zinapotea tu. Unachotegemea katika nchi nyengine sasa hivi watu wanasubiri kwa mapanga hapo nje.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninadhani njia sahihi ya serikali kuwajibika ni katika chombo hiki kwamba kila tunalolizungumza na kukubaliana, serikali ichukue

jukumu la kuyatekeleza kwa ukamilifu hayo. Hiyo ndio njia ya kistaarabu na huo ndio uungwana katika suala zima la kidemokrasia. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nilitoa changamoto kwa serikali, kwamba serikali haikusanyi si zaidi ya asilimilia 25 ya mapato hasa katika maeneo ya uwekezaji. Nilitarajia hapa wataalamu watakuja kuniambia si kweli. Mhe. Naibu Spika, ninarudia kwamba nilitoa changamoto kwamba serikali haizidi asilimia 25 ya makusanyo yake katika sekta ya uwekezaji. Nilitaraji kwamba wataalamu wa hesabu watakuja kuniambia si kweli, na nilijitayarisha kwamba wakija kuniambia si kweli tupambane katika hoja. (*Makofi*).

Kwa hivyo, hoja yangu inasimama pale pale kwamba serikali haikusanyi kodi. Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Wajumbe. Kwanza tumshukuru Mhe. Mwenyekiti kwa majumuisho yake mazuri sana, yenye utaalamu na yamezama kwa kina kabisa katika utekelezaji. Changamoto za serikali, serikali ipo imesikia na changamoto za Baraza kwa niaba ya Spika mimi nitazichukua hasa kuhusu muda wa kufanyia kazi ripoti hizi. (*Makofi*).
Baraza litajitahidi kwa hali na mali ili *CAG* asituache nyuma ili twende naye sambamba.

Baada ya maelezo hayo niwahoji Waheshimiwa, wale waliokubali ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya *PAC* kwa mwaka 2013/2014 wanyooshe mikono, waliokataa.
Waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

(Saa 1.45 usiku Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 5/2/2014 saa 3.00 asubuhi)